**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**Kikao cha Arobaini na Tatu - Tarehe 28 Juni, 2014**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu!

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2014**
**(*The Finance Bill, 2014*)**

*Kusomwa mara ya Pili)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Ahsante sana, jana sikuwa nimewataja watu lakini naona ambao walioomba na ninataka kuwapa nafasi. Yupo Mheshimiwa Pauline Gekul, Mheshimiwa Pauline Gekul, utaanza.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi ili niweze kutoa maoni yangu kuhusu Muswada wa Fedha ambao uko mbele yetu. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya njema na kuwepo siku ya leo katika Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, nina mambo machache yafuatayo ambayo ningependa kuchangia na Waziri aweze kuyachukua. Jambo la kwanza nazipongeza Kamati zote mbili, Kamati ya Bajeti na Kambi ya Upinzani kwa mawazo mazuri ambayo wameweza kuyatoa kuhusu Muswada huu na niombe tu Mheshimiwa Waziri na timu yake waweze kuyapokea na kuyafanyia kazi.

Lakini kubwa zaidi ambalo hata mwaka huu wa fedha kitu ambacho Serikali imeendelea kuangalia ni kuhusu *turnover* kwa wale wafanyabiashara wadogo wadogo katika kuwatoza kodi ambayo *turnover* yao ni chini ya shilingi milioni 4 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 35 katika Muswada ambao umeletwa na Serikali hili limeweza kuonekana na ni jambo ambalo limeanza mwaka jana na naona sasa Serikali imeendelea kuliendeleza. Ombi langu niombe kwa sababu hili bado limeendelea mwaka jana tunakumbuka tuliwasamehe kuwatoza kodi wale Mama Lishe, Boda boda, Bajaji na wale ambao biashara zao ni ndogo na *turnover* zao hazifiki shilingi milioni 4 kwa mwaka.

Niombe Mheshimiwa Waziri atoe mwongozo mapema sana kwa *TRA* katika Kanda zote na mikoa yote ili hawa wafanyabiashara wadogo wadogo wasisumbuliwe kwa sababu wao wanakosa mwongozo. Hili nililisemea hata katika hotuba zilizopita kwamba hata wale wafanyabiashara wangu wa Babati, walikuwa wanapata shida sana na *TRA* kwa sababu *TRA* iliwatoza.

Kwa mfano wale wa Bajaji na Ghuta walitozwa shilingi laki moja moja na Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, alilisema kwamba hili hapana, wakati anahitimisha hotuba yake.

Lakini pia limeendelea mwaka huu. Niombe tu Wizara ya Fedha basi muwapatie *TRA* mikoani mwongozo ili hawa watu wasisumbuliwe kwa sababu tuliwasamehe waendelee na waweze kukuza mitaji yao. Naamini hili Waziri amelichukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, ni kuhusu ada za leseni. Kwa kweli hapa kidogo pana tatizo. Tunafahamu hata mwaka jana hili halikuweza kutekelezwa vizuri na mimi binafsi nisingekubaliana na hii hali ya Serikali kuendelea kutoza leseni *as if* ni sehemu ya pato kwa kila mwaka ni *source of income*.

Niishauri Serikali kwamba waachane na hili kwa sababu hawa watu wanaomba tu kibali cha kuanzisha biashara unapofanya kibali kama ni chanzo cha mapato kila mwaka kwamba kila Juni 30 wawe wamelipa, kila mwaka biashara ni ile ile haijabadilika mimi naona kidogo tunawasumbua wafanyabiashara.

Kwa hiyo Kamati ya Bajeti ya Mheshimiwa Andrew Chenge, imeshauri kwamba ikiwezekana basi walipe kwa miaka 3 au 2 anapumzika badala ya kila mwaka anakwenda kulipa. Lakini tunazungumzia suala la *logic* kwamba huyu mtu ameomba kibali cha biashara, kama ni kibali biashara haijabadilika.

Ni kwa nini sasa kila mwaka Serikali inamtaka aombe kile kibali kwa *rate* ambayo kila mwaka kupitia *Finance Bill* Serikali inapanga ni kiasi kipi yaani kiwango kipya, utakuta kwamba hata hicho kiwango sio *constant* yaani leseni za biashara zinabadilika kila mwaka na inasababisha usumbufu mkubwa sana na Kambi ya Upinzani wamesemea hili kwamba hizi kodi zinawafanya hawa wafanyabiashara waone kwamba ni usumbufu. *By the way* wanalipa kwa *TRA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia Halmashauri wanapokusanya tuna Serikali mbili hapa, kuna Serikali Kuu lakini kuna Serikali za Mitaa maana yake huyu mwananchi ambaye ameanza biashara yake japo tunawahamasisha wengi wafanyabiashara ili tukusanye kodi ambayo kidogo haiwaumizi lakini anatumikia mabwana wawili kwa wakati mmoja.

Kama tumekubaliana hao watu kwenye Serikali za Mitaa basi ijulikane wanalipia huku lakini *TRA* wasiende kuwachukulia tena fedha kwa sababu sasa wanafanya biashara.

Ni vizuri basi hili suala leseni ambacho ni kibali cha biashara Serikali ikafikiria ikaacha na ikatumia maoni ya Kamati ya Bajeti na ikatumia maoni ya Kambi ya Upinzani wakati wamelisemea vizuri sana hili kwamba kwa kweli hili halistahili kwa wafanyabiashara wetu. Naamini Serikali wataufanyia kazi huo ushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije kwenye jambo la tatu. Suala la tatu ambalo napenda kulisemea ni suala la haya magari chakavu. Serikali jambo ambalo limelifanya mwaka huu kwamba yale

magari ambayo ni kuanzia miaka 10 wamefanya ni asilimia 30. Wakati mmeleta ule Muswada wa kwanza ilikuwa asilimia 25.

Mimi najua lengo la Serikali ni zuri sana lakini haya magari Watanzana ndiyo wanayanunua na Waziri wa Fedha nilimwambia kwamba mwaka jana ulitenga *estimate* ya shilingi bilioni 2 katika hili.

Lakini mkakusanya *more than* asilimia 320 shilingi bilioni 7 mkakusanya kupitia hizi asilimia ya magari kuanzia miaka 10, hii inaonyesha nini? Inaonyesha Watanzania bado wanaagiza magari haya kwa sababu hawawezi kununua magari mapya.

Kwa hiyo binafsi ninaona kama Serikali ina-*justify* kutoza haya magari asilimia kubwa ili kuepusha magari mabovu yasiingie kwenye nchi yetu basi wangekubaliana na maoni ya Kambi ya Upinzani na maoni ya Kamati ya Bajeti kwamba asilimia hii ya magari mapya kodi inayotozwa ipungue kwa sababu wamesema kabisa kwamba magari mapya yanayoingia nchini Serikali inatoza kodi zaidi ya asilimia 63 ya gari lenyewe walivyonunua.

*Imagine* asilimia 63 Serikali imeshaweka kodi nyingi hivi huyu Mtanzania atanunuaje gari jipya na Kamati ya Bajeti imeshauri vizuri kwamba basi hii asilimia ya magari mapyaipungue mpaka asilimia 30. Mimi ninapojiuliza hivi haki iko wapi kama kwenye magari chakavu mmepandisha asilimia mpaka 30, magari mapya asilimia 63 za kodi zenu ni kwa nini mnamuumiza huyu Mtanzania, Waheshimiwa Mawaziri?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi niiombe Serikali wakubaliane na mapendekezo ya Kamati ya Bajeti kwamba shusheni kodi ya magari mapya halafu mki-*justify* kwamba sasa magari mabovu tunayazuia kwa sababu yanaharibu mazingira tunaweza kuwaelewa. Leo nani anaweza kuwaelewa mnaendelea kupandisha mnapata kodi nyingi sana mnavuka asilimia mpaka 320 mkijua Watanzania wataagiza tu kwa sababu huku mmewabana kwa asilimia 63 hawawezi kuagiza.

Mheshimiwa Spika, lakini mwisho kwa sababu ya muda *TRA* wanafanya jambo ambalo silo kabisa. Utakuta gari halijapita barabarani kwa miaka miwili mitatu, minne liko *grounded* nyumbani kwa mtu *TRA* wanakwenda kulichukua hilo gari, wanakwenda kutoza fedha kwa miaka mitatu (3) hii inatoka wapi. Mheshimiwa Waziri tuambie. Mimi kuna watu wangu wa Babati pale magari yao hayajapita barabarani kwa muda mrefu miaka mitatu, minne *TRA* wanaenda wanalikokota wanalipeleka kwao wanatoza fedha.

Mheshimiwa Waziri hebu tuambie kama hajatumia *motor vehicle* tunalipa hizi barabara na mnapandisha kila siku mwaka mzima sijatumia barabara yenu kwa nini, gari langu limepaki nyumbani liko *grounded* wafanyabiashara hao wamiliki wa magari Babati wanalalamika sana utakuta mtu labda ni mjane amefiwa magari kayapaki hapo lakini TRA wanayachukua, wanamtoza kodi huyu mtu kwa sheria ipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri utuambie. Kwa kweli ni jambo ambalo hatuwatendei haki Watanzania kwa sababu sidhani kama sheria inaruhusu kwamba sijatumia, halafu mnachosema huku mnasema *okay* gari lako lilikuwa gereji basi tuletee *certificate* ya gereji. Hivi ni gereji zipi za Watanzania ambazo zinatoa *certificate* kwamba gari lilikuwepo gereji ……...

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Muda wako umekwisha.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Murtaza Mangungu, atafuatiwa na Mheshimiwa Aeshi.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kukupongeza wewe binafsi kwa uendeshaji mzuri na ubunifu ambao umetuletea katika mfumo wa uendeshaji wa Bajeti na *Circle* ya Bajeti katika Bunge letu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti ambayo umeiteua kwa kweli wanastahili pongezi na sifa za kutosha kabisa kwa umakini na umahiri mkubwa katika utendaji wao wa kazi.

Binafsi nimeshiriki vikao vichache na Kamati ile kwa kweli imejaa watu ambao wana umakini na wana nia ya dhati katika kuiongoza na kutetea maslahi ya wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Waziri pamoja na Manaibu wake tunaweza tukasema ni wapya lakini upya wao umeonyesha kabisa kutakuwa na mabadiliko chanya kutokana na uwezo mkubwa wa utendaji na uwasilishaji ambao tumeuona.

Pia tusiwe wezi wa shukrani Kamishna mpya wa *TRA* pamoja na Makamishna wenziwe kama Mzee Kasela pale tumeona wanafanya kazi kubwa sana kwa sababu tumeshirikiana nao kwenye vikao na wameonyesha umakini mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, lakini kwanza kabisa pamoja na mambo mengi mazuri ambayo yamefanyiwa marekebisho katika kipindi hiki lipo tatizo kubwa sana kwa Watanzania wengi na huu ni ugonjwa ambao wote tunao.

Hakuna jambo ambalo linatugharimu na litaendelea kutugharimu kama hatutobadilika mpaka mwisho wa dunia hii. Tatizo hili la ugonjwa huu ni nidhamu. Ikiwa hatutojenga mfumo wa kuwa na nidhamu, nidhamu ya ufanyaji kazi, nidhamu ya matumizi maana Watanzania tuna ugonjwa hata wa nidhamu ya kulala tu. Sasa pamoja na mambo mengi ambayo yamefanyiwa marekebisho.

Je, tumejiandaa kiasi gani kuwa na nidhamu katika utekelezaji wa haya. Hili ni tatizo ambalo ningeiomba Serikali na Watanzania wote tukubaliane kwa ujumla kwamba nidhamu yetu katika mambo mengi iko chini sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwenye Muswada huu ambao umewasilishwa yapo mambo mengi sana ambayo yamefanyiwa kazi na mimi naamini kabisa tunaweza tukafanikiwa. Lakini la kwanza nawaomba sana wenzetu wa Mamlaka ya Mapato wafanye jitihada za kila namna kuondoa vile vikwazo ambavyo vinaonekana vinakwamisha ukusanyaji wa mapato. Waongeze *efficiency* yao ya ukusanyaji wa mapato.

Lakini mwaka huu tunawapa changamoto kubwa yale maeneo yote ambayo tumeyaainisha kwamba ni vyanzo vya mapato kwenye Bajeti ijayo tunataka kwamba viwe vimeshaingizwa na ikiwezekana kama havitafanyiwa kazi kwa haraka basi Waziri uje kutuletea tuje kuidhinisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, lingine suala la bandari. Bandari yetu ni kweli ilisainiwa mikataba ya kufanya kazi masaa 24. Lakini tunawaomba kwamba ukusanyaji mapato mara nyingine tunawakatisha watu tamaa kwa sababu mizigo mingi inakuja inakaa muda mrefu bandarini na hawa watu wanaingia kwenye hasara.

Kontena zinakaa pale zina-*accumulate storage* matokeo yake hata kama akienda kulipia huo mzigo na kuutoa hautoweza kupata faida ile iliyokusudiwa na mara nyingine inachangia kuongeza mfumuko wa bei kwa sababu mfanyabiashara anapoagiza mali anategemea kuuza ndio akusanye mapato yake.

Kwa hiyo, mara nyingine hii inachangia. Kwa hiyo, nawaomba waongeze uharakishaji wa utoaji mizigo na kufanya kazi masaa 24 ndani ya Bandari yetu ya Dar es Salaam na Bandari ya Tanga pia ielekee huko ili kazi iweze kufanyika, mizigo iingie na tunufaike na hii *geographical location* ambayo tuko nayo, kwamba nchi za jirani kama Rwanda, Congo, Burundi, Zambia na Malawi waje kutumia Bandari yetu na tutaongeza mapato ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lipo jambo moja ambalo Mawakala wa Forodha wamelilalamikia na nampongeza sana Dkt. Mwakyembe kwa ziara zake za Congo na Burundi kuongeza matumizi ya Bandari yetu kwa nchi hizo ambazo tumezizunguka. Lakini kubwa kwamba Mawakala watakuwa wanakosa kazi katika Bandari hizi za kwetu. Sasa nilikuwa naiomba Serikali tuangalie mfumo mzuri isiwe mtu ana-*log document* kule moja kwa moja anaweza kuja kutoa mzigo huku.

Kwa hiyo, tunaweza tukahamisha kazi za Watanzania kutoka katika maeneo ya nchi yetu na yakaenda nchi nyingine. Kwa hiyo hili naamini kabisa Serikali mtaweza kulifanyia kazi kwa sababu tayari mlishakuwa mmefanya vikao kadhaa. Kwa hiyo nawaomba tu muendelee na hilo.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Uwekezaji Sura ya 38 imefanyiwa mabadiliko ambayo ni chanya kabisa. Lakini pamoja na uwekezaji huu huwa tunautegemea uwe na matunda yaliyokusudiwa. Naiomba Serikali sasa ipitie upya aina ya uwekezaji na kuwahamasisha Watanzania waelewe nini maana ya uwekezaji.

Mitaji ya uwekezaji Watanzania wengi wanayo kwa sababu mpaka leo hii haiwezekani mfanyabiashara aagize kontena 10 ambazo zina thamani ya zaidi ya Dola milioni moja wakati bidhaa anazoweza kuagiza kutoka nje anaweza kuzalisha hapa ndani.

Lakini hii pia itachangiwa na Serikali kuangalia ni kwa jinsi gani tunaweza tukapunguza gharama za uzalishaji ndani ya nchi yetu. Gharama za uzalishaji nchini zimekuwa ni kubwa na ndiyo maana wafanyabiashara wengi wanaona ni bora kuagiza kutoka nje kulikoni kuzalisha hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tumekubaliana kwenye Kamati kwamba Miswada ile ambayo inahusu *VAT* tutakuja kuijadili kwenye Bunge linalofuata pamoja na bidhaa nyingine. Kwa hiyo hilo tunawatakia kila la kheri. Kwa uchache hayo ndiyo niliyokuwa nayo na naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, sasa Mheshimiwa Aeshi atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Shekifu.

**MHE. KHALFAN H. AESHI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Awali ya yote naomba niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri pamoja na Kamati ya Bajeti kwa kazi kubwa na nzito wanayoifanya. Mimi kwanza naomba niunge hoja mkono, lakini la pili nilitoa ushauri tu kwamba mimi ni miongoni mwa watu ambao wanapinga.

Mheshimiwa Spika, naungamkono hoja ya kufutwa misamaha ya kodi. Mheshimiwa hili mimi linanipa taabu kweli. Hawa watu wanaomba misamaha ya kodi kidogo ni wadanganyifu

sana. Ukiangalia kwa haraka haraka tu utakuta hata hawa wananchi kwa kweli wanafahamu kwamba leo hii mahoteli mengi kila baada ya miaka 5 yanabadilishwa majina, hii ni ukwepaji mkubwa wa kodi.

Kwa hiyo nikuombe tu Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Waziri hii misamaha midogo midogo hii kwa kweli ingefutwa. Ni wizi wa wazi na wananchi sasa hivi wanaelewa.

Kwa hiyo, niwape moyo kwamba Wabunge wengi tupo pamoja na nyie na hata mwaka jana, mwaka juzi tumekuwa tukipiga kelele nyingi sana kuhusu misamaha ya kodi isiyokuwa na tija.

Mheshimiwa Spika, ipo miradi mikubwa ambayo ninaona kabisa ina tija ndani ya Taifa letu kwa mfano mradi mkubwa reli hii hata akija muwekezaji akasema anaomba msamaha wa kodi mimi kabisa ninaunga mkono apewe msamaha kwasababu italeta faida kubwa sana kwa wananchi kuliko misamaha midogo ambayo ninaamini kabisa kuwa ni watu wajanja wanaitumia misamaha hii ili kukwepa kodi.

Leo utaangalia kampuni nyingi hata za mitandao kila baada ya miaka mitano inabadilishwa majinamfano ni *Airtel* mwanzo ilikuwa *Zain* inakuja kila baada ya miaka mitano wanabadilisha majina, lingine ni *Serena Hotel* ilikuwa inaitwa *Moven Pick*, *Sheraton* leo hii inaitwa ni *Serena Hotel* hii yote ni ukwepaji wa kodi.

Kwa hiyo, mimi ninasimamia Mheshimiwa Waziri ninaamini kabisa kuwa ninyi ni wataalam na mna watalaam wengi na wamepitia kwa undani zaidi. Kwa hiyo sisi kama Wabunge asilimia kubwa tunaunga mkono kwa niaba ya wananchi na kwa niaba ya Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuipongeza tena Wizara kwa kuangalia wakulima hususani wa Mkoa wa Rukwa na Katavi kwa kupitisha malipo yao niwaambie tu wananchi wangu kwamba Serikali imeandaa malipo na muda siyo mrefu wale wote waliokuwa wamekopwa na wanaodai watakuwa wamelipwa. Ninaomba niipongeze sana Wizara kwa kusikia kilio change.

Vilevile niwaambie wafanyabiashara kule Sumbawanga, hususan wasafirishaji kwamba hela zao zimetengwa, siyo muda mrefu sana watakuwa wamepata fedha.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ninaomba nikushukuru kwa kusikia kilio changu na wananchi wangu sasa hivi wanakusikia na wafanya biashara wote wa Mkoa wa Rukwa na Katavi wanakusikiliza. *(Makofi)*

Mimi bado ninapata taabu kidogo kwa hawa wakulima wetu hususani wakulima wa wa mahindi.

Siku mbili zilizopita hizi, nimeona kabisa kuna watu wanalilia kuwa pamba ilipiwe na Serikali ushuru wa Halmashauri ambao ni 5% na Serikali kwa haraka haraka imekubali. Sasa ninataka kuuliza hivi zao la pamba ni pamba peke yake ndiyo inayolisha Tanzania nzima?

Mbona sisi wakulima wa mahindi hatupati bahati kama hii. Sisi Halmashauri inahitaji kodi kwa wakulima, inachukua ushuru kwa wakulima, lakini hatupewi ruzuku.

Sasa ninataka kujua hivi hawa wakulima wa pamba wanaweza kulima pamba bila ya chakula?

Sisi tunalima mahindi, tunalima mpunga, lakini endapo bei itashuka hatufidiwi. Lakini wakulima wa pamba wanafidiwa. Mwaka jana, wakulima waliolima mpunga wamepata hasara kubwa sana, lakini Serikali sikuiona hata siku moja kuliongelea hili, kusema kuwa tutawafidia wakulima wa mpunga. Lakini pamba, pamba, pamba nini pamba kila siku? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ni fidia tupewe wote, kama ni ushuru Serikali imeamua kuwalipia wakulima tuwalipie na wakulima wetu wa Sumbawanga, wakulima wa Rukwa, na wakulima wa Katavi. Sisi tukilima tunalipa ushuru, sisi tukilima tukaenda kuuza *SGR* pale, Serikali ya Halmashauri ina *charge* ushuru. Lakini nyie pamba mnawalipia. Sasa hizi kodi tulipiwe Watanzania wote, siyo wakulima wa pamba peke yao.

Mheshimiwa Spika, hili mimi limeniuma sana, hebu liangalieni hili, kwa nini pamba? Bei ikishuka mnafidia wakulima sisi mahindi yakishuka wapi. Lakini cha kushangaza mahindi yanapouzwa kwa Shilingi 70,000/= Sumbawanga hawa watu mnawapelekea kwa shilingi 5,000/=. Hivi jamani hawa watu ni malaika?

Kila kitu wenyewe mimi ninaumia sana. Lakini mkumbuke kabisa bei ikiwa shilingi 70,000/= Sumbawanga kuna wakulima ambao hawawezi kununua mahindi hayo kwa bei hiyo. Kwa hiyo, kama ikitokea msamaha huo wa shilingi 5,000/= basi na wakulima wa Sumbawanga nao wauziwe kwa shilingi 5,000/=.

Kwa hiyo, hili Mheshimiwa Waziri ninaomba mliangalie sana, msiweke upendeleo wa sehemu moja. Ukiangalia reli upande mmoja, barabara upande mmoja, meli upande mmoja hivi huku kwenye Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini tumelogwa? Kila kitu wao, kila kitu wao na leo hii mmepitisha Bajeti ya bilioni nane tunawalipia ushuru, tunalipia Halmashauri zao kutoka Serikali kodi ya wananchi wote kwa ujumla hapana hili hatuliungi mkono. Mimi ninasema kabisa kama ni hivyo basi tukubaliane wote na watu wa Sumbawanga wasamehewe ushuru huo ili tuwe na Wizara.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa kuliongelea hapa ninawapongeza Mawaziri ila niwaambie kwamba tuko pamoja lakini mkumbuke kwamba mmeandaa kusema leo hii wakulima mtawapa mikopo, hususani wakulima wa mahindi Mkoa wa Rukwa, Katavi, Mbeya na Ruvuma.

Lakini mkumbuke mwaka jana 2013 vikundi hivi vilijiandaa vizuri lakini havikupata mkopo walioahidiwa. Wakaenda kujiandakisha wakajisajili na akaunti wakafugua, lakini mikopo hawakupata sasa tunakwenda msimu mpya mmejiandaa vipi? *(Makofi)*

Mmesema mtawakopesha wakulima. Je, hawa wakulima wameshaunda vikundi vyao isiwe *story* ya mwaka jana na kama haiwezekaniki basi tuwaambie wakulima wajiandae kama mwaka jana. Lakini sasa hivi wakulima wetu wamejiandaa na vikundi vipo vingi. Lakini hakuna hata kikundi kimoja ndani ya Jimbo langu la Sumbawanga Mjini, kilichopata mkopo mwaka jana 2013.

Japokuwa tulipitisha Bajeti hapa tukasema tumeandaa fedha tutawakopesha wakulima sasa nikuombe Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Waziri kwamba hili linalokuja mwaka huu msimu wa kilimo na sisi Wabunge tutaandamana wa Nyanda za Juu Kusini tushikamane. Tuwatetee wakulima wetu kama wengine wanavyoshikamana kuwatetea wakulima wao tusilale tuamke sasa ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya mmesikia sasa ninamwita Mheshimiwa Dkt. Henry Shekifu, atafuatiwa na Mheshimiwa Ismail Rage.

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii lakini pia niipongeze Kamati ya Bajeti kwa kazi nzuri. Ni wageni katika kazi hii, lakini wamefanya kazi nzuri. Nimpongeze Waziri, pia ameonyesha ukomavu mkubwa. Ni mgeni katika Wizara hii hasa kama Waziri, lakini ameweza kutuletea Bajeti ya matumaini. *(Makofi)*

Mimi nianze kuchangia kwa kushauri. Kwanza nimwombe Waziri wakati wa kujibu hoja zetu, katika fedha ambazo zimewekewa wigo nimesikia zaidi kwa upande wa elimu, lakini sijasikia wigo wa fedha za umeme vijijini na maji vijijini. Ninaomba wigo huo utambulike na uonekane kwa sababu ni vitengo muhimu na ni lazima vipewe umuhimu. Lakini pia nimsisitizie Waziri kutenga fedha na zitoke mapema kwa ununuzi wa mazao kupitia *SGR* ni muhimu sana, mwaka jana walifanya vizuri kwa sababu fedha zilitoka mapema na manunuzi yalifanyika na wananchi walifurahi na hata *inflation* au mfumuko wa bei umepungua kwa sababu manunuzi yalikuwa makubwa. *(Makofi)*

Nimwombe tena Waziri aongeze kwa mwaka unakuja maeneo ya msamaha wa kodi kwenye Kilimo. Wenzangu wengi wamezungumzia, hili mimi sihitaji kurudia ni vizuri *spare parts,* vifungashio katika shughuli zote za Kilimo ziangaliwe vizuri. *(Makofi)*

Ninamshukuru kwa kupunguza mianya ya msamaha wa kodi, jambo hili liendelee liwe ni la kudumu kila mwaka tu *review* na tuletewe orodha kama Wabunge tujue. Nimwombe sana suala la magari chakavu. Ni kweli nia ni nzuri, lakini wananchi kwa njia moja au nyingine hawalifurahii sana. Nia ni nzuri, ninaomba tuendelee kama ilivyopendekezwa kupunguza kodi ya magari mapya. Hii ndiyo itawezesha Watanzania wengi kuwa na uwezo wa kununua magari.

Nishauri tena kuwa *TRA* ni kweli kuna matatizo kwa magari machakavua ambayo yanapaswa kulipia *road licence,* siyo halali gari halitumiki. Halitumii barabara wewe unam-*charge* miaka miwili, mitatu huko nyuma mimi ninafikiri hizi ndiyo kodi zenye utata ambazo hazimsadii mwananchi ni kumletea kero, kodi hizi tuzifute.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninashauri sana suala hili liangaliwe na Waziri ikiwezekana toa maelekezo kama gari kweli lina uthibitisho halitumiki basi hakuna sababu ya kulilipisha ule muda ambao halikufanya kazi. Suala lingine ni suala la kuwasilisha Sheria ya Bajeti, ninaishauri sana tulipoanzisha Kam

Lakini leo tunaona manufaa yake, tunaomba tupewe muda ambao Sheria ya Bajeti itakuja tujadili mambo kwa kina na kwa mujibu wa Sheria siyo hii ya kubahatisha tunakamatana, hatujui mipaka ya Kamati, hatujui uwezo wa Bajeti na haki zake, ninaomba hili lieleweke vizuri.

Niwapongeze pia kwa kutoa adhabu kwa wafanya biashara wenye kuleta bidhaa feki hili ni jambo jema na tunaomba liendelee. Ni kweli kwamba ni muhimu kuliona hili mimi nina mfano mdogo tu. Mjukuu wangu alienda kuchomwa sindano za huu ugonjwa wa watoto wadogo Surua. Kwa bahati mbaya alichomwa *vaccine* ambayo siyo sahihi.

Sasa inavyoonekana hiyo *batch* iliyokuja sasa hivi Dar es salaam liko tatizo, watoto wanaougua surua ni wale walichomwa sindano ya kuzuia surua. Lakini sasa wanaougua surua wana miaka miwili, mitatu, minne kwa sababu vile viatilifu havikukamilika au hakikuwa sahihi. Mateso makubwa na ni hatari kwa afya za watoto wetu. Ninaomba liangaliwe kwa kina suala hili.

Ninaomba na sijui lakini kuna suala la kuweka ushuru kwenye fenicha za hapa ndani nchini samani za hapa nchini. Hili halijatamkwa vizuri sijaliona, lakini ni vizuri Waziri akaligusia hii

ni sehemu ya ajira muhimu sana kwa vijana. Ni muhimu kama kodi ile ipo iondolewe ili vijana waweze kujiajiri na kwa sababu tuna matatizo ya ajira ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, niko eneo lingine la kulinda viwanda vyetu. Mimi ninakubaliana na suala hili na kwa kweli viwanda vyetu ni lazima vilindwe. Lingine ambalo ni muhimu ni kuondoa au kuongeza kodi kwenye maeneo ambayo ni ya *concentrates.*

Mimi ninatoka maeneo ya kulima matunda. Hatuwezi kushindana na wale wanaoleta *concentrates* kutoka nje kama hazina bei kubwa ndiyo leo unaona unaambiwa kwamba kuna juisi ya machungwa au juisi ya papai, au juisi ya guava, lakini haya hayalimwi hapa nchini, na hayatoshi kuendesha kiwanda mwaka mzima. Utakuta ni mengi yanatoka wapi? Sasa viwanda vyetu haviwezi kuhimili ushindani kama kweli *concentrate* hizi zinakuja bila ya kuangaliwa.

Mwisho, nishauri suala la *SGC* ninafikiri nimelizungumzia. Nimezungumzia pia *TRA* kulipisha magari kwa kweli hili jambo ni baya sana na zana za kilimo pia nimezungumza nitoe shukrani zangu kwa Bajeti nzuri ya kuleta matumaini na ninaomba sana sasa tuzingatie.

Mwisho kabisa ni nidhamu ya matumizi na nidhamu ya kukusanya ni ukweli kuwa tunahangaika mapato hayatoshi lakini mimi ninaamini kuna mianya mingi ya kodi zinazokusanywa udhibiti wa kodi hizi siyo mkubwa sana ninaiomba Serikali hasa Wizara itoe adhabu kali kwa wale ambao hawakusanyi kodi na ambao hawalipi kodi *TRA* wadhibitiwe watumishi wale wahakikishe wanaleta kodi na kodi ile iwasilishwe Serikalini,

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo ninakushukuru sana ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninakushukuru Mheshimiwa Spika, na ninapenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri na timu yake pamoja na Kamati ya Bajeti kwa kazi nzuri waliyoifanya.

Mheshimiwa Spika, ningependa kujikita katika maeneo kama matatu au manne moja nilitaka kuelewa tu kuwa Waziri atakapokuja kufanya *windup* ushuru wa bidhaa hasa katika vinywaji baridi vya soda na maji ambapo vilikuwa vimewekewa kodi ya shilingi tisini na moja imeshuka mpaka shilingi hamsini na tano, ningependa kujua Watanzania wa kawaida watafaidika vipi je vinywaji hivi na vyenyewe bei itashuka ili wananchi wa kawaida na wenyewe wafaidike?

Lingine katika hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha alitangaza kufuta msamaha wa kodi ya mapato kwa wamiliki wa *Cassino Gamming Games.* Lakini kitu kinachonishangaza mimi kidogo nimewahi kwenda kutembea mimi siyo mchezaji wa kamari lakini nimekuta wanaocheza mchezo huu ni watu wenye uwezo mkubwa sana kuliko Watanzania wa kawaida. Katika Muswada huu mliotuletea sasa mnafuta hiyo kodi sielewi Mtanzania wa kawaida anafaidika na kitu gani hapo.

Kwa hiyo nilikuwa ninaomba tuwe waangalifu sana ndiyo dhana inayokuja ile ya kwamba kuna watu wanafanya *lobbing* labda au nini inatia wasiwasi na inavunja hata heshima ya Bunge letu kwasababu haingii akilini *Cassino* ni mchezo unaochezwa na watu matajiri na wale wanaocheza *Cassino* ni watu ambao wana fedha zao halafu hawanyi hata kazi kazi yao wao ni kwenda usiku kwenye *Cassino,* wanacheza kamari wakimaliza asubuhi anafanya hesabu ya hasara aliyopata kwenye *Cassino* au faida aliyopata.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa ninaomba Mheshimiwa Waziri unishawishi nikubaliane na wewe kwa nini umeifuta hii. Kuna jambo moja limeongelewa hapa la hawa wanaolipa kodi ya mafuta wanaomba waruhusiwe siku arobaini na tano.

Mheshimiwa Spika, mimi hata sielewi ni *formular* gani inatumika hapo kwa mtu ambaye anachukua mafuta akae nayo, auze baada ya siku arobaini na tano ndiyo akalipe ushuru wa forodha.

Mimi ninaomba *I am challenging every body in this House* anipe mfano wa nchi moja Duniani ambayo inafanya biashara hii ya mafuta. Kwa mtu wa mafuta anatoa kwanza mafuta, anakwenda kuuza, anakaa baada ya siku arobaini na tano. Aje aniambie, ninaomba nitolewe mfano. Pengine wenzetu mnaiga kutoka nchi fulani mtuambie ni nchi gani? *(Makofi)*

Kwa sababu unapotaka kununua mafuta kuna *only two ways of payment.* Kwa wale wanaotoa mafuta kwanza utalipa kwa kitu kinachoitwa *Telegraphic Transfer (TT)* ambayo ni *cash 100%* au utalipa kwa kufungua *LC Irrevacable Confirmed Letter of Credit* ndiyo unapata mafuta. Ukishapata mafuta yanakuja Tanzania eti Serikali ya Tanzania ni matajiri kiasi hicho wanawaachia wanawakopesha wauza mafuta siku arobaini na tano.

Mimi ninaona kwa kweli hapa siafiki hata kidogo sidhani kama tuko *serious* katika mpango huu. Katika suala hilo hilo la mafuta ninapenda kumpongeza Waziri, umethubutu kujiondolea mamlaka ya kutoa mafuta nilikuwa jana *library* sijawahi kuona Waziri hata mmoja wa Fedha tangu tumepata uhuru aliyesema yeye hataki *it's a record* umeingia kwenye *Guiness Book* lazima niseme ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninavyofahamu mimi utaratibu wa Bajeti Serikali inaanza kutengeneza Bajeti mwezi wa kumi kabla ya kuja Bungeni mwezi wa nne na Serikali inafanya vikao mbalimbali na wadau mbalimbali pamoja na wafanya biashara hao hao. Wao inawachukua muda mrefu sana mimi ninaomba labda kwa sababu mwaka huu tulikuwa tuko *very tight* na mambo ya Katiba ili tutendewe haki na sisi tupate angalau muda wa kutosha wa kuweza ku *scrutinise* Bajeti hii kuliko utaratibu uliopita.

Ninasema hivyo kwa sababu wenzetu inawachukua muda mrefu wanafanya *consultation* na watalaamu wao muda mrefu halafu sisi tunakuja hapa kwa kipindi kifupi tu tunafanya mabadiliko ambayo kwa kweli wakati mwingine yanaweza kuleta madhara katika Bajeti yetu.

Kwa mfano, sielewi nitamwomba Mheshimiwa Waziuri atakapokuja nimeambiwa kwamba Muswada wa *VAT* umekuwa *suspended* mpaka hapo baadaye ninataka kujua.

Je, kuna *effect* yoyote katika Bajeti hii? Kwa sababu sisi tunajua tunataka tupate trilioni 19 hasa fedha zetu za maendeleo. Sasa kwa hii *VAT* kuondolewa isijadiliwe hivi sasa kwa hii *VAT* kuondolewa isijadiliwe hivi sasa haitadhuru Bajeti yetu? Nitamwomba Mheshimkiwa Waziri wakati unapokuja kufanya *windup* utueleze.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ningependa kukupongeza Mheshimiwa Waziri kwa kufuta msamaha wa kodi ya zuio *(Withholding Tax),* kwenye mapato yanayotokana na ukodishaji wa ndege kutoka nje ya nchi.

Kwa kweli hii mimi nina kupongeza sana kwa sababu tulichokuwa tunafanya hii *withholding tax*, mnapowasamehe hawa wakubwa, wasipolipa hapa Tanzania, kule kwao wanakwenda kulipa. Kwa hiyo, sisi kazi yetu hapa tunayofanya ni ndege hizo zinafanya kazi Tanzania lakini *withholding tax* zinakwenda kulipwa nchi za nje. Kwa hiyo, hatupati chochote, nchi za nje ndiyo wanafaidika.

Baada ya kusema hayo, kwa leo sina mengi napenda tena kuunga mkono hoja hii. Mwisho kabisa nawapongeza sana wasaidizi wetu ambao leo wamevaa makoti yao mazuri sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Si mavazi yao! Una matatizo! Waheshimiwa sasa nilisema nitamwita Mheshimiwa Mussa Zungu Azzan, atafuatiwa na Mheshimiwa Halima James Mdee. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. MUSSA ZUNGU AZZAN:**Mheshimiwa Spika, na mimi nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi.

**SPIKA:** Watu wakichelewa na ya kwao hayapo.

**MHE. MUSSA ZUNGU AZZAN:** Mheshimiwa Spika, lakini kabla sijaanza mchango wangu nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake wawili, niipongeze Kamati ya Bajeti inayoongozwa na Mtemi Andrew John Chenge, kwa kazi kubwa sana ambayo amefanya.

Lakini nichukue nafasi vilevile kumpongeza Kamishna Mkuu mpya wa *TRA* pamoja na Makamishna wenzake wote anaofanya kazi nao kwa kazi nzuri wanayoifanya na *they can do better* kwa ushirikiano ambao watapeana na Serikali na Wabunge, pamoja na wananchi kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nilitaka nizungumze suala neno moja linaitwa MKURABITA ambalo ni sera ya Serikali ambao Watendaji wengi wa Serikali hasa Halmashauri hawajui. MKURABITA ni mkakati wa kurasimisha biashara ambazo siyo rasmi za wanyonge na nchi nyingi sana zimefanikiwa.

Nchi jirani ya Kenya 2010, Sekta isiyo rasmi ilikusanya kwenye pato la Serikali trilioni 8 ambazo hapa miaka miwili iliyopita ndiyo ilikuwa ni pato ambalo *TRA* wanakusanya kwa mapato ya Serikali.

Wameweza kukusanya pesa hizi kwa sekta isiyo rasmi kwa hawa wamachinga, watu wa daladala, mamalishe, bodaboda kutokana na utaratibu mzuri waliouweka kuwapanga na kuwatambua pamoja na kuwaacha wafanye biashara zao ili waweze kuwatoza kodi.

Mheshimiwa Spika, nikizungumzia Mkoa wa Dar es salaam kuna Wamachinga na Wafanyabiashara Wadogo Wadogo zaidi ya milioni moja (1,000,000).

Hawa wakiwekwa na ambao tumeshawaweka katika utaratibu mzuri, tumekuja kuharibiwa hivi karibuni tu na Mkurugenzi mpya, sijui anatoka Mkoa gani, akahamishiwa Dar es salaam, kwa vile hajui na haelewi mazingira ya ki-Dar es salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wafanyabiashara wadogo wadogo milioni moja, wakilipa shilingi mia tatu kwa siku ni milioni mia tatu kwa siku. Kwa mwezi ni bilioni tisa (9,000,000,000/=). Kwa mwaka ni bilioni mia moja na nane (108,000,000,000/=). Hizi ni pesa ambazo zipo na zinaweza zikasaidia

Halmashauri zote nchini kwa utaratibu wa kuweza ku-*capture* na kutoza pesa hizi kwa kuwapa mazingira mazuri ya kufanya shughuli zao.

Lakini badala ya kuona hii ni sehemu ya kupata mapato, hawa sasa wanafukuzwa bila sababu yoyote. Hakuna mtu anayetaka uchafu katika maeneo yake na hawa wafanyabiashara wadogo wadogo wala siyo wachafu. Ni wafanyabiashara ambao wanafanya biashara wana mahitaji kama sisi ambao tunayo.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi naomba, Serikali ipo hapa na Mheshimiwa Lukuvi ameshawahi kuwa Mkuu wa Mkoa. Na alipokuwa alitoa ushirikiano mzuri sana kwa hawa wafanyabiashara wadogo wadogo na maeneo mengi sana yalikuwa salama. Huu ujambazi unaotokea Dar es salaam sasa hivi, unatokea sababu wafanyabiashara wadogo wadogo hawapo katika sehemu zao za biashara. Wakiwepo kwenye sehemu zao za biashara ujambazi na vibaka kunakuwa hakuna.

Mheshimiwa Spika, mataifa yote na najua Wakurugenzi wote wameshawahi kusafiri nje. Ni tamaduni za Miji yote duniani, usiku watu kula kwenye Mitaa. Hali kadhalika Mitaa ya Dar es salaam na Mitaa ya maeneo yote nchini mwetu. Ni utamaduni wa kawaida.

Lakini leo Dar es salaam, wapikaji, mamalishe na wapika *chips wote* wamepigwa marufuku kufanya biashara zao na hatujui ni kwa sababu gani. Hii inapunguza mapato ya Halmashauri ya Jiji ambayo wanataka sasa kukusanya ili waboreshe lile Jiji.

Mimi naomba na niposema Mwenyekiti na Mheshimiwa William Lukuvi, wote mko hapa. Jiji la Dar-es-salaam halina Mamlaka ya kuendesha *urban authorities* kwa mujibu wa *GN Number 77*.

Jiji la Dar es salaam limepewa kazi maalum ya sherehe kupokea wageni na bendera wakati wa sherehe za Kitaifa. Halina kazi hiyo! Nataka Mkuu wa Mkoa alisikie hili na elewe. Anamruhusu Mkuu wa Mkoa kufanya vitendo vya kuvunja Sheria kwenye Jiji la Dar es Salaam kwa kuchukua maeneo ya Halmashauri ya Temeke, Ilala na Kinondoni bila utaratibu wa Kisheria.

Tunataka Serikali itusikilize, ielewe makosa yanayofanywa na Mkurugenzi wa Jiji kwa kukamata maeneo yaliyoainishwa kisheria na Bunge hili. Tunataka majibu mtuambie! Mgongano huu unaofanywa sasa. Mapato Dar es Salaam hayapatikani kwa sababu hajui nani achukue mapato haya. Kwa hiyo, nilikuwa naomba hilo mlizingatie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakuja katika suala lingine la simu hizi za mkononono. Nimekwenda mimi Afrika Kusini, Namibia na nchi zingine. Ili kudhibiti mapato ya simu katika kodi za Serikali, unapoweka vocha yako kwenye simu, kwa mfano dola kumi, pale pale kwenye *screen* inaonyesha kwamba shilingi dola tatu au shilingi elfu tatu ni mali ya Serikali na shilingi elfu saba mtagawana na *operator* wa hiyo simu.

Naomba utaratibu huu sasa uchukuliwe Tanzania. Kwa kila anayetia *credit* kwenye simu yake, pato la Serikali lionekane pale pale kwenye *screen* ili *TRA* wasiwe na tabu ya kuweza kufuatilia mapato yao.

Mheshimiwa Spika, *importation* ya *airtime*. Hizi *vocha* zinazokuwa *imported* ambazo zingine huwa zinatengenezwa hapa na zingine zinakuwa *imported.* Zisiwe *cleared* Bandarini kama mzigo. Ziwe *cleared* kwa *value airtime imported in to Tanzania.*

Pale pale *TRA* unapoingia mzigo wajaribu kujua thamani ya *airtime* ambayo inakuwa *imported* na ma-*operator* ni shilingi ngapi, ili waweke rekodi waweze kuwadai 30% ya kodi ya Serikali wakati mzigo unaingia Bandarini.

Mheshimiwa Spika, nilikuomba unipe nafasi ya kuchangia kwa sababu nilikuwa na haya tu ya kuyasema ndiyo niliyoyaona ni muhimu kwa Kitaifa na hasa kwa Dar es Salaam. Nakumbusha tena Mheshimiwa *Attorney General (AG)* yuko hapa, nimeshawahi kuzungumza naye, yeye ndiye anayejua hizi Sheria. Tunataka Jiji la Dar es salaam liendeshwe Kisheria. Tunataka Mamlaka za Manispaa ya Ilala, Temeke na Kinondoni ziendeshwe Kisheria na Mkurugenzi wa Jiji aache kuingilia.

Nimeona anatumia magazeti sasa hivi kutuponda, kututukana sisi wala hatujali. Tunaendelea na kazi ya kutafuta haki za wananchi wetu wa Dar es Salaam na tutapambana kusaidia Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona Ng'ombe wakipata madhara ya ukame wanafidiwa, wakulima wa pamba wanafidiwa, stakabadhi ghalani wanafidiwa, korosho wote wanafidiwa.

Mheshimiwa Spika, kuna Wafanyabiashara Dar es Salaam wameunguliwa na soko lao la Machinga pale Karume. Tunaomba Serikali iwe na huruma, iwatizame na iwaruhusu hawa wajiendeleze.

Sasa hivi wanajaribu kuboresha eneo lao. Waache waboreshe na sisi tuwasaidie. Nasikia Mkurugenzi ametoa tanganzo wasiboreshe. Sidhani kama kuna mpango au kuna *project* ama Bajeti ya kujenga soko jipya la Machinga Karume, hakuna!

Kwa hiyo, kwa maana hiyo tumeshindwa kujenga Kisutu na Buguruni. Kwa hiyo, tusiwadanganye wananchi kama tutaboresha soko la Wamachinga pale Karume.

Mheshimiwa Spika, waachieni wajenge na kutafuta maisha yao. Hawa ni Watanzania na wana mahitaji kama binadamu wa kawaida. Wana mahitaji ya kuoa, wana mahitaji ya kusomesha, wana mahitaji ya kwenda Hospitali na wana mahitaji ya kula. Hii ni dhamana kubwa sana ya Serikali kwa hawa watu na Serikali haitaweza kupambana na watu wenye njaa.

Kwa hiyo, mimi naomba Serikali wote mpo hapa, muelewe kwa Dar es salaam kuna *crises* kubwa sana ya Kiutawala na *crises* hii inayofanywa sasa hivi, mapato hayakusanywi kwa sababu Jiji linataka kuteka maeneo ya Manispaa zetu bila utaratibu na mapato sasa wananchi hawajui nani wampe mapato haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno haya nakushukuru sana. Nampongeza tena Waziri na timu yake pamoja na *TRA*, naunga mkono kwa asilimia mia moja Bajeti hii. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Halima James Mdee, atafuatiwa na Mheshimiwa Said Zuberi.

**MHE. HALIMA JAMES MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti ninakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mdee, mbona mnaniita Mwenyekiti na mimi ni Spika? *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. HALIMA JAMES MDEE:** Mheshimiwa Spika, tunaambiwa hii ni Kamati ya Matumizi, kwa hiyo tunachanganya kidogo. Mimi niungane na Mheshimiwa Mussa Zungu Azzan, kwa yote anayozungumza ili kuepuka kuokoa muda kuhusiana na Mkoa wa Dar es Salaam na ni ukweli kabisa Serikali ni muhimu ikaelewa kwamba haitaweza kabisa kushindana na watu wenye njaa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kama mna nia dhabiti ya kuhakikisha kwamba tunakusanya mapato, tukiweka wafanyabiashara wetu katika mazingira mazuri, tukiwashirikisha wafanyabiashara wetu ndogo ndogo, mfano waendesha boda boda vya kutosha. Tutapata mapato ya kutosha na masuala ya kuomba omba yataisha. Ni muhimu muwe wasikiivu. Mwaka jana 2013 nilisema hapa kwamba taarifa ambayo imetolewa na *ESAP* inaonyesha kwamba ni watu, Makampuni, ama taasisi mia nne tu (400 tu), zinazo changia asilimia 80 ya makusanyo ya *TRA*.

Hii ni taarifa ambayo ilitiwa sahihi na aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha. Asilimia nyingine 20 ndiyo inachangiwa na watu wengine. Tunaambiwa Watanzania zaidi ya milioni 13 hawalipi kodi rasmi, tunalipa kodi zisizo rasmi. Kodi ambazo zinajaa kero, ambazo mnajikuta wafanyabiashara wadogo wadogo wanalipa kodi nyingi sana *unnecessarily.* Lakini tukitengeneza mfumo ulio rasmi, kodi zitakuwa rafiki kwa wananchi wote na wananchi watapenda kulipa kodi.

Kwa hiyo, mimi niwaombe! Mheshimiwa Lukuvi alikuja hapa akaniambia kitabu kipi? Nikampigia *picha (photo copy)*.

Sasa mimi nilitarajia kwamba mtaenda kusoma vitu vyote ambavyo vimeainishwa kule, ambavyo vina tija kwa Taifa hili. Hamjaenda kusoma! Leo mmekuja na *story* zile zile za miaka iliyopita.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa nashauri kwamba msome. Mmepata dhamana, umizeni vichwa, ili Taifa hili lisonge mbele. Siyo tukiwapa maoni mbadala, badala ya kuyafanyia kazi mnakuwa mna-*critisize.*

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti inafanya kazi nzuri. Lakini Kamati ya Bajeti na yenyewe iache kulalamika. Kwa sababu sote tunajua kwamba Kamati hii inafanya kazi kwa niaba ya Bunge zima. Inafanya kazi kwa niaba yetu! Sisi tunajua taratibu za Kikanuni kwamba kama Kamati ikiamua jambo lisifike Bungeni kwa sababu Serikali haisikii ama ina kiburi inaweza ikalimaliza huko huko mpaka Serikali i-*give in*.

Sasa Kamati ya Bajeti na yenyewe inakuja inatupa mbwembwe nyingi, lakini na wao wanaishia kulalamika. Sasa kama suala linakuja utekelezaji wa Sheria, nimemsikiliza kwa makini sana jana Mheshimiwa Hamad Rashid. Anasema kwamba Sheria ya *deep sea* iko wazi. Watu wakate leseni, wakimaliza kukata leseni wanatakiwa kila mwezi wanaripoti Bandarini. Wasiporipoti Bandarini wanatakiwa watozwe faini, dola milioni mia moja *(100,000,000 USD)*.

Sheria ipo haitekelezwi, Kamati inalalamika tokea mwaka jana, mwaka huu na Serikali inakosa mabilioni ya shilingi halafu tunakuja tunatoza kodi feki. Tunakuja tutoza kodi viroba, tunatoza kodi *lip stick* na wanja? Hivi hizi ni akili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Kamati yako imejaa watu ambao wamesheni, watu ambao wana vipaji lakini kutakuwa hakuna maana kwamba wakaa masaa ya ziada ni kweli, wanakaa mpaka saa nane usiku lakini kukaa kwao hakuna tija kama hawatalisaidia hili Bunge liweze kwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Spika! *Sorry* hii mizuka ikipanda mtanisamehe. Tumeambiwa Kamati ya Matumizi sasa muwe mnaweka vizuri. Mwenyekiti! Spika sorry! *(Kicheko)*

**SPIKA:** Endelea tu unaeleweka.

**MHE. HALIMA JAMES MDEE:** Mheshimiwa Spika, suala lingine, Waziri wakati anatoa hotuba yake, kajiondolea mamlaka ya kusamehe kodi. Mimi nikaona ni jambo la busara sana ya misamaha ya kodi kwenye mafuta na mambo mengine.

Alifanya hivyo kwa sababu ameona kwenye taarifa za *CAG* za miaka mitatu ama minne mfululizo, imetuonyesha kwamba katika mifumo iliyopo sasa ya kutoa misamaha ya kodi, kuna mianya mikubwa sana hali iliyopelekea kwamba tunatoa misamaha ya kodi mpaka asilimia 4.3 ya pato la taifa.

Kwa walioona kuna mianya cha kunisikitisha, Kamati inakuja jana inatuambia kwamba lile wazo lililotolewa na Waziri siyo sahihi na kwamba tumrudishie Waziri Mamlaka ya kusamehe ama kutoa misamaha ya kodi.

Mheshimiwa Spika, hii ni aibu, ni aibu kwa Kamati, ni aibu kwa Bunge hili Tukufu kama Serikali inakuja na *proposal* ya kujaribu kutafuta suluhu na sisi ndiyo tunajibana. Tunaleta Mabadiliko ya Sheria. Sheria ya *VAT*, Sheria ya Utawala wa Kodi. Hivi vitu ndivyo vitatuambia misamaha ya kodi inaendaje endaje, kwa utaratibu gani na kwa mipaka ipi.

Kwa hiyo, hoja ya Kamati ni kwamba eti Waziri tukimtolea mamlaka yanaweza yakaibuka masuala ya dharura haina mantiki. Tukija kutunga hizo Sheria na naamini itakuja Bunge lijalo, tutaweka mazingira ya dharura ambayo tutampa Mamlaka Waziri wa Fedha ya dharura na tutaainisha kwenye Sheria.

Tukiacha utararatibu uliopo sasa. Tukiamini kwamba *TRA* wana uaminifu Mtakatifu. Huo uaminifu wa michakato iliyopo ndiyo imelifikisha Taifa hapa. Kwa hiyo, mimi naliomba Bunge lako Tukufu, uamuzi ambao uliletwa na Serikali kama *proposal,* ambao Kamati yetu imeenda kule imeugeuza geuza, ibaki vilevile. Mamlaka ya Waziri yaishe, yabaki kwenye hii mikataba ambayo wataingia na Wawekezaji kama ambavyo ilibaki katika hatua ya mwanzo.

Mheshimiwa Spika, niliombe Bunge lako Tukufu, tulizungumza hapa tukasema ni aibu kwa Rais kutengewa shilingi bilioni 50 apande ndege kuzunguka huko duniani eti akisema anaenda kuanga washikaji kwa sababu muda wake wa Urais umeisha. Aongezewe kutoka bilioni 15 mpaka bilioni 50 wakati juzi Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika anasema wanahitaji bilioni 400 lakini wamepewa bilioni 42.

Mheshimiwa Spika, naliomba Bunge lako Tukufu, katika hatua hii ya kamati ihakikishe zile bilioni 50. Ninajua Mheshimiwa Waziri hataki kusikia Rais wake anapunguziwa mshiko. Lakini tunasema hivi kama mnaipenda nchi hii ni aibu, ni uchizi, ni wendawazimu, kumpa Rais bilioni 50 halafu kutoa kwa kilimo bilioni 42. *We are not serious, we are not focused*. *(Makofi)*

Benki ya Dunia inatuambia kwamba ikifika 2050 mahitaji ya chakula duniani yataongezeka kwa asilimia 70. Uchumi wa dunia sasa hivi ni kilimo. Hivi tunaangalia kesho? Kila siku nawaambia kama tuna *focus 50 years to come, 20 or 100 years to come* kwa Tanzania bora tutaangalia fursa za baadae ni zipi, tunawekeza. *By the time* fursa zinajiachia tunakuwa tupo tayari, siyo sasa hivi sisi ni wakukimbiza kimbiza tu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Kengele ya pili. Mheshimiwa Said Zuberi, atafuatiwa na Mheshimiwa James Mbatia.

**MHE. SAID MUSSA ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nami kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kunipa afya njema.

Lingine ni kuunga mkono kwanza kwa asilimia mia moja Muswada huu. Vile vile naipongeza timu kuanzia Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake wawili pamoja na Kamati ya Mheshimiwa Chenge kwa kazi pevu na nzito waliyoifanya na leo kutuletea mambo ambayo kidogo yanaonekana kwamba yanaweza yakalisaidia Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nianze moja kwa moja kwenye masuala yanayohusiana na magari ambayo tayari yana umri wa miaka kumi na kuendelea kama alivyotueleza Mheshimiwa Waziri kwamba wamepunguza, badala ya miaka kumi sasa wametuwekea miaka nane; na magari ya miaka kumi na kwenda mbele wameongeza malipo.

Mheshimiwa Spika, nataka niwafahamishe tu kwamba mbinu nzuri ilikuwa ni kuondoa kabisa, yaani kupunguza kwa asilimia kubwa ushuru wa magari mapya, kwa sababu sidhani kama kuna mtu yeyote ambaye anahitaji kununua mitumba, lakini kufuatana na hali za wananchi wetu inawabidi wafanye hivyo.

Mheshimiwa Spika, lingine nizungumzie kuhusu uchakavu na uharibifu wa mazingira. Naomba niulize hii *vehicle inspection* inafanya kazi gani? Kwa sababu kuna magari yana zaidi ya miaka 12, lakini ukiliangalia kwenye *mileage* pengine labda ndiyo kwanza lina kilomita 90,000 au laki moja. Pia kuna magari ambayo yana miaka mitatu au minne tu tangu kutengenezwa, lakini ukiangalia lilivyochakaa hata kwa macho, basi huwezi kwenda kulinunua.

Sasa wanapozungumzia suala la ku-*reduce* kutoka miaka kumi mpaka minane, kwa mategemeo ya kwamba wanahisi ndiyo tutapata gari nzuri, kuna magari yanakuwa yanachafuka sana kufuatana na kazi zinazofanya zile gari ama na mtumiaji mwenyewe wa ile gari. Hili nahisi kama hawakulizingatia. Kwa hiyo, sidhani kama hii hoja bado ina mashiko. Mimi nilikuwa naona cha msingi hapa cha kufanya ni kushupalia *vehicle inspector* wafanye kazi yao kwa uadilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiki ndiyo kitu ambacho kingeweza kutusaidia, kwa sababu kuna magari yanakuja, kama nilivyozungumza, yanakuwa ni mazuri, na bado yana hali nzuri na hayaweki *pollution*, wala hayafanyi chochote na wala hayaharibu mazingira kufuatana na utumiaji wake.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo linaweza likatusaidia nahisi nalo wamelisahau au vipi, katika kuanzisha hivi vyanzo vipya ili tuweze kupata mapato mengine mapya kuongeza kwenye kodi, suala la vitambulisho *NIDA;* Serikali ingekamilisha mapema suala hili kwa Watanzania wote, basi tungeweza kuwapata watu ambao wanastahiki kulipa kodi na hawalipi. Hapa tungepata chanzo kingine cha mapato ambayo yangetusaidia katika kuondokana na matatizo haya tuliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukiendelea ku-*delay* na suala hili la vitambulisho, bado tunaendelea kubaki kule kule tulikotoka, tutaendelea kupandisha bei kwenye vinywaji na vitu vingine. Mimi ningeshauri Serikali tujitahidi iongeze *speed* katika suala hili kuhakikisha kwamba kila Mtanzania anapata hii *ID* ili aweze kutambulika kwamba huyu tayari ameshafikia kulipia kodi na ana haki ya kulipa au hakuna. Nafikiri hapo *gap* inaweza ikapanda kutoka hapa tulipo na tukaongeza watu ambao wataweza kulipia kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tusidharau hizi kodi ndogo ndogo, ndizo zinazochangia mapato makubwa kuliko zile kodi kubwa ambazo ni wachache wanaoweza wakalipa. Tulio wengi mapato yetu ni madogo, lakini tuna uwezo kufuatana na huo udogo wa mapato yetu, tutaweza kulipia kodi na ikaisaidia Serikali hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Bahari Kuu; kama alivyozungumza jana Mheshimiwa Hamad Rashid, hili eneo haidhuru Mheshimiwa Waziri umetuambia hapa kwamba mko kwenye kufanya uchambuzi wa kina, lakini huku tunafanya uchambuzi wa kina ili tuje na kitu kizuri, tuziangalieni basi hizi sheria zetu ambazo tunazo kwa sasa hivi. Hivi ndiyo imetosha kwamba mtu ameshakata *license,* basi anajifanyia tu anavyotaka huko? Iweje Mtanzania aliyepo humu ndani anakata *license* kila mwaka na bado kodi anaendelea kulipa? Lakini mtu mwingine aje kwa kuwa ameshakata *license,* basi ndiyo afaidi afanye anavyotaka huko, kuwe hakuna chochote ambacho anaweza kulipia ama sisi tukamwangalia nini anafanya na tukajua nini sisi kama Taifa tunapata?

Mimi naona bado tuendelee kufanya hizo tunazoziita ni michakato lakini bado kabisa tunahitajika kuanza na hizi sheria tulizokuwa nazo.

Tukianza nazo hizi tulizonazo, tutajua upungufu uko wapi na wapi tunahitajika turekebishe huku tukiendelea kufanya na hiyo michakato mingine. Lakini tusiwaachie tu kwamba wao wakishalipa hizo *license* tena ndiyo iwe imekwisha, wanajifanyia wanavyotaka; hii haiwezi ikatusaidia. Mimi naona tungeanzia hapa halafu tukasonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, naipongeza Kamati kwa kuliona suala hili la masuala haya ya *computer* na hizi *monitor* pamoja na baiskeli kuondoa kwenye malipo yale ya asilimia 25 ya vitu chakavu ambavyo vinaingizwa kwa ajili ya matumizi ya nyumbani.

Mheshimiwa Spika, hili jambo kwa Watanzania walio wengi na kama tunataka tupige hatua, basi hapa tumefanikiwa. Tungeviingiza na vitu hivi vidogo ambavyo ndiyo vitu vinavyosaidia sasa hivi watu kuweza kuelimika kwa haraka, ukweli tungekuwa tumerudi nyuma hapa.

Mheshimiwa Spika, hii kodi isingetusaidia na wananchi bado wangeendelea kuwa ni watu wa mwisho au wa mkiani. Lakini wameliona jambo hili, nawashukuru sana na nawapongeza kwa kuweza kuondoa kodi hizi kwenye vitu hivi ambavyo tunaviita *used, monitor* pamoja *computer* na baiskeli kwa sababu kwanza Watanzania walio wengi kipato chao ni cha chini.

Mheshimiwa Spika, tunategemea huko mashambani na vijijini watu kutumia sana baiskeli; na huu ulimwengu wa teknolojia unaokuja tusipokaza buti na sisi tukataka kuelekea na wenzetu tutashindwa. Kukaza buti ni kwamba tumeliona hili na tumejua kwamba hizi *computer* sijui mpakato na hizo nyingine zote tunziondoa kwenye *group* hili. Hapa nawapongeza sana kwa kuligundua hili tatizo.

Mheshimiwa Spika, nziungumzie kuhusu *money transfer*. Hili nalo vilevile nampongeze Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kuliona. Ukweli, tulikuwa tunaumia sana na wazee wetu tunawatumia fedha kule vijijini wanakuwa wanaumia mpaka mtu sasa anaanza kufikiri kwamba hii sasa inasaidia au haisaidii?

Kulikuwa kuna watu wa kati wana-*enjoy* ambao wao ndiyo kazi yao pamoja na mabenki kuweza kufanya *transfer* ya zile fedha. Hili nashukuru kwamba mmeliona na mmekusudia kwa dhati kuondoa mzigo kwa wananchi, ndiyo maana nikasema niwapongeze. Hawa waliokuwa wana-*enjoy* hii fedha ambayo sisi tunalipa ada, sasa ninyi mmegundua kwamba sasa itabidi mabenki pamoja na wanaofanya mambo haya ya mitandao, ndio … *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante. Muda wako umekwisha. Sasa namwita Mheshimiwa Mbatia, atafuatiwa na Mheshimiwa Selasini.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia Muswada huu wa Fedha wa mwaka 2014.

Mheshimiwa Spika, dhana ya matumizi ya Serikali na mapato ya Serikali; kwenye mapato tunapata wakati mgumu sana kuishauri Serikali kwa sababu Serikali inafanya ni siri mapato yake mpaka siku ya bajeti hapa Bungeni ndiyo bajeti Kuu ndiyo inatoa uwazi wa mapato yapatikane vipi.

Kwa hiyo, unakuta tunatumia muda mrefu sana kwenye matumizi ambapo hatutumii muda na tukakubaliana vyanzo vya mapato viwe namna gani. Ndiyo maana inakuwa ni siri, inakuja na *measures* za mapato, unakuta Serikali hiyo hiyo inaumizana kwenye sekta nyingine. Unakuta Waziri mmoja kwenye Sekta labda ya Utalii au mwingine kwenye Sekta ya Miundombinu au ni Uchukuzi, hawashirikishani hata wao wenyewe ili kuona kwamba: Je, nikichukua mapato kwenye Sekta yako, Sera za Uwekezaji inakuwaje? Ndiyo maana kunakuwa na msuguano wa vuta nikivute.

Mheshimiwa Spika, bajeti, hasa mapato katika dunia ya leo ni shirikishi. Ndiyo maana unakuta mambo ya uvuvi hata ripoti ya Kamati ya Spika yamezungumzwa; sheria zipo, miaka nenda rudi hawachukui yale mawazo, dakika ya mwisho wanasema bado tunaendelea na mchakato, bado tunaendelea kutafuta watalaam.

Mheshimiwa Waziri, kuna mambo mengine, sawa; Watendaji wanaweza wakashauri, lakini kukiwa na muda wa kutosha wa kuanza kazi hii, makubaliano yatakuwepo na hakutakuwa na misuguano mikubwa ya namna hii ya kufikiria vyanzo vilevile tu vya mapato.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, *PAYE* kwa wafanyakazi wetu hawa, punguzo la kutoka asilimia 13 kwenda kwenye asilimia 12 mwaka huu, yaani unamwongezea huyu mfanyakazi Sh. 1,900/= tu. Mheshimiwa Waziri Sh. 1,900/= inakutosha kununua mkate? Yaani ndiyo kitu tulichomwambia mfanyakazi Serikali inatamba kwamba tumepunguza kwa asilimia moja Sh.1,900/= kwa mwezi. Jamani, jamani, *you cannot imagine*! Wakati unawaambia *source* ya mapato iko pale, tunaenda huku, angalia ile tofauti iliyopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia takwimu, tulipotoka kwenye tarakimu 14 kwenda 13, yaani mwaka 2012/2013, mapato ya Serikali yalikuwa Shilingi bilioni 425.96, mwaka huu tunaomaliza sasa, walipokuja asilimia 13, mapato yakaongezeka yakawa Shilingi bilioni 509.997 na mwaka ujao tunategemea kupata mapato ya Shilingi bilioni 568, yanaongezeka. Kwanini yanaongezeka? Utaona kwamba ukiamua kushusha zaidi ule mzigo wa waajiri, ikienda kwenye tarakimu moja, wanaweza zaidi na wana-*formalize* badala ya wafanyakazi wao kuwa vibarua, wanakuwa ni waajiriwa rasmi, wanakuwa ni watumishi na wanalipa hizi *Pay As You Earn* lakini

wakiona kuna mzigo mkubwa, watakuwa wanakwepa, kwasababu hakuna mtu anayependa kulipa kodi.

Ndiyo maana tunaposema, badala ya kuangalia kumgandamiza huyu mfanyakazi, tuangalie sehemu nyingine ili tuhakikishe kwamba wafanyakazi na hasa wale wa kipato cha chini maisha yao yanaboreka wakati vyanzo vingine mbadala vya mapato vipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda niseme sehemu nyingine, nitoe mfano wa Sekta ya Utalii. Ukubwa wa Tanzania ni kilomita za mraba 945,203, Kenya 541,309, Uganda 236,040, Burundi 27,834, Rwanda 26,338. Ni kwamba katika Afrika Mashariki yote, Tanzania tumezidi wenzetu na kilomita za mraba 73,682, yaani sisi tunachukua asilimia 52 ya eneo lote la Afrika Mashariki. Je, soko hili kubwa, ukubwa wa nchi yetu, wakati takwimu zinatuonyesha kati ya utafiti uliofanyika kwenye nchi 133 duniani, kwenye vivutio vya utalii Tanzania ni ya pili duniani, lakini kwenye mapato katika sekta hii tumeshika nafasi ya 110 kati ya nchi 133. Kenya ni wa 28 kwa vivutio vya utalii, wanashika nafasi ya 103; Mauritius kwenye vivutio vya utalii ni ya 131 yaani tofauti ya nchi mbili, inashika mkia, lakini kwa mapato kutokana na Sekta ya Utalii ni ya 53. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa yapo wapi mazingira ya utalii wakati sisi ni wa pili kwa vivutio vya utalii duniani? Wa kwanza ni Brazil. Tunaunganishaje rasilimali hii aliyotujalia Mwenyezi Mungu ukaiunganisha na Sekta ya Anga kwa sababu leo hii Mheshimiwa Waziri unatoka Zanzibar, unajua *Italian Airline* inakuja Zanzibar mara tatu kwa wiki, na ikifika pale, watalii wakishafika pale ni lazima wawe na *connection* ya *domestic airline* ambayo itawatoa watalii hao iwapeleke *selous*, iwatoe iwapeleke Serengeti. Sisi Mwenyezi Mungu ametujalia Serengeti tuna kilomita za mraba zaidi 14,000, wenzetu Kenya Maasai Mara wana kilomita 1,500. Wataendaje na ndege? Sekta hii imeandaliwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tusipoliangalia hili kwa mapana yake, ukaangalia tu mapato, yaani unaangalia chakula cha kula leo jioni, huangalii chakula mwaka ujao, miaka kumi ijayo, ndiyo tatizo. Ndiyo maana tunakuja na kodi ya mwaka huu mmoja tu. Tunaangalia *measures* fupi hapa!

Mheshimiwa Spika, anga letu sasa hivi limeanza kuchanganya kwa kiasi, mmesharudi tena kukamua pale pale, wakati mnaacha Sekta nyingine kubwa ambazo tungepata mapato na ndiyo maana tunabaki hapa, sasa tunalalamika badala ya kufanya maamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni dhamira au ni nia ya Bunge lako Tukufu na nikupongeze kwa kuanzisha mfumo huu wa bajeti shirikishi, lakini kwenye mapato bado kabisa! Vyanzo vipo wazi. Ili tuondokane na h ii tabia tu ya kuja kufikiria soda, juisi, sigara; yaani Bajeti ya Amiri Jamali ya mwaka 1963 ya Tanganyika Huru, ndiyo mnayoileta mpaka leo hii. Mnafikiriaje jamani? *Can't we be serious*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mwenyezi Mungu ametujalia kilomita za mraba kwenye *deep sea fish* 230,000 halafu leo hii tunawezaje tukalalamika? Yaani *you cannot imagine* kwamba tuna kilomita za mraba 230,000, hakuna chochote tunachopata, tunaenda kwenye *Pay As You Earn. How*! Halafu tupo washindani hapa!

Mheshimiwa Waziri, umezungumzia kuhusu nondo. Tunazo nondo za kutosha humu ndani, viwanda vyetu vinatosheleza; mmeenda *East Africa* mmekubaliana asilimia kumi kama zinaingia kwenye nchi yako. Wenzetu wa Kenya, niwe wazi, wamekwenda asilimia 25. Wamevunja! Sisi tunapata kigugumizi gani? Kabla huja-*wind up,* useme asilimia 25 Tanzania na sisi tunaenda kama wenzetu wa Kenya tulinde soko la ndani. Ni lazima tulinde soko la ndani! hatuwezi tukaogopa! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, angalia Uganda wamefanya vipi? Sasa sisi hatuwezi tu tukawa kana kwamba basi ni hewala, hewala! Uswahili kwenye mambo hayo, hapana! Tunapambana kwa ajili ya uchumi. Na kodi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa. Sasa namwita msemaji wetu wa mwisho, Mheshimiwa Selasini.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru sana kwa kunipa nafasi kuchangia kwenye hoja hii. Kabla sijachangia, niseme tu kwamba naunga mkono kwa dhati maoni ya Kamati yetu ya Bajeti na kumpongeza Mwenyekiti wetu kwa namna anavyotuongoza kwenye Kamati yetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia suala la *PPP*. Hatutaweza kuendelea na hatutaweza kupanua wigo wa kodi kama Serikali itaendelea kushikilia, kufanya mambo yenyewe. Naishauri Serikali ianze sasa kuhakikisha kwamba inashirikiana na baadhi ya watu wenye fedha zao na wenye ujuzi katika kuendesha kwa pamoja baadhi ya miradi ili kuweza kuipunguzia Serikali mzigo wa matumizi ili fedha za Serikali ziweze kufanya kazi muhimu ya Serikali ambayo ni kuangalia uendeshaji wa nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, miradi kama ya reli na barabara ni miradi ambayo kama Serikali itaamua, inaweza ikaifanya kwa ushirikiano na wafanyabiashara, watu wenye pesa na matokeo yake, mzigo huu tunaoupata kwa kujenga barabara zetu au aibu hii tunayoipata ya hii reli yetu ikamalizika.

Mheshimiwa Spika, hili ni jambo ambalo limezungumzwa muda mrefu na ni jambo ambalo linaweza likachukuliwa hatua, lakini nadhani bado uamuzi haujafanyika. Nami naishauri na kuisisitiza Serikali, kama kweli tunataka kuondoka katika kilio cha kila mwaka cha sungura mdogo, tuangalie namna ambavyo Serikali itashirikisha *private sector* katika baadhi ya miradi mikubwa ili Serikali ijikite katika kuhudumia wananchi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kuzungumza ni wizi wa fedha za Umma ambao bado unaendelea.

Mheshimiwa Spika, kupanga ni jambo mojawapo, lakini vile vile kusimamia matumizi ya Serikali yaende sawa sawa, nalo ni tatizo lingine. Bado kuna wizi mkubwa sana unaendelea katika Wizara zetu na katika Taasisi za Serikali. Wakati tulipokuwa tunafanya kazi katika Kamati yetu, tulipata taarifa kwamba pamoja na kwamba tulianzisha Kitengo kile cha *Internal Audit* ambacho tulitegemea kwamba kitafanya kazi ya kukagua Hesabu za Wizara vizuri, bado Maafisa Masuuli wanapopeleka maombi ya fedha Hazina, Hazina inapokagua yale maombi ambayo yametoka Wizarani ambako kuna ma-*Auditor* wa Ndani kule kule Wizarani, Hazina inaenda kugundua kwamba karibu robo tatu ya maombi yaliyotoka kwenye hizi Wizara ni maombi hewa. Hii ina maana kwamba bado fedha za Serikali zinaibiwa na Serikali haichukui hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninachofikiria, kwa hali tunayoiona, bado Serikali haijaamua. Nami niseme eneo moja tu ambalo lilielezwa kwa wazi kabisa. Wizara ya Ujenzi inadaiwa takribani

Shilingi bilioni 800 mpaka sasa hivi. Lakini hii ni Wizara mojawapo kati ya Wizara ambazo maombi yaliyotoka Wizarani…

**SPIKA:** Mheshimiwa Machali nakushauri ungemwacha huyo asikilize kusudi atujibu sisi wote. Usi-*consult* na mtu mwenye hoja yake.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, maombi yaliyotoka Wizarani yalipofika Hazina, karibu robo tatu ya yale maombi yalikuwa feki, na bado Hazina walipoamua kulipa yale machache ambayo waliona kwamba yanastahili, Wizara inalalamikia Hazina kwamba kwa nini mmelipa, kwa sababu hao mliowalipa ni feki. Sasa inaonekana kabisa kwamba miradi ya Serikali inaibiwa, kuna miradi hewa, wizi bado ni mkubwa, lakini Serikali bado inalia, haichukui hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama Serikali haitamua kupambana na wizi ndani ya Wizara zake, ndani ya Taasisi zake, Waheshimiwa Wabunge tutapiga kelele ya kutosha lakini hakuna kitakachofanyika.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumza ni kuhusu kupotea kwa mapato ya Serikali ambapo kunaandamana pia na wizi. Tumeelezwa kwamba kama Bandari ya Dar es Salaam ingesimamiwa vizuri, mapato yanayotokana na ile bandari yangeweza kulisaidia Taifa hili kwa kiasi kikubwa sana. Lakini bado bandarini pale kuna udanganyifu, wizi, kanga zinakuja watu wana-*declare* kwamba ni neti za mbu, na bado hali hii inaendelea.

Mheshimiwa Spika, lazima tuamue. Kweli wizi ni mkubwa, kweli uvujaji wa mapato ni mkubwa na lazima Maofisa waliopewa dhamana washughuliwe.

Mheshimiwa Spika, tunaelezwa pia kwamba mpaka wetu na nchi za jirani uko wazi kiasi kwamba mizigo mingine inapita mpakani bila kulipiwa ushuru. Nami najiuliza, kama watu wadogo wadogo wanapitisha bidhaa kwenye mipaka yetu na Serikali inalalamika; hivi jamani tuko salama? Kama mtu anapitisha mizigo mpakani, inapita, itashindwa kupitisha bomu? Mimi ninachofikiria ni kwamba hatujaamua.

Mheshimiwa Spika, mizigo inatoka kwenye nchi za wenzetu, inapita mipakani, inaingia, haitozwi kodi, hakuna chochote! Mizigo, *transit goods* ambazo zinatoka bandarini kwenda nchi za wenzetu, sukari, unga wa ngano, hata mafuta haya kama dizeli na petrol yanashuka tu hapa hapa nchini yanaingia kwenye magodauni yetu, hakuna ushuru, hakuna chochote!

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali iwe makini, ichukue hatua kama walivyosema wenzangu badala ya kulialia. Ichukue hatua ya kuhakikisha kwamba fedha zake zinakusanywa na zinalindwa vizuri. Zile ambazo Waheshimiwa Wabunge tumepitisha ziende zikafanye kazi, tuhakikishe kwamba zinafanya kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ni lile ambalo Mheshimiwa Halima alilizungumza kuhusu wafanyabiashara wadogo wadogo na Mheshimiwa Zungu naye alilizungumza.

Mheshimiwa Spika, tunazungumza kila mara habari ya Sekta isiyo rasmi kwamba irasimishwe; mpaka lini? Huwa tunasema kwamba Sekta isiyo rasmi itatambulika vitambulisho vya Taifa vitakapokamilika. Lakini hata hivyo, wafanya biashara ndogo ndogo wanalipa pesa nyingi sana kila siku kwenye Mifuko ya Mgambo wa Majiji na Halmashauri, kwenye mifuko ya Polisi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, utaratibu ukifanyika, kabla hata vitambulisho havijapatikana, bado hawa wafanyabiashara ndogo ndogo wanaweza wakatengenezewa utaratibu wakachangia kwa hiari na kwa njia ya kirafiki kabisa katika Mfuko wa Serikali na Serikali ikapata pesa. Tofauti na sasa hivi ambapo wanafukuzwa tu; anaamka Mkuu wa Mkoa fulani au anamka Mkurugenzi fulani, anaenda anavuruga utaratibu wa wale vijana; wanapigwa, wananyang'anywa bidhaa zao na kadhalika, na matokeo yake wanajenga chuki kwa Serikali na matokeo yake fedha ambazo zingepatikana kwa ajili ya matumizi ya Serikali, zinaingia kwenye mifuko ya Migambo wa Jiji pamoja Polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba utaratibu ufanyike ili isionekane kwamba hawa vijana wetu wanaishi kijanjajanja. Hawa ni vijana ambao wameamua kujiajiri na hii ni kauli ya Serikali, Wabunge tunahimiza vijana wajiajiri; hakuna ajira zilizo rasmi, lakini hizi ambazo siyo rasmi, bado vijana wanakwenda kutafuta mikopo, wanafanya kazi zao na wanaendelea kubughudhiwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, naomba, kama mwarobaini ni vitambulisho vya Taifa, basi hivyo vitambulisho vya Taifa vishughulikiwe vipatikane.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tunaenda kwa mujibu wa muda na walioomba kwa mujibu wa utaratibu. Kwa hiyo, wengine hawakuomba na pia leo inatakiwa tumalize saa 7.00.

Kwanza nitambue wageni waliopo humu ndani. Kuna wageni 97 wa Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu, ambao ni wanafunzi wa Chuo cha Uuguzi cha Kinga, *Mkinga Institute of Health Sciences* Wilayani Igunga. Naomba hawa Wataalam wasimame. Asante sana. Tunawatakia masomo mema na wema kwa wagonjwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

Tuna wageni wengine wa Mheshimiwa Ismail Rage wa Tabora Mjini, kutoka Kata ya Chemchemi Tabora ambao ni Ndugu Chiku Maulidi na ndugu Anna Chiyengo. Naomba hao wasimame. Ahsante sana. *(Makofi)*

Tuna wageni wa Mheshimiwa Khalfan Hilaly Aeshi, ni Mjumbe wa Baraza la UVCCM ambao ni Ndugu Hussein Mtoro, halafu yuko Ndugu Nicodemus Tambo, Katibu wa Vijana Mkoa wa Morogoro. Naomba wasimame pale walipo! Ahsante, wako huku. Karibuni sana! *(Makofi)*

Tuna wageni wa Mheshimiwa Magdalena Sakaya, ambao ni watoto wake. Naomba hawa wasimame walipo! Aah, kweli! Ukiangalia umri wao, kweli ni watoto wake. Ahsante sana.

Halafu tuna wageni watano wa Mheshimiwa Dkt. Fenella Mukangara, ambao ni Viongozi Muungano wa Machinga kutoka Mwanza ukiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Denis Lekela Nyamlekela na Ndugu Mwege, Fyeka, Mshauri wa Machinga Mkoa wa Mwanza. Wapo Dodoma kushuhulikia Mfuko wa Vijana. Naomba hawa waliotoka Mwanza wasimame. Ahsanteni sana. Wanawateteeni sana katika mfuko huu Waheshimiwa Wabunge hawa. *(Makofi)*

Tuna wageni waliokuja kwa ajili ya mafunzo, ambao ni wageni 36 kutoka *Nuru Lutheran Church Mbalizi,* wakiongozwa na Askofu Dkt. Erick Mwambigija. Nafikiri hata juzi walikuwepo. Wasimame walipo! Ahaa, ahsante sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wanafunzi wawili wa Kidato cha Sita, kutoka Shule ya Sekondari ya Ashira iliyopo Marangu, Moshi na wengine wanne kutoka Shule ya Sekondari Ruvu iliyopo Kibaha ambao pamoja na mafunzo, wanafanya *project* zao za kumaliza Sekondari kuhusu kazi za Bunge. Hawa watu wa *project* wapo wapi? Nadhani wako sita, wasimame kwa pamoja. Wako sehemu ile pale! Ahsante, na karibuni. Tunawatakia heri kwenye *project* hiyo. *(Makofi)*

Tuna Viongozi 91 wa SHIMIWI Taifa; Wenyeviti na Makatibu wa Vilabu vinavyoshiriki michezo ya SHIMIWI. Naomba na wanamichezo hawa wasimame kama wapo. Watakuwa wamekosa nafasi, basi tunawakaribisha.

Tuna matangazo ya kazi. Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Gosbert Blandes anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kuwa leo tarehe 28 saa 7.00 mchana kutakuwa na kikao cha Kamati. Kikao kitafanyika katika Ukumbi Na. 229 ghorofa ya Utawala. Tunaendelea. Mheshimiwa Mwigulu Mchemba!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. MCHEMBA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba nitumie dakika kadhaa kuchangia na kufafanua baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge. Nianze tu kwa kusema kwamba baadhi ya hoja nyingine tutazichukua kwa ajili ya kwenda kuzifanyia kazi kiofisi na nyingine tutatolea ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, kwanza niwapongeze Wabunge wote pamoja na Kamati kwa hoja ambazo wametupatia na kwa ushirikiano ambao wametupatia. Jambo la kwanza ambalo ningependa kuanzia kulitolea ufafanuzi kwenye hatua tuliyochukua, ningeanza na lile la ushuru wa kwenye ngozi. Alilisemea Mheshimiwa Mnyika hili.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba, alichokuwa anakielezea ni kile kinachoendana na utaratibu kama mambo yote yangekuwa yanaenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, tukiangalia mazingira ya nchini kwetu hapa, ukifuatilia utaratibu wa jinsi ngozi ambavyo imekuwa ikitolewa nje, takwimu zinaonyesha kwamba Tanzania hatuuzi ngozi nje. Ukifuatilia, utakuta ngozi zote zinaonekana zinauzwa kutoka Rwanda na hiyo inatokana na kwamba Rwanda wao hawajaweka kodi kwenye kuuza ngozi nje.

Mheshimiwa Spika, niseme tu jambo hili kwamba ni kweli tunahitaji kulinda viwanda, lakini kwa wakati ule ule tunatakiwa tuzingatie kwamba ngozi ni zao linalotokana na mifugo na wafugaji wanahitaji maisha mazuri.

Mheshimiwa Spika, naomba niweke wazi kwamba mimi ni mtoto wa mfugaji, niliyekulia Ronjo kule makambini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inapotokea ngozi yote Tanzania inauzwa kwa magendo, wafugaji hawapati faida kwa sababu wanauza kwa magendo. Kwa hiyo, tumeona, pamoja na kuvilinda viwanda vyetu, lakini ni vyema sana vikawapatia wafugaji bei inayoendana na soko ili waweze kuwauzia wafugaji badala ya kupitisha ngozi zile kwa magendo. Lakini tumechukua hatua hii tunaangalia uwezekano wa kuwa na kodi ya aina moja kwa nchi zote za Afrika Mashariki ili kuondoa huu utaratibu wa ngozi kwenda kwa magendo na hatimaye kuwanyima soko ama kuwanyima faida wafugaji wetu.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba, tunatakiwa kama Wabunge na Wataalam, tuwe makini sana na hatua tunazochukua hasa zinazohusu mazao ya wakulima pamoja na wafugaji.

Kuna wakati tuliwahi kuchukua hatua kwa nia njema kwamba tuzuie mahindi yasiuzwe nchi za jirani ili kuweza kuepusha upungufu wa chakula ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, nikwambie, jambo hilo liliwatia umaskini mkubwa sana wakulima pamoja na kwamba waliloa jasho sana wakati wa kulima mazao hayo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ni vyema tunapoangalia Sera kwa ujumla wake tuwaangalie pia na wahusika ambao wameloa jasho kwa ajili ya jambo hilo. Ndiyo maana tumesema, sasa mkulima akipata soko la bidhaa zake ni vyema tusimwekee vikwazo, auze ili na yeye apate faida, kwa sababu maisha yake yako kwenye eneo hilo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hivyo hivyo na kwenye ngozi hivyo hivyo na kwenye maeneo mengine ambayo yanamgusa mkulima au mfugaji moja kwa moja, tunatakiwa tusiwawekee kikwazo tukawafaidisha walioko kwenye biashara ama walioko mjini ilhali wao wakaendelea kuwa masikini kwa namna ile ile ya miaka na miaka. Kwa hiyo, tunaangalia namna ya ku-*balance*. Tulinde viwanda lakini na viwanda na wenyewe wajue wana wajibu wa kuhakikisha kwamba wakulima na wafugaji wanapata tija halisi ya kile kitu ambacho wanakizalisha. Kwa sababu tukienda kwenye Sheria kusema kwa nini tusizuie mia kwa mia kutoa ngozi nje? Wafanyabiashara wasio waaminifu, wataenda kuchukua ngozi zile bure na mfugaji ataendelea kuwa masikini milele na milele. Kwa hiyo, tunatengeneza *balance* ili na wafugaji waweze kupata faida iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo liliongelewa na Waheshimiwa Wabunge tangu jana, ni kuhusu misamaha ya kodi. Jambo hili amelisemea Mzee Ntukamazina, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Esther, Mheshimiwa Mwijage, Mheshimiwa Aeshi na Mheshimiwa Rage, hasa hatua hii ya kijasiri ambayo Waziri wangu, Mheshimiwa Saada amelichukua la kuonyesha mfano kwanza yeye mwenyewe kujiondolea mamlaka ya kusamehe, kutoa misamaha kwenye mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo hili ni vema sana Wabunge tukalielewa na Watanzania wote tukalielewa. Tukiwa na uelewa wa pamoja, tutaenda vizuri. Tulichokuwa tunasema, Watanzania wote, hata wa kawaida, wanalia sana kuhusu unyonyaji ama matumizi mabaya ya misamaha yanayotokea kwenye bidhaa hii ya mafuta. Kila mmoja analia kwenye migodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilipata bahati siku moja nikaongea na tajiri mmoja wa kwenye migodi ambaye alikuwa anafuatilia zaidi ya bilioni 100 *refund* ya kwenye mafuta. Nikamwuliza; hivi nyie ni matajiri sana, watu hatuna maji, hatuna fedha kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu, hatuna madawa mahospitalini, mnafuatilia hii hela na mnapata faida; *(Makofi)*

Hivi ni kweli kabisa, kabisa! Ni nchi gani mnafanya hivi? Akasema nchi nyingine hatufanyi hivi, lakini hapa tunafuatilia kwa sababu nyinyi wenyewe mmeweka kwenye Sheria kwamba tunastahili tupate hivi. Wanapata kwa sababu tumeweka sisi wenyewe kwenye Sheria. Sasa wapo wengine wanaweza wakawa sio waaminifu, atapata msamaha wa kodi kwenye mafuta, halafu kwenye faida ataandika hakupata faida, ata-*post* hasara, kwa hiyo, atapata msamaha na kodi anayotakiwa alipe kwenye faida, hatapata. Kwa hiyo, anachua hizi ulizompa kwenye msamaha kama ruzuku, halafu anakwepa huku kwa kusema hajapata faida. Kwa hiyo, sisi tukaona kwa kweli ni muda muafaka sasa kuanzia muda huu, sekta yoyote ambayo itaingia mkataba, hili la mafuta liwe limeshaondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi nilisema kwamba hatufukui makaburi. Wengine wanaweza kusema sasa si watu walishaingia mikataba! Sisi hatufukui makaburi, lakini tunasema kuanzia

sasa tuwe na ukurasa mpya ambao utaondoa hili ambalo limekuwa kilio cha muda mrefu kwa Watanzania na kwa Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mlikuwa mnaongelea mazingira ya dharura, ama mazingira ya miradi mikubwa. Mimi niwaambie, ni vyema tukaangalia utaratibu mwingine. Tusing'ang'anie utaratibu ambao tumeshaona kabisa unalipatia Taifa hasara. Tuangalie utaratibu mwingine na huu siyo lazima urejeshwe kwa Waziri tena. Tunaweza tukaangalia; kwa mfano, watu walikuwa wanatolea mfano wa dharura, vita na vitu vya hatari.

Mheshimiwa Spika, nasema, kikitokea kitu cha hatari cha aina hiyo, Bunge lazima litafanyia uamuzi, kwa hiyo, kwenye uamzi huo linaweza likasema na Majeshi yapewe mafuta. Hilo linaeleweka! Lakini tusimpe mfanyabiashara ambaye anaweza akatumia vibaya msamaha huo kwa matarajio kwamba inaweza ikatokea siku moja jambo la hatari. Ikija siku ya hatari, tutaichukulia katika mazingira ya hatari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata wawekezaji wakubwa, anaweza akaja mwekezaji mkubwa sana ambaye kwa kweli ili mradi ule uweze kwenda, unahitaji *offer* hiyo ama utatoa faida kubwa ya ajira, ni vyema jambo hilo, tumekuwa tukililia kwamba hata mikataba iangaliwe na Bunge na ipitishwe na Bunge, ni vyema jambo hilo likaja na Bunge, Bunge likaamua na ripoti hiyo ije itolewe kwa Bunge kama ule msamaha ulifanya kazi iliyokuwa imekusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeshasema kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali tunamwagiza aanze kuangalia uwezekano wa kuikagua hata ile misamaha ambayo ilienda kwa sababu ile ni ruzuku. Namshukuru sana Mheshimiwa Zitto Kabwe kwa uzalendo wake, pamoja na matatizo yaliyompata, lakini bado akachangia kwa maandishi. Tumeipata, na Wabunge wengine mliosema hili.

Mheshimiwa Spika, ni vyema kila fedha ambayo ni ya Serikali iwe kwa namna ya ruzuku ama kwa fedha *cash,* lazima itumike ilivyokusudiwa na Taarifa ile ioneshe kwamba imetumika kama ilivyokusudiwa. Hili la misamaha kwa kweli, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania tunaomba tuelewane kwa namna hii. *We have heard a lot of it, we have heard enough of it and enough is enough. We have to start a new chapter. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna jambo lingine nalo ambalo nitaomba nilisemee na Waheshimiwa Wabunge tuelewane vizuri sana. Tuna jambo hili la *Withholding Tax.* Ni kweli, Sekta yetu ya Utalii ni changa. Ni kweli, Waheshimiwa Wabunge wanapata wasiwasi kwamba labda litapandisha bei. Mimi niwaambie tu, kiutalaamu kabisa, kodi hutolewa kwa watu kwa namna mbili. Inatolewa kwa wakazi ama inatolewa kwa wageni.

Mheshimiwa Spika, hii tunayoongelea ya kukodisha ndege ni kodi ambayo kwa wenyeji wanatolewa kwenye faida waliyoipata kwenye kuendesha biashara hiyo ya kwenye Sekta ya Ndege. Akipata faida, anatozwa kodi. Mtanzania akipata faida kwenye sekta hiyo, anatozwa kodi. Kwa mgeni, akija, akipata faida; narudia tena! Akipata faida, anatozwa kodi, ndiyo inayoitwa zuio. Kwa hiyo, tunachofanya, kama tutasamehe, maana yake ni nini? Ni kwamba, Mtanzania akipata faida, tunamtoza kodi, lakini mgeni akipata faida, anaondoka na faida yake nzima nzima bila kutozwa kodi. Hicho ndicho tunachokisema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa sisi tumesemaje? Kwa taratibu za Mikataba ya Kimataifa, akipata faida, ataondoka na faida yake vilevile, anaenda kuilipia kule kwenye nchi yake. Sasa kwa sisi kwa sababu tunajali sana misaada, tunamwacha aende na hiyo fedha, halafu baadaye aturudishie kama msaada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sasa tunasema, kama Mtanzania akipata faida anatozwa kodi; mgeni naye akipata faida atozwe kodi. Hii haihusiani na gharama kwa sababu faida ni mauzo yote, anatoa gharama alizotumia. Kwa hiyo, hata kama hatujamtoza, maana yake ile ni faida tu hatujaitoza anaondokanayo. Kwa hiyo, hili ni vyema sana tukalielewa vizuri sana na twende na utaratibu huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mambo haya yanakuwa hayana uwiano sana. Hebu tuone; hivi kama tusingekuwa tunatoza kodi hii, hivi mnafikiri bei ingekuwa nyingine?

Mheshimiwa Spika, kuna mambo mengi sana watu wanaongelea kuhusu kodi ambayo inahusu walaji. Lakini ukiwauliza, hivi baada ya kuindoa hii kodi, mlaji yeye ananufaika vipi? Linakuwa halina majibu. Kwa hiyo, kwa muda mwingi ambacho tumekuwa tukikifanya, tunanufaisha ngazi fulani ya watu waliopata misamaha ya kodi na hii tunatengeneza jamii ya watu masikini kuendelea kuwa masikini na matajiri kuendelea kuwa matajiri. *(Makofi)*

Silaha ya Kisera inayoweza kupunguza pengo la wenyenacho na wasionacho ni kodi. Unamtoza aliyenacho kiwango kikubwa, unampa huduma asiyenacho ili na yeye aweze kuinuka. Lakini utaratibu wa kumtoza zaidi masikini na kumsamehe tajiri, unafanya masikini aendelee kuwa masikini na tajiri aendelee kuwa tajiri. Ndiyo maana tunataka tufute misamaha ili tuweze kupeleka fedha zile kwenye huduma, masikini naye aweze kuinuka na Taifa letu liendelee kuwa ni la watu ambao wote wanafurahia matunda ya uhuru na amani iliyopo kwenye nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna jambo hili la *SDL* ambalo limeongelewa. Tumeendelea kupunguza kidogo kidogo.Waheshimiwa Wabunge, lakini nawaomba sana, tutambue mwaka huu tuna majukumu gani mbele yetu. Mwaka huu tungeweza kupunguza hata zaidi, lakini tutambue tuna vitu gani vikubwa mbele yetu.

Tuna Daftari la Wapiga Kura. Kuboresha Daftari la Wapiga Kura, linahitaji hela; tuna jambo la Katiba, linahitaji hela; kuna uchaguzi wa Serikali za Mitaa, unahitaji hela; kuna Maandalizi ya Uchaguzi mwaka kesho, 2013 yanahitaji hela. Kwa hiyo, sisi wenzenu ambao tulikuwa tunaandaa jambo hili la fedha, kwa kweli tunakuwa na nia ya kufanya mambo mengine ambayo yameshauriwa na Waheshimiwa Wabunge, lakini tunabanana kwa aina hiyo. Kwa hiyo, tuangalie kwamba nia ya Serikali ni kupunguza kwenye *SDL,* lakini sasa kwa mazingira tuliyonayo, tunaomba mwone kwamba nia ipo na leo hii tumeacha kwa sababu ya mazingira hayo.

Mheshimiwa Spika, angalieeni, fedha hii inaenda kwenye Mifuko ya Elimu ya Juu. Hivi tukipunguza leo hii, mwaka jana tu, 2013 zaidi ya wanafunzi 12,000 waliokuwa na sifa ya kupata mikopo, hawakupata. Leo hii tukiwaambia kwenye chanzo hicho tumepunguza pesa hiyo, tutawaeleza nini; na hatuna fedha nyingine?

Mheshimiwa Spika, mara zote, hata wakati naleta hoja inayohusu mikopo ya Elimu ya Juu, nilisema mwanafunzi akishapata Chuo tu, Chuo kikasema ana sifa ya kuwa kwenye Chuo hiki, anatakiwa apate mkopo 100/100. Lakini leo hii, 12,000 hawakupata mkopo, halafu kwenye chanzo kile tupunguze. Nawaomba wale wanaohusika na kulipa kodi hii watambue kwamba, tunatakiwa tubane mikanda, tunatakiwa tufunge mikanda, watoto wetu waende shule.

Mheshimiwa Spika, inaumiza sana inapotokea mtoto amesoma shule ya kwenye Kata yake, amesomeshwa kwa vitumbua, amesomeshwa kwa kuuza karanga, anafaulu anaenda Kidato cha V na VI; anafaulu, anatakiwa aende Chuo Kikuu, amepata Chuo; ghafla anaambiwa fedha ya mkopo haipo. Siyo fedha ya bure! Fedha ya mkopo ambayo atairejesha,

haipo! Kwa hiyo, ndiyo maana tunasema, ni vyema sana tukabanana. Ndiyo maana tunasema wakati tunabanana hivyo, ni vyema kabisa tuhakikishe na ukusanyaji wa kodi unakusanywa kama ulivyokuwa umekusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme moja dogo tu. Kuna Mheshimiwa Shekifu na dada yangu, Mheshimiwa Gekul, walisema kwa nini magari ambayo yako *grounded* yanatozwa kodi?

Mheshimiwa Spika, hili ni ufahamu tu na ninawaomba watu wote ambao wanahusika na hili wajue. Kama gari imeharibika au iko gereji, unatakiwa uripoti *TRA* ili waiandike kwamba hii limeshaondoka barabarani, na siku ikishatengemaa, uende kudai kibali chako. Hapo huwezi kutozwa kodi. Ukiwa kwenye Mamlaka ya Mapato hapa Tanzania, ukahusika na watu waaminifu na ukahusika na watu wasiokuwa waaminifu, unapata shida sana namna ya ku-*balance*. Ukiliachilia tu hili, hawatafanya kazi, kwa hiyo, ndiyo maana inabidi ukaripoti kwamba, gari lako limeshaharibika ili uweze kuaminiwa kwamba sasahivi haliko barabarani na siku likiwa barabarani uende ukachukue kibali chako na uendelee kulitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, watu wameuliza, kwa nini, mmesema fedha za kwenye mashirika mbalimbali Bajeti zao ziweze kupelekwa kwa *Pay Master General?*

Mheshimiwa Spika, katika ile tuliyokuwa tunasema ya kutengeneza nidhamu ya matumizi ya fedha za Umma, kwa kweli tumeona kama Mamlaka ya Mapato inakusanya fedha zote na inapeleka bajeti, ni vyema pia Mashirika ya Umma yanayokusanya maduhuli, ijulikane yanafanyia nini zile fedha. Watanzania huwa tuna katabia ka kuogopana kuambizana ukweli. Tunasema mtu ukimwambia ukweli, umemtia aibu.

Mheshimiwa Spika, hivi mnajua kama leo hii kuna wanafunzi hawana madawati? Leo hii kuna watu ambao hawawezi wakapata *panadol?* Leo hii kuna watu hawana maji? Leo hii kuna watu hawana fedha za mikopo? Hivi mnajua kwamba kuna baadhi ya Bodi za Mashirika zinafanyikia nje ya nchi? Hivi mnajua baadhi ya Mashirika, timu nzima inajaa Daraja la Kwanza la Ndege, Daraja la Pili la Ndege, wanaenda mwezi mzima kufanya Semina nje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunataka vitu vya aina hii Mlipaji Mkuu wa Serikali aseme havina maana, viondolewe na visipitishwe na wao wafanye vitu ambavyo vina manufaa kwa Taifa hili. Kwa kipengele hiki hiki naagiza Wizara, Idara zinazojitegemea, Mikoa, Manispaa, Majiji, Halmashauri, Wakala na Taasisi, Mamlaka zinazokusanya maduhuli, zianze kutumia mfumo wa *electronic* ili fedha ile iweze kujulikana kwamba hiyo ndiyo iliyokusanywa na ndiyo iliyotumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, narudia tena! Mkisema umeagiza kama nani; naagiza kwa niaba ya Waziri wa Fedha. Hilo linahitaji litekelezwe na tupate taarifa yake tujue limeshafikia wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na malipo yake, yafanyike! Hatuwezi tukawabana wafanyabiashara wadogo wadogo, halafu Taasisi zile zile ambazo ni za Serikali ambazo lugha yetu ni hii, zikabaki kutumia risiti za kuandika na kuweka *forgeries* ambazo hazitoi sura halisi ya fedha ambayo ilitakiwa itumike.

Mheshimiwa Spika, hili amelisemea na Mheshimiwa Selasini. Tulishasema na nilisema juzi wakati nachangia. Tutakagua madeni yote kabla hatujalipa. Lakini Wahasibu na Wakaguzi walioko katika Wizara, Idara na Halmashauri wakileta yale madai kwamba, haya Wizara ya Fedha lipeni, wakati tukikagua, tukiikuta tofauti, yule aliyetuambia lipeni, anatakiwa aanze kutafuta kazi nyingine ya kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ni ile ile, Wahasibu ni wale wale, Wakaguzi ni wale wale, shule walizosoma ni zile zile; kwa nini Mkaguzi wa Wizara ya Fedha ama Mkaguzi Mkuu aone tofauti na yale aliyoletewa? Watu wanakuwa hawako *serious* na kazi walizopewa. Na leo hii katika Taifa hili kuna watu wengi wanatafuta kazi. Tunaweza tukapangua timu yote iliyoko Ofisini, tukaweka timu mpya leo leo na kazi ikaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna vijana wana *spirit* kubwa kabisa ya kufanya kazi, wanasubiri kazi zaidi ya miaka minne, wako *reserved* hata hawajaanza kupasha. Sasa mtu ambaye ataleta hesabu akasema Wizara ya Fedha lipeni hii, tukikagua tukakuta badala ya Shilingi milioni 600 zilikuwa Sh. 600,000/=, yeye aanze kutafuta kazi mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii naisema na Mheshimiwa Mama Celina Kombani upo. Kama Sheria za Kazi haziruhusu hii, ni vyema ukawahisha sana, ukabadilisha hiyo. Nasi kwenye udhibiti wa fedha, hili ndilo tutakalopendekeza. Lazima fedha Umma iheshimiwe! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna jambo lingine liliongelewa la wafanyabiashara, la leseni. Waheshimiwa Wabunge, nawaombeni sana kwenye hili…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante  sana. Hiyo ni kengele ya pili!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. MCHEMBA):** Mheshimiwa Spika, basi niwatakie tu Waislamu wote Ramadhan njema, na kwa wale wa Jimboni kwangu, Iramba, tende ziko njiani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa namwita Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Malima? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA):** *Bismilah Rahman Rahim!*

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru wewe, Naibu Spika na Watendaji wote wa Bunge. Naomba nimshukuru Mheshimiwa Saad na Kamanda Mwigulu Nchemba na Watendaji wote wa Wizara yetu. Naomba niwashukuru na niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao katika kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa, naomba niwashukuru Wana-Mkuranga kwa kuitikia mikakati ya maendeleo yanayosimamiwa na Mheshimiwa Mbunge wao wa *CCM*.

Mheshimiwa Spika, tunajadili *Finance Act*. Nilikuwa napitia pale, kuna bingwa mmoja alisema, Sheria kama hizi ni *Living Organisms.* Ni vitu vilivyokuwa hai! Kwa hiyo, vinavyoendelea kukua, alisema, *it is supposed to grow in experience changes that demonstrate maturity continuously.* Yaani Sheria kama hii inatakiwa kila mwaka mnapokaa mnaingalia, mnaona ukuaji wake na ukomavu wake katika kutekeleza yale ambayo yanaitikia mikakati ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo naomba niseme, mimi binafsi nawapongeza walioshiriki wote, lakini na Kamati ya Bajeti pia na Serikali na Watendaji wangu wote wa Serikali kwa vile tulivyokaa na kuhakikisha kwamba tunajaribu kuleta jambo ambalo linakwenda ku-

*address* matatizo yanakusudiwa. Ni ukweli kabisa kwamba, labda kama ulivyosema mwenyewe jana na juzi kwamba tungepata muda wa kutosha tungekuja na jambo ambalo ni kamili zaidi. Kwa hiyo, tunatoa ahadi kwa Waheshimiwa Wabunge na kwa Taifa letu kwamba tutakwenda tukiboresha vitu kama hivi ambavyo vinakwenda kugusa maendeleo ya Watanzania moja kwa moja. Ni lazima twende tukivifanyia kazi na tathmini moja kwa moja, *continuously,* ili viende vinaboreka.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo nililisema na nalisema tena kuhusu suala la adhabu kali kwa wale wanaokwepa kodi, wanaosababisha uharibifu, wanaosababisha uharibifu kwenye mapato. Hata tukija na *Finance Act* iliyotoka Mbinguni ikaja kusema bwana, kuweni na *Finance Act* ya namna hii, lakini kama Wasimamizi wetu ndani na nje ya mifumo ya Serikali, kama watu wanakwepa, hatutoki! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namna mojawapo ya kusema hivyo, tumeliangalia. Kuna suala la nidhamu katika matumizi, ambalo amelisema Mheshimiwa Selasini na Mheshimiwa Shekifu; bado tunaliangalia na kusema kwamba, ni lazima tujielekeze huko kwenye adhabu kali sana.

Mheshimiwa Spika, hili la misamaha ya kodi, kuna jambo ambalo tumekuwa tunalirudia. Kuna neno moja ambalo linateleza pale; lakini misamaha ya kodi tumeendelea kusisitiza, kuna miradi ambayo ina tija kubwa. Kuna ile miradi ambayo ni *ground breaking, once in a million.* Ikitokea miradi kama ile, huifanyi tena katika miaka 50, 60, 70. Tanzania tuna miradi kama hiyo kama minne, mitano. Tuna Mradi wa Reli ya Kati.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Reli ya Kati, tutakapoukamilisha, *standard gauge* kilometa 1,800 zile unakwenda mpaka Shinyanga – Mwanza - Mpanda, Kigoma; ule mradi unafungua Tanzania yote. Pia ni lazima iendane na Miradi ya Bandari; Mradi wa Bandari ya Dar es Salaam, Bandari ya Kigoma, Bandari ya Kemondo na Bandari ya Bukoba. Sasa ukishakuwa na miradi ile, unajenga *net-working* ambayo ukitoka hapo Tanzania inakuwa ni *hub,* unatumia *geographical advantages* zake.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mwakyembe yuko pale, atakwambia. Mradi huo tunaouzungumzia wa reli ni *seven billion dollars* kuukamilisha. Yaani kwa kifupi ni Shilingi trilioni 12. Sasa siyo mradi ambao tutakuja hapa tukasema aah, Serikali ikaenda kuujenga.

Mheshimiwa Spika, mradi kama huo, nawaambia Watanzania na Waheshimiwa Wabunge, bila *PPP* hatutoki! Ni mradi ambao; jamani, mimi nimekuja hapa Bungeni mwaka 2005. Tangu 2006 tunazungumzia mradi huo. Sasa Waheshimiwa Wabunge, ni lazima tufike sehemu tuseme kuna *economics* na kuna *facts* na kuna mahitaji tunayotaka sisi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna Serikali ya Tanzania ambayo yenyewe inakusanya trilioni 12 kwa muhali kwa mwaka, halafu tuchukue hizo trilioni 12 tuzi-*commit* kwenye Reli ya Kati; hatuwezi kulipa mishahara, hatuwezi kulipa madeni, hatuwezi kulipa nini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mradi kama huo ni lazima tukubaliane humu ndani, kwamba tutatoka kwenda kuufanya kwa njia ya *PPP* na kwa maana hiyo kwamba; kwa mfano, kile kipande cha Serikali ikiambiwa nyie asilimia 30 ni Serikali; hiyo asilimia 30 ya *12 trilion* ni *four trilion.* Lazima twende sehemu tukatafute na sisi kukopa ili tuendane na wawekezaji wa namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuna *concessions* ambazo tunaweza tukafanya. Naomba niwasihi Waheshimiwa Wabunge wenzangu, miradi mikubwa kama hii ya Bandari ya Dar es Salaam;

sasa hivi Bandari ya Dar es Salaam inasemwa kwa sababu ya *efficiency* zake. Kitu ambacho kingeweza kufanywa na Bandari ya Dar es Salaam sasa watu wanakimbilia Beira, wanakimbilia Mombasa, kuna watu wanakimbia mpaka Durban kupeleka mzigo *DRC* wakati sisi Bandari ya Dar es Salaam na Tanga tuko karibu zaidi. *Why?* Ni kwa sababu, hatuna *economic efficiencies* za *Port Operations.*

Mheshimiwa Spika, haya ni mambo ambayo hatuwezi kuendelea kuyapeleka mbele. Tutaingia kwenye ubia, tutakopa, tutatoa *concessions* kwa wawekezaji, lakini kwa maana ile ambayo imepimwa na inaonekana ina tija ya moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, niongelee kuhusu miradi ya umeme ya Mchuchuma - Liganga kwa mfano. Mchuchuma - Liganga kuna miradi minne ya pamoja. Kuna Mradi wa *Mining Operation* ya makaa ya mawe, mkubwa! Kuna Mradi wa kuzalisha *Mega Watt* 600 za umeme, mkubwa; kuna Mradi wa Kuzalisha Chuma kutokana na *Iron Ore;* lakini kuna Mradi wa Reli wa kutoa ile *Iron Ore* pale Liganga kuipeleka ama kuunganisha na *TAZARA* ama kuileta Mtwara. Kila Mradi mmoja katika huo ni *more than almost 700 million Dollars.* Sasa siyo miradi ya hovyo hovyo na mirdi kama ile tafuta Afrika nzima iko mingapi? Hupati! Hata haizidi minne, mitano.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba niwasihi Waheshimiwa Wabunge kwamba wanapokuja Wawekezaji kwa jambo kama hili, tunapomwangalia Mwekezaji au Serikali itakapokaa naye, mradi kama ule, tunajua ni miradi minne, mitano Afrika nzima; tutatoa *concessions* kwa kuangalia manufaa mapana ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzetu wanafanyaje? Miradi kama ile ambayo inakuwa ni *special cases,* unapomaliza Serikali kuingia ubia na mwekezaji, unakuja Bungeni kusema.

Kwa hiyo, niseme na ni *commitment* ya Serikali kwamba kama tutaingia ubia, sisi Wizara ya Viwanda, Wizara ya Uwekezaji, na kadhalika, ni lazima tuje Bungeni tuseme; jamani, tumeingia mradi, kwa sababu ule ni mradi pekee.

Mheshimiwa Spika, huezi kuu-*treat* mradi wa Mchuchuma, ambao ni *3.54 billion dollars* sawa na mradi wa uwekezaji wa Dola milioni 20. Hatuwezi! Lakini maelezo yake haya ni lazima tuje tukae kwenye Kamati za Bunge, lakini tuje kwenye Bunge Zima isomwe Taarifa ya kusema Serikali imeingia ubia kwa mradi moja, mbili, tatu, nne ili mambo haya pia yaweze kuleta uwazi na kuondokana na fikra za kwamba kulikuwa na mambo ya kanjanja mle ndani.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni hili la wafanyabiashara wadogo. Katika hoja ambazo zilizungumzwa na Waheshimiwa Wabunge, naomba niliseme kwamba limezungumzwa sana.

Mheshimiwa Spika, imezungumzwa kuhusu wafanyabiashara wadogo kuwa ni *tax base* ambayo haijarasimishwa, *it has not been formalized;* ni kweli, tumejaribu kwenda na njia ya *EFDs* lakini tunakwenda vizuri. Mheshimiwa Waziri amelitolea msimamo mzuri.

Nataka niseme tu kwamba, wenzetu huko nyuma kuna baadhi ya nchi kama General Lee kule *South Korea* 1964, kwenye mifano ya uchumi tunaizungumza sana South Korea, lakini *Harvard School of Governance* inasema, South Korea haikutoka isipokuwa iliwahamasisha wafanyabiashara wao kujua kwamba na wao wana mchango wa kuweka kwenye maendeleo ya kiuchumi. Sasa walichofanya ni nini?

Mheshimiwa Spika, walitengeneza mikakati ya kufanya sekta mdogo ijue kwamba nayo ina nafasi ya kuchangia. Kwa hiyo, ile misamaha ya kodi ambayo sisi tunasema misamaha ya

kodi kwa watu wakubwa na nini na nini; kuna baadhi ya misamaha inaweza kwenda kwa wale wafanyabiashara wadogo. Unaifanyaje hiyo? Kwa mfano, nilikuwa naangalia pale kwenye utafiti, ile *level* ya *presumptive tax,* wale wamesema kwa mfano, mtu anayeshiriki kwenye biashara ambazo zinachangia kwenye kilimo, mtu ambaye anaanzisha biashara ambayo inaanzisha *packing* ya mahindi na kubangua na kadhalika kule kule Sumbawanga, anaanza mwenyewe anabuni mradi mdogo, unamhamasisha ile *tax heaven* unaweza kumpa *tax heaven* ya miaka mitatu, minne, mfanyabiashara mdogo ili na yeye akue aweze kuchanganya zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivyo vitu ambavyo wenzetu wamefanya, vinahitaji utafiti. Labda niseme kwamba, na sisi tutakwenda tukiangalia namna ambavyo wenzetu wamefanya. Haya masuala nimesema mwanzoni, ni viumbe hai, *these are living organisms,* vinakwenda vikiboreshwa kila siku. Hamuwezi Waheshimiwa Wabunge, wamelalamika, Waziri wa Fedha Kivuli amesema amesema bajeti ya Amir Jamal ndiyo hii hii; si kweli. Ametupiga kidogo ni sawa, lakini huwezi kuchukua bajeti ya Amir Jamal ya mwaka 1977 ukailinganisha na hii hapana, hii vitu vyake vikubwa, hii ni ya sayansi na teknolojia na mambo ya dijitali. Niseme tumeridhia.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo Waheshimiwa Wabunge wamelisema sana, kuhusu ufanisi wa bandari na uchangiaji wake kwenye Uchumi wa Tanzania. Jambo ambalo limezungumzwa kwa kiasi kikubwa ni suala la mahusiano ya Mamlaka ya Bandari na *TRA*; kila mmoja anasema huyu anamkwaza mwenzake. Sasa hili limezungumzwa, Waheshimiwa Wabunge wamelichangia, tayari *TRA* wameanza kuchukua hatua stahili nyingi tu. Naomba niseme kwamba, kwa mfano tu ni kwamba, kwenye masuala ya ushuru wa forodha, miaka tisa iliyopita tulikuwa tunakusanya trilioni 1.7, mwaka huu tunatarajia kukusanya trilioni 3.9. Ukusanyaji huo unaenda na *volume of trade*. Kwa hiyo, hii ni ishara kwamba, *volume of trade* inaongezeka, lakini bado kwa *geographical advantage* iliyokuwa nayo Tanzania *we can do better*.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge, naomba nimtambue Kiongozi wa Upinzani, Mheshimiwa Mbowe, Mheshimiwa Zungu, Mheshimiwa Abbas Mtemvu na Mheshimiwa Halima Mdee wamelisemea sana ni hili suala la *property tax* na *specifically property in Dar es Salaam.*

Mheshimiwa Spika, wenzetu wanachofanya, ukiwa na *property* yako imekuwa *evaluated* kwa shilingi milioni mia tatu, mia nne, kodi zake zinakwenda zinapanda. Sasa hebu si tuangalie tu, Masaki ile, Dar es Salaam ile, Mikocheni ile, kuna maeneo kule Tegeta na wapi, nyumba hamsini za Dar es Salaam zinaweza zikalipa *property tax* ya Iringa yote au Mbeya yote. Sasa kama Dar es Salaam haikusanyi *property tax* ya kutosha, *something must be wrong,* kwa sababu ukiangalia *volume* ya nyumba zinazojengwa Dar es Salaam, hakuna nyumba inayojengwa chini ya milioni mia mbili au milioni mia moja hamsini. Milioni mia moja hamsini tayari ni nyumba kumi kwenye Mikoa mingine, *except* Arusha na Mwanza.

Mheshimiwa Spika, kuna ushauri umetolewa wa kuanzisha hii *Real Estate Regulatory Authority,* Serikali tumeikubali, tunakwenda kuangalia. *In the mean time,* hizo Manispaa na Halmashauri nazo ziangalie, kwa sababu hili ni jambo ambalo limekaa pale na ikibidi ndiyo yale aliyokuwa anasema Mheshimiwa Mwigulu, hizi Idara za Ardhi kwenye hizi Manispaa na Halmashauri, kama zinashindwa kufanya kazi hii waje watu wengine wafanye.

Mheshimiwa Spika, kuna suala hili la ushuru wa bidhaa kwenye vifaa chakavu nyumbani, ofisini na kadhalika. Serikali imelichukua hili, lakini katika mantiki hii nilitaka kusema tu kwamba, kuna Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia masuala ya utozaji kodi kwenye huduma za jamii, *taxation on social services,* kama elimu na afya na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, elimu na afya unaweza kusema utaweka misingi ya kodi, lakini misingi yake ya kodi haipo kwenye *capital expenditure*. Misingi ya kodi mle kwa wenzetu wanavyofanya ni kwenye utoaji wa huduma zenyewe. Sasa, kwa mfano, tunajua sisi nataka nitoe mfano wa Marekani, Marekani ziko Hospitali binafsi, lakini ukienda *Mount Sinai* siyo sawa na Hospitali nyingine, *Mount Sinai* ni zile Hospitali ambazo ukiweka mgongo tu dola 10,000. India yenyewe tunakokwenda, sisi tunapeleka wagonjwa wetu wote Apollo, lakini India kuna Hospitali moja inaitwa Fortis. Ukienda kuweka tu mgongo Fortis ni mara tatu au mara nne gharama yake ya hiyo Apollo.

Sasa na sisi tunasema na sisi Tanzania tutaendelea kuruhusu uwekezaji kwenye huduma za jamii; kwenye shule na kwenye hospitali; lakini lazima tukubaliane kwamba, yule ambaye anaenda kuwekeza Hospitali kwa ajili ya watu wa Babati, anawatoza shilingi elfu ishirini, hamsini, kuweka mgongo kwa huduma ya siku moja, tofauti na yule ambaye anaweka Hospitali Masaki ambayo kulala mgongo ni dola 2,000. Kwa hiyo, *these are things that within the tax framework,* pamoja na kwamba zote ni huduma za jamii, lakini lazima tutakuwa tunakwenda tukiziangalia tofauti kwa madhumuni ya *taxation*.

Mheshimiwa Spika, hili lingine nimelisema la *presumptive tax* na namna ambavyo wenzetu wamekuwa wanaliangalia suala hili, katika kuangalia namna ambavyo watawafanya wafanyabiashara wadogo wawe walipaji wa kodi ya hiari. Hili lingine ambalo limeletwa na Wabunge na hasa Mheshimiwa Jitu Soni na Wabunge wengine ni suala la kodi kwenye vifaa vya pembejeo na mashine na kadhalika kwenye vifaa vya kilimo, lakini wengine wameleta wafugaji, wengine wameandika masuala ya wavuvi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hili la kodi tunatambua limekuja tangu mwaka jana na mwaka juzi, Mheshimiwa Jitu amelisemea sana. Labda niseme tu katika hili, ziko kodi kadhaa ambazo kimsingi ni kodi ndogo ndogo lakini zinawatoa Watanzania walio wengi katika kuwafungulia maisha yao kwa wingi. Hili la kodi kwenye vifaa vya pembejeo za wakulima na vupuri vya vifaa vya kilimo, vya uvuvi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kuna kodi nyingine ambazo wale watafiti wanaochangia kwenye maeneo kama haya, nao wanapata *benefit* hizo za kodi kama hizo. Sasa hizo ni *tax structures* ambazo sisi hatujaendelea kuziangalia, lakini watafiti wanaoingia kwenye shughuli hizi za kilimo nao wanapata *concession* zao.

Jambo ambalo ni lazima tuliangalie kwa karibu na Serikali tumekubaliana na Mheshimiwa Kamani ni namna ya kuangalia wale wanaotaka kufanya biashara ya kuzalisha samaki, mashamba ya samaki *(aqua culture)*. Sasa ina uwekezaji kidogo mkubwa, lakini *traditionally* Dunia nzima, inafanywa na wawekezaji wadogo kwenye Ziwa Victoria, ziwa Tanganyika, Pwani ya Mwambao, lakini wanahitaji vifaa fulani fulani ambavyo vinawafanya wawekeze kwenye mbegu za samaki. Vitu kama hivi, *aqua culture,* vitabadili kabisa uvuvi wa Tanzania. Tumesema ni jambo ambalo hatujalifanyia utafiti kamili, lakini tumekubaliana na watu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwamba, tutakaa na kufanya nao kazi kwa karibu ili tuangalie namna ya ku-*address* suala hili.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ambalo nilitaka kulisemea ni suala la Uvuvi wa Bahari Kuu. Linasemwa sana kama chanzo cha mapato; ni kweli. Pamoja na *aspect* inayosemwa ya kukata leseni, tulipokuwa kwenye Kamati ya Fedha mwaka 2007 tulipendekeza Serikalini na bahati tulikuwa tunaipendekeza kwenye Wizara ya Fedha na sasa ndiyo najipendekezea mwenyewe. Tulisema wakati huo kwamba, lazima Uvuvi wa Bahari Kuu uwe na uwezo wa *monitoring for compliance*. Kuna meli ziko kilomita 50, 60, 100, kule zinavua kwenye bahari kuu, huwezi

kuzifuata kule na hii mitumbwi. Kwa hiyo, tulikubaliana na hili jambo tunaendelea kuliangalia; *investments* kwenye masuala haya uwekezaji wa Bahari Kuu, lakini pia na *marine research.* Mtu hawezi kusema alikwenda akavua kwenye eneo ambalo utafiti umebaini kwamba kuna samaki kadhaa, kwa wingi wa kiasi hiki.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba, hilo Serikali tumeliangalia na tunataka tukae tuliangalie. Kama ni chanzo cha kodi, Mheshimiwa Hamad Rashid na Waheshimiwa Wabunge wengine wamelisemea sana, isionekane kuna maneno ya kusema kwamba labda Serikali haisikii na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, kuna Mheshimiwa Mbunge Mahiri, Kijana, amesema Serikali hii inafanya kazi kwa Katiba dhaifu na Katiba mbovu. Mimi nataka niseme tu kwamba, sisi tuliokuwepo humu ndani ndiyo Katiba yenyewe hiyo inayotuongoza. Sasa ukiutemea mate mkono unaokulisha basi muhali, lakini kuna Sheikh mmoja, Imamu Hathali alisema, unapokaa unabishana na mtu unamwuliza je, kijana una umri gani? Anasema nina umri kadhaa. Umeshabalehe? Ndiyo. Umebalehe tangu lini? Ndiyo. Umeoa? Aaah. Sasa ukishakusanya majibu yote yale ndiyo unapata nafasi ya kujibishana na mtu. Kwa hiyo, mimi naomba niseme tu kwamba, katika hili hii Katiba tuliyokuwa nayo ndiyo inayotusimamia sisi humu ndani, tunaapa juu yake na mimi naomba tu kwa sisi wote kama tunaona ina madhaifu, ina udhaifu, ina uchache na nini, sehemu ya kuibadilishia ni humu ndani; kwa hiyo, tukutane tena mwezi wa nane humu ili tuwekane sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nisihi na niseme kwamba, bado Serikali iko *committed* kuboresha vyanzo vya mapato, kwa utaratibu huu wa kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge, lakini kurudi pia na kuambizana yale yanayofanyika ili sote tukienda sawa, tukienda huko mbele, tunajua utekelezaji wa jumla wa mambo moja, mbili, tatu yanakwenda katika hali hii.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo, kabla sijagongewa kengele, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Asante. Hapa kuna Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Dunstan Kitandula, anaomba Kamati yake ikutane saa saba na nusu katika Ukumbi Namba 227.

Jana niliwatangazia kwamba, kuna semina. Mheshimiwa Mabumba, Katibu wa Chama cha Wanaohusika na Hifadhi ya Miradi ya Wanyamapori, anasema; kwa mara nyingine tena naomba uwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Chama cha Wabunge kinachojihusisha na Uhifadhi wa Wanyamapori kwa kushirikiana na Mradi wa *LSP*; *LSP* ni Mradi wa *Legislative Support Program,* leo tarehe 28 katika Ukumbi wa Msekwa, wameandaa semina kwa Waheshimiwa Wabunge wote, itakayohusu usimamizi bora wa wanyamapori. Kwa hiyo, kuna semina baada ya kikao hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa mtoa hoja.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na mimi kupata nafasi hii adhimu kabisa ya kuhitimisha hoja yetu ambayo imechangiwa na Wabunge. Michango yao yote ni muhimu, makini na mingine inatupa changamoto ya kwenda kuifanya kazi zaidi.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na nawashukuru Wabunge wote, ambao wameendelea kuchangia hoja hii. Kwa dhati kabisa naishukuru Kamati ya Bunge ya Bajeti, tumefanya kazi usiku na mchana katika kukamilisha hatua hii. Vilevile nawashukuru Naibu Mawaziri; Mheshimiwa Adam Malima na Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, kwa kutoa ufafanuzi

wa baadhi ya hoja. Kwa dhati kabisa nawashukuru Watendaji wetu wa Hazina na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, tumekaa, tumefanya kazi usiku na mchana; naomba kuwaambia kwamba, tukaze moyo, kazi ni ile ile, tubadilike kuwaletea matumaini Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mengi yameshazungumzwa lakini nitatoa ufafanuzi tu kwa baadhi ya hoja mbili, tatu, ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya punguzo la *PAY AS YOU EARN* kutoka asilimia 13 hadi asilimia 12. Limesemwa na Wabunge wengi kwamba ni ndogo. Kwanza, napenda tu kutoa taarifa kwamba, eneo hili tumekuwa na mashauriano na Vyama vya Wafanyakazi. Kwa hiyo, punguzo hili la asilimia moja ni makubaliano kati ya Serikali na Vyama vyenyewe vya Wafanyakazi. Hawakusema mbili, hatukukubali mbili, tatu, tumesema ni asilimia moja *gradually* mpaka kuelekea katika *single digit.*

Mheshimiwa Spika, tuangalie eneo la punguzo, wengi hatujaangalia, hatujalisemea eneo tulilozidisha, tumepunguza asilimia moja, tumezidisha asilimia 10.4. Kwa hiyo, hiyo ni baraka yenyewe. Mheshimiwa Mbatia amelizungumza si tu kupunguza shilingi 1,600 ni kuongeza 62,000. Kwa hiyo, hiyo ndiyo *approach* ambayo tunakwenda nayo, maana tunachotaka wakati tunapunguza, wakati huo huo tunamwandalia mazingira mazuri mfanyakazi. Shilingi 1,600 huwezi kununua mkate, *I don't know,* labda mkate wa boflo kwetu unauzwa shilingi mia tatu, *we can buy that*.

Mheshimiwa Spika, tumesema kwamba tunakwenda vilevile kutengeneza mazingira mazuri ya mfanyakazi. Tunatoa punguzo, lakini tunampandishia. Kwa hiyo, *actually* anapata *two times* ya *benefit*. Nilitaka kutoa huo ufafanuzi, *concept* hiyo isiwe *mislead.* Hicho ndicho ambacho Serikali tumeamua kufanya.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na wazo la kupunguza umri wa magari ya kutozwa ushuru wa uchakavu kutoka asilimia kumi hadi nane liangaliwe upya. Eneo hili limekuwa *supported* na Mheshimiwa Mnyika, lakini vilevile limechangiwa na Mheshimiwa Mussa Zubeir. Tuangalie wakati tunawasilisha zile hatua za kodi tulisema, kwanza, Mheshimiwa Mnyika, gari lenye umri wa miaka minane kwenda chini, halitozwi kodi ya uchakavu, hakuna hiyo kodi. Kunakuwa kuna kodi nyingine lakini siyo kodi ya uchakavu. Kwa hiyo, kwanza hilo halipo.

Tulichokifanya, gari ambalo lina umri wa miaka minane kwenda tisa, tumelitolea ushuru, yaani ushuru sasa utakuwa asilimia kumi na tano. Mwaka jana kuanzia miaka kumi kwenda juu ilikuwa asilimia 25. Sasa hivi kwa ajili ya ku-*encourage* watu kununua magari mapya, tumesikiliza sana hoja zenu Waheshimiwa Wabunge, tukasema magari yenye umri wa miaka minane kwenda tisa, tutasema kwamba tunatoza ushuru wa asilimia kumi na tano, lakini kwa sababu tunataka nchi yetu Tanzania isiwe ndiyo *dumping place,* kwa sasa magari hayo ya umri chakavu mengi yanakuja. Mengi sana yanakuja na bei ni chee kabisa, kwa hiyo, kuanzia miaka kumi kwenda juu tunatoza 30%.

Mheshimiwa Spika, tumepunguza eneo la magari mapya, lakini tumezidisha eneo la magari machakavu. Kwa hiyo, hiyo peke yake tunawa-*encourage* watu kuanza sasa kununua magari mapya kabisa. Wakati huo huo, pato la Mtanzania linakua, tunajua tunaimarisha maisha ya Mtanzania na *affordability* sasa inakuwa *spread*. Kwa hiyo, nimeona niangalie vilevile eneo hilo ambalo kidogo naona kama lilikuwa halijaeleweka vizuri.

Kodi ya zuio ya uendeshaji wa ndege nadhani limeeleweka vizuri sana. Tunataka kuondosha hii misamaha ambayo haina tija. Kodi hii ya zuio wala haisababishi sekta yetu isikue,

kwa sababu sekta yetu ya utalii *is not all about ndege, is about everything else.* Tunasema kwamba, kwa mfano, Shirika letu la *ATC* linakodi ndege, basi badala ya zile fedha yule mtu kumpa yeye, *afterall* yeye atakwenda kulipia kwenye mamlaka zake huko za kodi, basi bora aingize kwenye mamlaka za Tanzania, ili *at the same time* tunaweza tukamega tukampa yeye *ATC* ikaweza kuimarika. Sasa tunamwachia yule, *ATC* hafaidiki na yule mwingine ndiyo anakwenda kulipia kodi huko. *Once* huku ile kodi ikishakuwa *deducted,* kule anapata *tax credit,* kule hakatwi. Kwa hiyo, *there is no way* kwamba hii ita-*increase* gharama.

*Analysis* hiyo imefanyika na hicho ndiyo kitu ambacho kinaendela. Kwa hiyo, *is a high time now* Watanzania tuchukue kilichokuwa na haki yetu tuendeleze nchi yetu, maana yule anacho ametukodisha ndege tunamwongezea; hiyo haipo. Hayo ndiyo mapendekezo ambayo tumekuja nayo mwaka huu. Mheshimiwa Mbatia, hii siyo bajeti ya Mheshimiwa Jamal *in 1964,* hii Bajeti ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Waziri wa Fedha Saada Mkuya na Manaibu wake; Mwigulu Nchemba na Adam Malima ya 2014. Havikuwepo vitu kama hivyo. *(Makofi)*

Leo Waziri wa Fedha nadhani ni tofauti kubwa, sijaiona Bajeti ya Mheshimiwa Jamal. *I appreciate what he did, from what I hear,* lakini *you can see a very huge different.* Kweli mimi nadhani wakati tuna-*criticize,* uungwana tu tuna-*appreciate* hata zile hatua ambazo tumezichukua. *You completely criticize everything a hundred percent, you might be an opposition* lakini nadhani vilevile na sisi Watanzania tuko hapa kwa ajili ya Tanzania; kuna vitu ambavyo ni vizuri viwe *appreciated,* inatupa moyo wa kuleta mabadiliko zaidi. Sasa ooh soda, soda, kweli lakini kuna mambo mapya mengi tumeyaleta, *it makes a huge difference. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili eneo tumeliangalia sana, *motive* yetu sasa hivi tunakokwenda, tunaendelea kufanya *analysis* ya misamaha hii ya kodi ambayo itakuwa haimletei tija kabisa Mtanzania. Ni eneo ambalo tunapoteza fedha nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kwa mfano tu, ushuru huu wa mafuta. Ipo kwenye sheria, unatolewa na Waziri wa Fedha na mamlaka ya kutoa *exemption* kwenye mafuta, hakuna siku ambayo *file* la *exemption* linakaa siku mbili kwenye meza yangu kama *file* la kutia saini *exemption* za mafuta. Inauma roho, inauma sana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunaomba *support* yenu kwenye hili. Tumeanza tutaendelea kufanya *analysis* kwa misamaha ambayo haiathiri *investment* kabisa, haiathiri uwezekaji katika hali yoyote, tunaomba *support* yenu. Serikali hii imeendelea kuwa sikivu kwa sababu ndiyo kitu ambacho mlikuwa mkitushauri kila mara. *Gradually* tunakwenda kidogo kidogo kufikia asilimia moja ya *GDP*. Hatukusema leo tunaondosha misamaha yote, hapana, tunakwenda tukifanya *analysis* hili halitoleta athari na hili halitoleta athari basi tunakuwa tunaondoka. Tunaomba mtu-*support* kwa hilo. Hiyo ni Bajeti ya Mwaka 2014. *(Makofi)*

Hoja nyingine Mheshimiwa Ismail Aden Rage, aliulizia kuhusiana na Muswada wa *VAT* kuwa *postponed. Effect* ipo kwenye bajeti lakini tuko na *sincere hope* kwamba, Muswada huu wa Sheria utakuja katika Mkutano wa Novemba na tuna matumaini makubwa kwamba, Waheshimiwa Wabunge mtau-*support* Muswada huu. Kwa hiyo, si kama tumeuondosha umekufa, nimeona *some media* wanasema umezikwa; *no*, uko *alive and very active* tunauleta katika Bunge letu la mwezi wa Novemba. Tunaomba hilo mtu-*support* vilevile Waheshimiwa Wabunge, ni nia ya Serikali sasa kuanza kuhakikisha kwamba, yale mambo ambayo yana masilahi ya Taifa tuyafanyie haraka, tuyalete myachukue mya-*prove* ili twende tukayatekeleze.

Mheshimiwa Sika, eneo lingine lilizungumzwa kuhusiana na maboresho ya huduma za bandari; ni kweli huduma za bandari tumeendelea kuziimarisha. Waziri yupo, nilimwona nadhani

katoka, lakini Waziri yupo, anafanya kazi nzuri sana. Bado kuna changamoto bandarini, lakini tunakwenda tuna-*improve*. Wameanza sasa kufanya kazi saa 24 na hatua hii imesaidia kwa kiwango kikubwa, kupunguza muda wa kukaa mizigo bandarini. Vilevile Mamlaka ya Bandari imeongeza idadi za bandari kavu *(In Land Container Deport - ICDs)* hadi kufika 16, zilikuwa 12, ili kupunguza msongamano wa makontena bandarini. Vilevile bandarini hapo katika kuboresha huduma za forodha, *TRA* nayo imeanzisha mfumo mpya wa forodha *TANSIS,* ambao utaunganishwa na mfumo wa *single window*, unaojumuisha wadau wote wanaoshughulikia uondoshaji wa mizigo bandarini kama vile Mamlaka ya Bandari *(TPA),* Wakala wa Meli *(TICTS)* pamoja na wengineo.

Maboresho ya shughuli za forodha yanajumuisha utekelezaji wa mifumo ya *revenue get away, the electronic cargo tracking system* na vilevile *the national single window for trade risk management system* na vilevile vituo vya huduma mipakani, yaani *OCBPS*. Kwa hiyo, kwa utekelezaji tu wa maboresho ya huduma forodha, mapato ya Serikali kutoka forodha, yameongezeka kutoka shilingi bilioni moja katika Mwaka wa Fedha 2008/2009 hadi sasa hivi tumefikia shilingi 2,971,000,000 kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013. Kwenye matarajio yetu, kwa mwaka 2013/2014, hadi mwezi Juni tunatarajia tutafika shilingi 3,900,000,000. *This is an achievement* na tutahakikisha kwamba tunaendelea kuboresha huduma hizi za bandari.

Mheshimiwa Naibu Waziri alizungumzia kuhusu eneo hili la kodi ya majengo *(property tax)*. Mheshimiwa Mbowe, hujaunga mkono hoja, lakini eneo hili umezungumza vizuri sana; tunalichukua, maoni yako tunakwenda kuyafanyia kazi. Sasa hivi Benki Kuu ya Tanzania kuna Mradi wa *Housing Project* ambao *within that* ndiyo tunatarajia kuanzisha *Real Estate Authority.* Kwa hiyo, tumelichukua na maeneo mengine ambayo umetushauri nayo tutayachukua tutakwenda kuyafanyia kazi vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna eneo ambalo limezungumzwa, kodi ya mapato kwa walipa kodi wadogo, *presumptive tax* ni ndogo na haitoki kutengeneza hesabu. Wengine vilevile wamekwenda kwenye eneo hilo wamesema kwa nini wale wanatozwa kodi!

Tuna dhana hii nzima ya kurasimisha biashara ili zile biashara ziko *informal* ziwe *formal.* Sasa wakati tunamtaka mtu aweke hesabu na tumtoze kodi kutokana na hesabu zake ni katika *process* ya kurasimisha. Hatuwezi tukawaacha nje watu kama hawa. MKURABITA ni mkakati mmoja, ni mpango mmoja, lakini vilevile katika eneo la kodi nalo ni mpango mpana zaidi wa kuweza kuwafanya wafanyabiashara sasa wawe rasmi; kwa sababu mtu akiwa anaweka risiti zake alizonunulia bidhaa na gharama alizotumia na vitu vingine, pale ndipo inapompa mtoza mkodi kujua ile gharama yake. Tusipoweka hesabu ndiyo inakuja sasa utakadiriwa makadirio makubwa, lakini kama ungekuwa unaweka risiti zako basi hakuna haja ya wewe kukadiriwa, unaangaliwa hizo risiti zako za matumizi.

Tunaomba tuwa-*encourage* hawa watu kuwa wana-*keep receipt* ili kuondokana na ile adhabu ya kutozwa kodi za kukadiriwa. Hili ni jambo la msingi na ni muhimu na ndiyo nia yetu. Tukienda hivyo ndiyo utaratibu sasa tunawachukua wale *informal sector* tunawaingiza katika *formal sector.* Leo utakuwa huwezi kufanya hesabu zako, lakini *as you move, as you go along, definitely* ukipata *experience* kubwa, utakuwa unaweza kabisa kufanya hesabu zako wewe mwenyewe. Hili ni eneo pana zaidi, *is not about* tunakwenda kuwatoza kodi tu, lakini vilevile ni kuwa-*encourage* wao kuwa wanaweka hesabu, ili sasa na wao wawe wafanyabiashara ambao wako *formal.*

Wao ni wafanyabiashara wadogo wadogo, lakini wakati tunafanya hivi watakuwa wanakua, kwa sababu watakuwa wanapata *experience* ya kuweka hesabu zao na hivyo kuepukana na mzigo mkubwa wa *presumptive tax*; maana kama hujaweka hesabu itabidi

tukisie tu kwa biashara yako. Kwa hiyo, tunaomba sana wafanyabiashara wadogo, kuepukana na tatizo hili, tuweke hesabu zetu sawasawa. Risiti zetu za matumizi tunazotumia lazima tuwe tunazihifadhi ili atakapokuja mtoza kodi, awe anajua kitu gani *exactly* umetumia.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine lilikuwa hili la ufundi stadi, limezunguziwa vizuri na Mheshimiwa Nchemba.

Eneo la kuongeza ushuru wa forodha kwenye nondo na mabati kutoka asilimia kumi hadi 25, labda azma yake ieleweke. Sisi tumeondosha kwanza kwenye nondo, mabati na saruji katika *list* ya *deemed capital goods*. Tuangalie asilimia 25, tunaweza tukasema wenzetu Kenya wameweka, ndiyo wameweka. Kenya wana viwanda vingi sana, kwenye East Africa nadhani wao ndiyo wanaongoza kama siyo Afrika nzima kwenye eneo la nondo na mabati.

Sasa wakati Kenya wameweka asilimia 25 ya *import,* ina maana wanauzia kuleta hizo bidhaa kutoka nje kuingia ndani. Tanzania tunakwenda na sisi tunaweka asilimia 25 *simple* kwa sababu Kenya ameweka, tutalinda viwanda vya ndani, lakini kwa sababu Kenya bidhaa hii wao wanatengeneza kwa wingi, kama sisi tumeshaweka asilimia 25, maana yake zile Kenya sasa hapa ndipo zitakapokuwa soko lake. Itabidi tutumie hizi bidhaa za Kenya. Maana kama tumeshazuia na sisi tumeweka *25 percent import* na Kenya ameshazuia na yeye *25 percent import* na wakati Kenya ana viwanda vingi vinavyotengeneza hivi vifaa kwenye *quality* inayotakiwa, maana yake sasa inabidi yeye auze kwetu, Tanzania ndiyo itaendelea kuwa soko. Hiyo ndiyo *logic* nzima.

Tunafanya hivi, tunaomba Waheshimiwa Wabunge, tutumie *tactics* zetu, jana nimesikia msamiati kwamba, hii ni biashara ya mdomo, fani sijui ya mdomo, kitu kama hicho. Tunaomba tuwe tuna-*encourage* wawekezaji wetu wa ndani au viwanda vyetu, watumie *opportunity* hii kuweza na sisi kuzalisha bidhaa kama hizi zenye *quality* kubwa, tushindane na wenzetu. Kama *quality* yetu itakuwa nzuri, basi na sisi sasa tutaweza hata bidhaa zetu hizi tukazipeleka Kenya, maana wao wameshazuia. Tumeanza na kuingiza kwenye hizi *deemed capital goods,* hatutozi msamaha, yaani tumeondosha msamaha kwenye hili, *at the same time* tuanze kulifikiria hili suala la asilimia 25. Hatujaliweka bado kama Serikali, kwa kuona kwamba sasa sisi ndiyo tutakuwa soko la Kenya.

Kwa hiyo, tunaomba Waheshimiwa mlifikirie hili na sisi tutakuwa tunaendelea kusikiliza ushauri kutoka kwenu. Hoja kubwa sana imeelezewa vizuri na mtaalam, Mheshimiwa Lugola, kuhusiana na kulipa kodi ya mafuta yote *up-front* wakati wa kuingiza mafuta nchini, badala ya utaratibu wa zamani unaopendekeza kulipia kidogo kidogo. Amelielezea vizuri na yeye ni mtaalam katika eneo hili. Ametuambia vilevile tumpelekee hawa vijana waende wakasome kwake; tunashukuru kwa *offer* hiyo…

**SPIKA:** Basi Mwijage huyo.

**WAZIRI WA FEDHA:** Samahani, Mheshimiwa Mwijage. Tunashukuru kwa *offer* na tutakuja kupata *consultation.*

Nia yetu hapa tulikuwa tunafanya huo utaratibu, kwanza, tukumbuke kwamba, utaratibu ule ni *administrative* na ndiyo maana haujaingia kwenye *Finance Bill,* siyo *fiscal,* ni *administrative,* ndiyo maana hatujausoma jana, lakini wakati wa kutoa hotuba tuliuzungumzia. Tuangalie masilahi ya pande zote mbili; masilahi ya Serikali katika kupata fedha zake za kodi, lakini masilahi ya hao ambao wanaingiza mafuta.

Tunapotoa *offers* kama hizi, *very unfortunate*, inakuwa kwa upande wa wenzetu sasa *abuse* inakuwa ni kubwa. Tunatoa kwa nia safi kabisa, lakini *abuse* inakuwa kubwa. Sasa, ndiyo maana tukasema kuepukana na hili basi bora tulipe *up-front*. Kwa sababu ndiyo dhana ya kulipa kodi, umeingiza mzigo wako lipia. Wengine ndivyo wanavyofanya. *Issues* zilikuwa ni hizo tukasema tuwape hizo siku 45. Tunatoa siku 45, baadhi ya wale ambao hawana uaminifu hata kidogo, wanatoa mafuta wanauza, wanazungusha mara tatu, mara nne, mara tano, mara sita, siku hiyo ya 45 ndiyo anakuja kulipa. Ameshatengenza faida *to the extreme* na *government* imesha-*suffer to the extreme. (Makofi)*

Kwa hiyo, sasa tunapotoa *offers* kama hizi tuwe na ushirikiano na ndiyo maana sasa tunapokuja kusema hapa, tumeshaangalia *both ways.* Kwa kuwa sisi Serikali ndiyo tunao-*suffer* zaidi na watu wana-*abuse opportunities* kama hizi, ndipo tunaweka misimamo kama hii. Hatuna nia ya kumdhuru yeyote, hatuna nia ya kumfanya yeyote asafe, lakini kwa nini kunakuwa kuna *abuse* upande mwingine?

Hili ni suala la kiutawala zaidi, tumesema tutakaa na hao watu *once* tukirudi Dar es Salaam. Tumeshapata *communication* na *EWURA,* tutakaa sote kwa pamoja tujue jinsi gani tunakwenda.

Hatuwezi kutoa *statement* hapa tunawapa thelathini, tunawapa arobaini na tano, tunawapa hamsini, *no*, kwa sababu *abuse* ya *opportunity* tuliyokuwa tukitoa ilikuwa kubwa, inayokosesha mapato Serikali na inawatajirisha wengine. Kwa hiyo, ndiyo mantiki ya kupendekeza kile kitu ambacho tumekipendekeza. Waheshimiwa tunaomba na sisi sasa kwa upande mmoja mtuangalie Serikali, jinsi gani tunavyosafa kutokana na *opportunities* kama hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya uhawilishaji wa fedha imetolewa, nadhani ilizungumzwa jana na Mheshimiwa Betty Machangu. Nia ya Serikali ni ile ile, kumpunguzia gharama mteja au Mwananchi. Mwaka jana tulipoileta ile ya ushuru wa bidhaa wa asilimia 0.15, ilikuwa ni mzigo kwa Mwananchi. Kwa upande mwingine tulipofanya *analysis,* ilisababisha watu sasa badala ya kutumia mifumo ya kibenki na mifumo mingine ya kifedha, kwa sasa wanachukua fedha mikononi, yaani wanafanya malipo kwa kutumia fedha tu mikononi.

Kitendo hiki kime-*attract* ujambazi *for sometimes.* Tulipoangalia kwa sababu ya *effect* hii tukasema hapana, bora hii *charge* iwe inatozwa kutokana na ile gharama na ndiyo *practice* ambayo inafanywa na wenzetu. Kwa hiyo, nia ya pendekezo hili siyo kumwongezea gharama Mwananchi, lakini kumrahisishia yeye kufanya *transaction* hizi, kutumia mifumo rasmi ya kusafirisha fedha na gharama yake ni ndogo sana. Hatuamini kama mzigo huo utakwenda kwa Mwananchi, kwa sababu ya *competition,* tuna uhakika kwamba, wengi watashusha, watakuwa wanaweka bei za chini kidogo.

Kwa hiyo, badala ya kutoza 0.15 ya zile fedha, sasa hivi *exercise duty* itakuwa ni ile *charge* ambayo wewe unatozwa. Kwa mfano, kutuma shilingi laki moja unachajiwa shilingi elfu moja, kwa hiyo, hii itakuwa ni shilingi 1,100, lakini yule ambaye unampelekea anapata fedha yake kamili. Kwa hiyo, hii ni kurahisisha utumaji wa fedha kwa njia hizi za Kibenki na za *Telecommunications*. Vilevile kumpatia yule ambaye anatumiwa fedha yake kamili na tunajua kwamba, utaratibu huu utakuwa ni utaratibu sahihi kwa Mwananchi na hivyo kumpunguza gharama na ku-*encourage* uhaulishaji wa fedha kwa kutumia mabenki na mitandao ya simu. Nia yetu nzuri na lengo ndilo hilo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Fatma Mikidadi alituandikia vizuri, tunamshukuru sana. Alikuwa na *concern* kuhusiana na kodi ya mazao ya chumvi iondolewe, lakini tunasema

kwamba, *iodine* yenyewe haitozwi ushuru wa forodha inapoingizwa nchini, kwa sababu ipo katika kundi lile la malighafi ambazo kwa kawaida zinatozwa ushuru wa forodha wa kiwango cha asilimia sifuri. Kwa hiyo, hili halisababishi gharama sana kwa mlaji. Tunakushukuru sana kwa mapendekezo yako. Vilevile alizungumzia kodi ya mapato ya nyumba za kulala wageni. Hili tunasema kwamba, liko TAMISEMI zaidi litakuwa linaangaliwa kadiri tunavyokuwa tunakwenda. Tunakushukuru kwa mapendekezo yako Mheshimiwa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna *notion* moja, kurejesha ada za leseni ya biashara. Labda inachukuliwa kama ni kero. Kwetu sisi kama Serikali tunahisi hii siyo kero na *spirit* yetu ileile ku-*formalize* biashara. Unakwenda kufanya biashara ili usipate bughudha, usibughudhiwe, basi kata leseni yako. Anasema iliondoshwa mwaka 2003/2004, lakini hii imerejeshwa toka mwaka 2012 na taarifa kutoka Wizara ya Biashara wametuambia kwamba, inafanya kazi vizuri. *Spirit* ile ile ya ku-*formalize* biashara, kata leseni fanya biashara yako; *no stress, no hiccups,* ndiyo tunavyokwenda. Hatuamini kwamba, hii ni kodi ambayo itakuwa ya kero, *unless* unaangalia tu katika eneo la ulipaji kodi wenyewe. Hilo tukasema sasa kuanzia mwaka huu leseni zitakuwa zinakatwa kwa kipindi cha mwaka mmoja, miaka miwili kwa mfululizo na mpaka miaka mitatu, kama tunavyokata zile leseni zetu za udereva.

Kwa hiyo, ukishakakata leseni yako kwa miaka miwili, huna haja tena ya kwenda kukata. Ukishakukata leseni yako kwa miaka mitatu huna haja ya kurudi. Cha msingi, Wizara au Taasisi inayohusika, iwe na usimamizi madhubuti katika maeneo haya ya biashara na kuhakikisha hawa wanafanya biashara *accordingly*. Tunaangalia eneo moja hili tutatoa hiyo *opportunity* lakini lazima watatokea wajanja wata-*abuse*. Kwa hiyo, tunaomba Wizara ya Viwanda na Biashara ilisimamie vizuri eneo hili ili isije ikatokea athari yoyote kwa upande wa Serikali, lakini vilevile isije ikatokea athari yoyote kwa upande wa wafanyabiashara.

Mheshimiwa Spika, vyanzo vya mapato kwenye Uvuvi wa Bahari Kuu. Mheshimiwa Hamad Rashid amekuwa mweledi sana na tunamshukuru ameendelea kusisitiza hoja hii bila ya kuchoka. Nasi *commitment* yetu ileile kwamba, tutakwenda kuliangalia kwa udhati kabisa eneo hili. Nimeongea na Waziri kwanza anasema, sheria yenyewe inafanyiwa marekebisho, kwa hiyo, tutakuja kutoa taarifa kuhusiana na marekebisho hayo ya sheria. Vilevile kama Serikali kwa ujumla tutaendelea, tunamhakikishia kwamba tutafanya kazi kwa pamoja. Kumsifu si kwamba tu nimemsifu, ni kweli amekuwa akisisitiza sana kwenye eneo la Uvuvi wa Bahari Kuu. Mpaka sasa hoja imekuwa ni chanzo mbadala Uvuvi wa Bahari Kuu, kwa sababu amekuwa akilisisitizia sana eneo hili.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Zungu, alitoa pendekezo zuri kabisa ambalo tunaweza tukaliangalia kwa kushirikiana na Taasisi husika, kuhusiana na ku-*pop in* ile thamani ya kodi ya Serikali kwenye simu. Maoni ni mazuri na tutashirikiana na *MOAT* na *TCRA* kuona kwa hali gani tunaweza tukalitekeleza. Ni kweli linaweka uwazi na wenzetu wanafanya; kwa hiyo, tutashirikiana kwa pamoja katika kuangalia uwezekano wa utekelezaji wa eneo hili.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Murtaza Mangungu amezungumza vizuri kuhusiana na nidhamu ya matumizi. Kweli tunaweza tukakusanya 120% ya *revenue*, lakini kama hakutakuwa na nidhamu ya matumizi, hatuwezi kufika mahali popote. Tunaomba Waheshimiwa Wabunge, tushirikiane katika hili. Tunaweza tukaja na Sheria ya Bajeti, tunaweza tukawa na Kamati za kila aina, lakini kama hatujashirikiana pamoja katika kulisimamia eneo hili, basi bado tutakuwa hatujafanya kitu. Tumelichukua, kwa upande wetu hatua ambazo tumezisema tutaanza kuzitekeleza ikiwa ni pamoja na kutumia Mifumo ya TEHAMA katika kufanya manunuzi, ikiwa ni pamoja na kufanya *performance based disbursement*.

Mheshimiwa Spika, tunashauri sana na ninaamini kwamba, hii *notion* tayari imeshaingia huko kwamba, tunafanya *performance based disbursement*. Kama kuna eneo ambalo mtu atakuwa hajatumia, fedha haitoki. Madai mengine yanayoletwa tutaendelea kuyahakiki, mifano nimekutoleeni na mifano sahihi kabisa, hiyo ndiyo hali ambayo ipo sasa hivi. Kwa hiyo, tutakwenda kwa uangalifu mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Khalfan Hilaly Aeshi umezungumza vizuri kuhusiana na yale madai na kama tulivyokwambia, tutalifanyia kazi eneo hili kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo tu-*fast truck* haya madai ya wazabuni.

Mheshimiwa Esther Bulaya, kama ilivyo kwa Mheshimiwa Hamad Rashid na Uvuvi wa Bahari Kuu, Mheshimiwa Esther Bulaya na vijana. Yeye na vijana na ana hoja ya msingi sana. Katika eneo moja ambalo tumefanya *addition* ya fedha ni hili, tumeongeza *two billion*. Tutaendelea kusimamia tuhakikishe zile fedha zinawafikia walengwa. Kwanza, tutazitoa lakini zinawafikia walengwa. Tunaomba sana tushirikiane pamoja na Wizara ya Vijana kuona fedha zile zinakwenda na vijana nao wanazifanyia kazi kama ilivyokuwa imekusudiwa.

Mheshimiwa Esther Bulaya, nataka tu nikupe *comfort* kwamba, tunalichukua eneo hili na sisi unatupa *challenge* ya kwenda kusimamia zaidi. Tunataka vijana wetu wawe na ajira, wapate ajira na wawe wanaendelea kujiimarisha kutokana na fedha hizi za Mfuko wa Vijana.

Mheshimiwa Dkt. Shekifu tunakushukuru sana na wewe kwa mchango wako na *support* ambayo umetupa. Eneo hili la *imported furniture*, kwa sababu tu ya kuhimiza matumizi ya samani ambazo zinatengenezwa hapa ndani, ndiyo maana *imported furniture* tumezitoza kodi. Vilevile *concentrates* tumewekea kodi ili hao wenye viwanda watumie mazao yetu ya ndani. Ita-*create* ajira, itaongeza *supply,* lakini vilevile tunaamini kwamba, hata hizi *products* zitakuwa zinapatikana kwa urahisi zaidi. Kwa hiyo, tunakwenda sambamba na mawazo yako Mheshimwia Dkt. Shekifu na tutashirikiana katika kutambua maeneo mengine ambayo unahisi yatakuwa na mwafaka katika suala hili.

Wengine ambao walichangia ni Mheshimiwa Pauline Gekul na wengine ambao sitawataja, lakini tunashukuru sana kwa michango yao.

Mheshimiwa Jitu Soni, kila siku amekuwa na michango mizuri zaidi na tumeifanyia kazi. Tumekaa naye kwenye Kamati mpaka usiku, kila akizungumza mimi nasema hii ndiyo ya mwisho, zikaja za mwisho kama 20 hivi, wakati huo Mheshimiwa Andrew Chenge kanywa vikombe vya chai kama 40 hivi, tunamsikiliza, lakini ana mawazo mazuri zaidi.

Mwisho wa yote nadhani mengi tumeyazungumza. Mheshimiwa Akunaay, nadhani tumetolea ufafanuzi hoja yake. Mengine ambayo hatujayajibu hapa, basi tutaendelea kuyajibu kwa maandishi na tutaendelea sana kushirikiana katika eneo hili, tunaomba mtuunge mkono ili twende tukayatekeleze.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali wa Fedha Ulisomwa Bungeni kwa mara ya Pili)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2014**

***(The Finance Bill, 2014)***

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Mwongozo wa Spika, hauko kwenye Kamati ya Matumizi, naomba tuendelee na kazi.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Haupo kwenye Kamati ya Matumizi, kwa sababu siyo Bunge, hii ni Kamati ya Matumzi.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Tupo kwenye Kamati ya Matumizi.

**MWENYEKITI:** Eeh, Waheshimiwa naomba tukae. Tupo kwenye Kamati ya Matumizi mwongozo wa kitu gani? Tunapitia vifungu kwa vifungu, nikikaa pale mnaniuliza mwongozo, nikikaa pale mtaniomba mwongozo. Tunaendelea!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani kabla ya kupitia vifungu!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika tuelewane, naomba ukae chini.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Kwa hatua hii hii ya Kamati, jambo linalohusu hatua hii ya Kamati.

**MWENYEKITI:** Itafika wakati wako utasimama siyo sasa! Katibu, hatua inayofuata!

Ibara ya 1
Ibara ya 2
Ibara ya 3
Ibara ya 4
Ibara ya 5
Ibara ya 6
Ibara ya 7
Ibara ya 8 - Pamoja na Jedwali la Kwanza
Ibara ya 9
Ibara ya 10
Ibara ya 11
Ibara ya 12
Ibara ya 13
Ibara ya 14
Ibara ya 15
Ibara ya 16

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamatiya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 17

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 17. Niliwasilisha Jedwali la Marekebisho, ambalo Waheshimiwa Wabunge wenzangu hawana nakala kwa sababu halijasambazwa na ndiyo jambo ambalo nilitaka kuomba utaratibu kuanzia mwanzoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Wabunge wenzangu waweze kufuatilia mapendekezo yangu ya marekebisho niliyowasilisha jana, pamoja na vyanzo mbadala vya mapato, kwa mujibu wa Kanuni ya 109, nitaomba Jedwali ambalo nililiwasilisha lisambazwe ili Waheshimiwa Wabunge wenzagu wawe na nakala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ....

**MWENYEKITI:** Sasa nikueleze kwa nini Jedwali sina hapa na halipo.

Waheshimiwa Wabunge, toka tunaendelea kujadili hoja hii ya bajeti yenyewe, nimetangaza zaidi ya mara nne, wale wote ambao wanafikiri wanataka kufanya mabadiliko katika Muswada walete amendments kwenye Kamati. Tarehe 26, Ofisi yangu imepeleka message kwa Wabunge wote, yule mwenye Jedwali alete. *(Makofi)*

Ninajua ni mafundi sana wa kusema lakini si mafundi sana wa kujibu. Mheshimiwa Kafulila, wewe nimeshakwambia saa zote, sema wewe sasa umalize, kama ndiyo Mbunge kabisa, sema wewe. Usidhani ninapokwambia usiseme maana yake sisemi. Mimi ndiyo Spika, naomba ukae chini. Ninyi kawaida mnataka kuvunja taratibu, tumebembeleza, huyu mwingine Kafulila ameleta asubuhi. Kwa hiyo, mimi nasema hatutaki kubishana katika kundi hili. Kifungu kinaafikiwa?

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 18
Ibara ya 19
Ibara ya 20
Ibara ya 21
Ibara ya 22
Ibara ya 23
Ibara ya 24
Ibara ya 25
Ibara ya 26 - Ikisomwa pamoja na Jedwali la nne (4)
Ibara ya 27
Ibara ya 28
Ibara ya 29

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 30 ikisomwa pamoja na Jedwali

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kupata ufafanuzi kutoka kwa Serikali, juu ya kifungu hiki ambapo Serikali yenyewe ilileta hoja ya kuongeza kiwango cha kodi kwenye ngozi ghafi na Serikali ilipotuletea hoja, ilisema kwamba, ni kwa minajili ya kulinda viwanda vya ndani, kuongeza ajira ndani na kutoa soko kwa wafugaji ndani.

Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri katika majumuisho ya hoja, amesema kinyume na vile ambavyo Serikali imekuwa ikisema. Kamati nayo katika Taarifa yake, imeonesha mashaka juu ya jambo hili kwamba, Serikali haijaonesha utafiti. Nitaomba tujielekeze kwenye sehemu ya Taarifa ya Kamati, ambapo Kamati imeeleza bayana kwamba, Serikali haijaonesha utafiti iwapo hatua hizi zitaweza kudhibiti magendo.

Nimejaribu kufanya consultation na baadhi ya watu wanaotoka maeneo ya wafugaji na wameonesha bayana kwamba, hatua kama hizi zinakwaza kuanzisha viwanda katika maeneo ya wafugaji na kuendeleza viwanda ambavyo vitatoa mazao kwa mazao ya mifugo. Kwa nini Serikali inaleta mapendekezo ya namna hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusisitiza, Kanuni zetu za Bunge zinatoa haki katika hatua hii, Wabunge kuweza kuleta Majedwali kwa mujibu wa Kanuni ya 86, Kanuni ya 109 na Mwongozo wako wewe mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kwamba, Wabunge hatuwezi kuleta Majedwali katika hatua hii ya Bunge …

**MWENYEKITI:** Bakia kwenye hoja!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Nabaki kwenye hoja kwamba, Serikali itoe ufafanuzi juu ya jambo hili na ikubali marekebisho ambayo tumeipatia kupitia Majedwali juu ya jambo hili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. MCHEMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Mnyika aielewe *logic* hii tunayoizungumzia kwamba, lile analolisema, kiutaalam tungeweza kusema anatumia *ceteris paribus* kwamba, *other things remain constant, but in the actual sense other things never remain constant;* yaani kama viwanda vyetu vingekuwa vina-*perform perfectly,* tungesema tunavilinda viwanda vyetu na mfugaji naye anapata faida.

Kinachotokea, ukiweka *zero rate* kwenye ngozi, natoa mfano, ukiweka *zero rate* kinachofuata …

*(Hapa Wabunge fulani walifanya vurugu kuonesha kutokukubaliana na maelezo yaliyokuwa yanatolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha)*

**MWENYEKITI:** Naomba endelea kuzungumza, Mheshimiwa Mnyika, kwa nini huna uvumilivu Mheshimiwa? Acha amalize kusema, Mheshimiwa endelea.

Mnyika, nasema unajiaibisha kwa watu wote, tukiwa katika Bunge…

Haya basi naomba, anasema una nafasi ya kuuliza tena, kwa nini unabaki unaingilia kati, kwa nini msiwe na heshima ndugu zangu wapendwa? Hebu endelea Mheshimiwa Waziri. Kwa maana si wewe peke yako, anatuambia sisi wote tusikilize, sasa siyo unajisikiliza wewe mwenyewe, hee!...

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. MWIGULU L. MCHEMBA):** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kinachotokea…

**MWENYEKITI:** Malezi haya aaah.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. MWIGULU L. MCHEMBA):** Sisi tulichozingatia, tukaona tukiweka *zero rate* maana yake tukizuia kabisa, nilikuwa natolea mfano, tukizuia kabisa ngozi ghafi kwenda nje, maana yake viwanda vya ndani wataokota bure tu zile ngozi na

kuokota bure ngozi maana yake wafugaji tumewaua kabisa kabisa. Lile ni zao la wafugaji na wanalihangaikia. *(Makofi)*

Kwa hiyo, sisi tukaona tusizuie kabisa kabisa na wakati ule ule tusiruhusu kabisa kabisa, kwa hiyo tukatafuta *balance*. Nilisema wakati nachangia kwamba, bado tunahangaikia uwezekano wa kutafuta asilimia ambayo itakuwa ya katikati, *let's say* kama 50 hivi ambayo itawezesha viwanda kuwa vimelindwa na wakati ule ule iwawezeshe wafugaji waweze kupata faida kutokana na bidhaa yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikatolea na mfano, mwaka wa juzi tulisema kwa ajili ya njaa tuzuie mahindi, watu wasiuze nje ya nchi. Tuliwaumiza wakulima, mahindi yao mpaka yakanyeshewa mvua, mtu ana magunia 800 yakanyeshewa mvua na Serikali haikununua. Kisa tulisema tunalina yasiende nje. Kwa hiyo tunasemaje, tunalinda viwanda vyetu vya ndani sawa, lakini na wakati ule ule mfugaji kama anapata soko lililo jenga la mifugo yake afanye hivyo, kwa sababu yeye maisha yake bora ni mazao ya mifugo yake yale yale.

Kwa hiyo ndicho hicho, niwa-*encourage* watu wetu wa viwanda vya ndani ya nchi, wakati tunawalinda na wenyewe wahakikishe wanatoa bei ambayo ni *competitive,* ambayo itawasaidia wafugaji wasitake kupeleka ngozi kwa magendo na tukasema tunavyopandisha bei, kitu gani kinatokea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rwanda hawana kodi yoyote ya kuzuia ku-*export,* kwa hiyo, ngozi zote zinakwenda kwa magendo Rwanda, zikitoka Rwanda kwa sababu wao hawana kodi ya aina yoyote zinapelekwa Mombasa. Tanzania pamoja na kuwa na ng'ombe wengi kiasi hicho, tunaonekana hatuuzi ngozi nje kwa sababu zilikwenda kwa magendo, Rwanda ambao hawana ng'ombe ndio wanaonekana wameuza ngozi. Na mtu anapokwenda kununua ngozi kwa magendo hatoi bei inayomnufaisha mfugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema mimi ni mtoto wa mfugaji na anavyosema ametumiwa meseji, nimetumiwa meseji na kiongozi wa wafugaji nitakusomea kwa sababu naona bado anataka kusema.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

*(Hapa kuna baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wengi walionesha kutaka kuchangia hoja fulani katika kifungu hiki)*

**MWENYEKITI:** Msifanye fujo, hakuna suala lingine, tumeshamaliza hapa.

Ibara ya 31
Ibara ya 32
Ibara ya 33
Ibara ya 34
Ibara ya 35

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 36

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii, lakini labda kwa heshima ya Waziri wa Fedha, nilimuona naye amesimama, kwa sababu ndiye mwenye Muswada nimsikie alichonacho kwenye kifungu hicho kwanza. Ahsante sana.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hapa kwenye kifungu cha 36(3) ni *typos* tu, tunataka kurekebisha. Kwenye sentensi inayoanza *where dividends referred to in subsection (1)*, kwa maana tunafanya *reference* kwenye *the main act, i-read subsection (2)* na Sentensi zinazoendelea mpaka pale tunakwenda *is entitled to a proportionate amount*, ile *amount* tuifute kuwe kuna neno *deduction*, kwa hivyo ita-*read proportionate deduction of withholding tax credit*. Badala ya neno *deducted* tunasema neno liwe *withheld*. Kwa hiyo, hiyo ndiyo iliyokuwa *typo* tu ambayo nilikuwa nataka kurekebisha katika kifungu hiki.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 37
Ibara ya 38
Ibara ya 39

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 40

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Jedwali hili linahusu kodi kwa wafanyakazi na nimewasilisha mapendekezo ya mabadiliko ya kufanya marekebisho kadhaa. Serikali imekuwa ikiahidi kila mwaka Bungeni na hata nje ya Bunge, kwenye Siku za Wafanyakazi na nje ya Siku za Wafanyakazi kuharakisha kufikia tarakimu moja ya kodi ya mishahara ya wafanyakazi; kushuka kwa kwa kodi ya mishahara ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na ahadi hizo za Serikali kwa wafanyakazi na hapa Bungeni mpaka sasa ahadi hizo hazijatekelezwa na mwaka huu Serikali imeleta mapendekezo ambayo kimsingi yanashusha tena kwa tarakimu moja. Kama alivyosema Msemaji wa Upinzani, kama tukiendelea kwa Ari, Kasi na Nguvu ndogo ya namna hii itachukua miaka mingi sana mpaka kufikia asilimia tisa, hii ambayo inasemwa na wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, sasa Mheshimiwa Waziri katika majumuisho yake amesema kwamba, uamuzi wa kukubaliana na asilimia 12 ni matokeo ya Shirikisho la Wafanyakazi kukubali kasi ndogo hii ya kushuka namna hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa tu kulitaarifu Bunge lako kwamba, katika mazungumzo na Serikali wafanyakazi walikwenda na hiyo tarakimu moja, lakini *fallback position* ilikuwa ni asilimia 11. Kwa ajili ya msimamo ambao wafanyakazi walikuwa nao wa asilimia 11, nimependekeza katika jedwali hapa kwamba kodi ishushwe mpaka asilimia 11. Sisi upinzani tunasema tisa, Serikali ya CCM hamtaki tisa, basi angalau mkubali ishuke mpaka 11 na tumeainisha vyanzo mbadala vya mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili katika jambo hili hili, kiwango cha chini cha kutoza kodi, Serikali imeendelea kuweka kima cha Mshahara cha 170,000 kama ndicho kiwango cha chini

cha kuachwa kutozwa kodi, wakati Serikali inajua kabisa hiki si kima cha chini halisi ukilinganisha na gharama za maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo langu ni kwamba kima cha chini cha kutotozwa kodi, yaani cha kodi *nil* kiwe ni 350,000 ili walau tuwaachie fedha wafanyakazi hawa wenye mishahara midogo waweze kupata fedha za kujikimu na maisha yao. Pendekezo hili linaendana na Kambi Rasmi ya Upinzani, lakini vile vile linaendana kwa kiwango fulani na mapendekezo ya wafanyakazi ya kima cha chini cha mishahara cha 315,000 kwamba ndicho kima cha kuachwa kutozwa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti naomba Serikali iyakubali mapendekezo haya ambayo nilikuwa nayo na nimeshayafanyia kazi.

**MWENYEKITI:** Ufafanuzi!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. MWIGULU L. MCHEMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna anayebisha…

**MWENYEKITI:** Tumwite Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Utumishi!

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS, UTUMISHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika Baraza la Majadiliano katika Utumishi wa Umma ambalo liko kwa mujibu wa Sheria huwa tunakaa kupanga kima cha chini pamoja na hiyo *Pay As You Earn*. Kwa hiyo, tarehe 5 Mei, 2014, Baraza la Majadiliano lilikaa, upande wa Serikali uliwakilishwa na upande wa Vyama vya Wafanyakazi viliwakilishwa.

Mheshimiwa Spika, hicho kilio cha asilimia kutoka *double digits* kwenda *single digit* ni kweli ni kilio cha *TUCTA* na sisi tumekubaliana nao, tumesema tutashusha mwaka hadi mwaka. Tumeanzia mwaka 2008, tumeshusha. Tumesema mwaka ambao itakuwa asilimia tisa ni mwaka 2018. Tunakaa, tunapanga, tunakubaliana na si kama alivyosema Mheshimiwa Mnyika ambaye hakuingia kwenye kikao hicho na si *member* wa kikao hicho. *(Makofi)*

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba ufafanuzi katika eneo hili, kwa sababu nilileta mapendekezo ambayo kwa bahati mbaya…

**MWENYEKITI:** Ohooo! Kama ni eneo hilo hilo utaratibu wetu unakataa.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 41
Ibara ya 42
Ibara ya 43
Ibara ya 44
Ibara ya 45
Ibara ya 46
Ibara ya 47

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 48

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi kwenye kifungu cha 48 ambapo zile *deemed capital goods* pamoja na *cement* na nondo zimeongezwa. Naipongeza Serikali kwa hatua hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Kamati tulikubaliana na Serikali kwamba kwenye *Common External Tariff East Africa,* wenzetu wametoka kwenye asilimia 10 kwenda kwenye asilimia 25 na wale wenye viwanda vya ndani *TBS* imetoa taarifa yake kwamba wanafikia viwango vya ubora wa nondo, *according to international standards.* Humu ndani tunazo nondo za kutosha na *surplus* ya zaidi ya asilimia 40. Sasa tukakubaliana kwamba hii ni kuongeza mapato ya Serikali, iongezwe ifike asilimia 25 kama wenzetu walivyofanya ili kulinda viwanda vyetu vya humu ndani.

Sasa naomba ufafanuzi, wakati Mheshimiwa Waziri anafafanua hapa alisema hapana tunabaki kwenye asilimia kumi sisi, wakati wenzetu wamekwenda asimilia 25 na kigezo alichosema ni kwamba ubora. Sasa sisi wenyewe tunalindaje viwanda vyetu wakati ubora, nani anahakiki ubora huo ni *TBS* na imesema ubora huo unafikiwa. Sasa tunalindaje viwanda vyetu vya ndani na hapa ndipo eneo vile vile la kupata mapato ya Serikali, sasa najiuliza, kulikoni au? Kwani Mheshimiwa Waziri tulivyokubaliana kwenye Kamati imekiukwa, inatutia wasiwasi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti kwenye Kamati tulilijadili hili kwa kina na tulitoa hiyo *assurance,* lakini kwa sababu hili ni eneo ambalo liko kwenye *Common External Tariff* na tulisema wakati nilipokuwa nikitoa *summary* ya hii kwamba yale ambayo yanaingia *CET* tutaya-*gazette* katika gazeti hilo la *CET*. Lakini haya mengine lazima tuya-*consider* na sasa hivi tumeshaweka *proposal* twende tukalijadili hili kupata *assurance* ya Serikali kuhusiana na jambo hili.

Mheshimiwa Spika, nimepata nakala ya barua ya kiwanda kimoja kinatoa hiyo *assurance* ya *quality* sina tatizo. Tumepata vile vile katika ngazi ya Kamati barua ambayo inatoka kwa Waziri, lakini hili ni eneo pana ambalo linahitaji kabisa ufahamu wa Serikali, ukubaliano wa pamoja. Kwa sababu wengine tunasema bado *quality* iko chini, wengine bado *quality* iko juu, lakini tumesema kwamba tupate *decision* hasa ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, hatujachelewa, hatuwezi kuingiza hapa. Tukikubaliana kwamba hiki kitu kipo tutakwenda tu tuta-*gazette* katika *Common External Tariff* gazeti la Afrika ya Mashariki. Hatujakwenda mbali na makubaliano ambayo tulikuwa kwenye Kamati. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Serukamba ulikuwa na tofauti au hili hili.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 49

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kwamba tufanye marekebisho kwenye kifungu hicho, lakini naomba kwanza nitoe maelezo ya awali kwa nini napendekeza mapendekezo haya. Inaonekana kwamba kuna *strategic investments* ambazo ni kubwa kuliko haya tunayoyasema hapa kwenye maeneo ya ujenzi wa reli, ujenzi wa bandari na miradi mikubwa kama Mchuchuma na Liganga.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napendekeza kuwe na (c) ambayo inasema *for strategic investment exceeding the threshold, sorry,* kwenye…

*(Hapa Mheshimiwa Fulani alikuwa anauliza kitu kwa mzungumzaji)*

**WABUNGE FULANI:** Endelea.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Hapana, ngoja nimjulishe, nafikiri swali lake ni zuri. Kwenye *section* 49, haijawa *section* ni *paragraph*, kwenye *subsection* 4(a), (b) nilikuwa napendekeza kwamba tuongeze (c) kwa ajili ya ku-*deal* na *special strategic investments.* Kwa mfano, kwenye bandari, kwenye reli na kwenye chuma. Hii ni miradi ambayo sasa hivi inakuja sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza (c), *for the purposes of differentiating strategic investments and the manner that investments shall be considered and enjoy such privileges as may be described by;* nimepewa kitu hapa lakini sikikubali hicho; nasema kwamba *for investments exceeding the threshold stated above*, yaani hizi zilizotajwa kwenye (a) na (b) *the amount shall be prescribed by a law enacted by Parliament*. Kwa maana kwamba kutakuwa na sheria mahsusi itakayo-*deal* na hii miradi mikubwa na sheria hiyo itapitishwa na Bunge. Kwa hiyo, viwango hivyo vitawekwa na Bunge.

**MWENYEKITI:** Naomba Isomwe kikamilifu kwa sababu inaingia kwenye Sheria.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *I am proposing a new (c) to read, for investments exceeding the threshold here in above…*

**MWENYEKITI:** Naomba usome taratibu!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** *Dictation Speed…*

**MWENYEKITI:** Naomba ukae chini kwanza.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** *For investments…*

**MWENYEKITI:** Naomba ukae chini kwanza

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** *For investments exceeding the threshold here in above, that is to say fifty million US Dollars, the amount shall be prescribed by a law enacted by Parliament.*

**MWENYEKITI:** Naomba urudie.

**MWANASHERA MKUU WA SERIKALI:** *For investments exceeding the threshold here in above, that's to say fifty million US Dollars, the amount shall be prescribed by a law enacted by Parliament.* Tunaweza kuzungumzia *threshold,* lakini ndivyo ninavyopendekeza mimi.

**MWENYEKITI:** Tundu Lissu!

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ututendee haki na utendee Bunge hili haki. Umemnyima Mheshimiwa Mnyika kuwasilisha jedwali ambalo kanuni zinataka liwasilishwe Bungeni kwa hoja kwamba linatakiwa liwasilishwe kwenye Kamati, ambao si utaratibu wa Kanuni, halafu Mwanasheria Mkuu wa Serikali analeta kitu ambacho hakijawasilishwa Bungeni, Wabunge hawanacho, hakijapelekwa kwenye Kamati, halafu mnataka tuendelee, tutaendeleaje na upendeleo wa aina hii wa wazi namna hii. *(Makofi)*

Kwa hiyo kama Mnyika amekosa na *Attorney General* amekosa, anachotaka kukileta sasa hivi hakiruhusiwi, kisiingie, vinginevyo Mheshimiwa Mnyika aruhusiwe kuleta alichokuwa amekileta kwa mujibu wa kanuni. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tundu Lissu, nasikitika sana, maneno hayo kutoka kwako. Nasikitika sana, kwa sababu hata wewe mwenyewe unaelewa kabisa kwamba maneno unayoyasema siyo sahihi. Huu ni Muswada wa Serikali, unaweza kufanya *Amendment,* lakini wengine wote kwa sababu ya kuongeza ama kupunguza pesa, inabidi tuweze kufanya *verification. (Makofi)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu Serikali inatakiwa ilete Jedwali. Kwa mujibu wa Kanuni mtoa hoja anatakiwa alete Jedwali, la kufanya marekebisho.

**WABUNGE FULANI:** Hawakusikika.

**MWENYEKITI:** Kama hamna maelezo mengine basi.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Hata yeye mtoa hoja anatakiwa alete marekebisho kwenye Jedwali.

**WABUNGE FULANI:** Hawakusikika.

**MWENYEKITI:** Mmezoea kutokuwa na adabu. Fanyeni hatua mnayotaka kufanya, kila siku mnafanya. Sasa tunaendelea!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Aaa *amendment* analeta…

**WABUNGE FULANI:** Alete Jedwali mahali hapa….

**MHE. JOHN J. MNYINKA:** Aaa, *amendment* analeta. Hata Serikali analeta Jedwali la kufanya *amendment.*

**MWENYEKITI:** Kama hamna maelezo mengine basi.

**WABUNGE FULANI:** Kwa pamoja walete Jedwali…

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**WABUNGE FULANI:** Kuna *double standard.*

**MBUNGE FULANI:** Mnafanya mambo ya nanihi hapa.

Mheshimiwa Spika, Bunge limekushinda.

**MWENYEKITI:** Tumeshazoea…

**MBUNGE FULANI:** Tokeni nje.

**MBUNGE FULANI:** Toka nje mwenyewe. Kwendeni zenu huko, mnafanya mambo ya ajabu kabisa.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** *Double standard* za wazi kabisa hizi.

**MBUNGE FULANI:** Tokeni nje.

**MBUNGE FULANI:** Kamwambie Bibi yako ndiye atoke nje.

Ibara ya 50
Ibara ya 51
Ibara ya 52
Ibara ya 53

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2014**
***(The Finance Bill 2014)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mtoa Hoja, toa Taarifa tafadhali.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima limepitia Muswada wa Sheria ya Fedha *(The Finance Bill, 2014)*. Kifungu kwa kifungu na kukubali pamoja na marekebisho yake.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba taarifa hiyo sasa ikubaliwe rasmi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali wa Fedha wa Mwaka 2014 (The Finance Bill 2014) Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nachukua fursa hii, kushukuru sana, tumeweza kumaliza kipindi chetu cha Bajeti, lakini napenda pia ieleweke, utaratibu wote tunaoutunga ni lazima ufuate taratibu tulizojipangia. *(Makofi)*

Tofauti na *Amendments* za Miswada mingine kwa mujibu wa Sehemu ya nane, unaweza Mbunge kuleta mabadiliko hapa, lakini kwa mujibu wa Bajeti, ni lazima tu-*verify* zile *figure* tunazozisema. Hawezi mtu mmoja akaja na *figure* yake hapa tukakubali sisi hivi hivi kwa sababu utekelezaji wake hautawezekana, lakini kwa mujibu wa Sheria na Utaratibu. Hata Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ameleta kitu kinachobadilisha mabadiliko tungelihoji, lakini tunasema kwa kiwango cha Miradi mikubwa iletwe hapa na hiyo ndiyo kimekuwa kilio cha Wabunge siku zote. *(Makofi)*

Kuhusu kama Spika, anapendelea, iko wazi kwamba nafuata Kanuni, *and I am strictly about that.*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA FEDHA:**

Hati za Uhamishaji wa Fedha Namba (1) na Namba (2) kwa mwaka wa fedha 2013/2014 (*Statement of Reallocation Warrant No. (1) and (2) for The Financial year 2013/2014)*.

**SPIKA:** Ahsante. Ile *addendum* iliyogawiwa pale siyo uhamasishaji ni uhamishaji. Nafikiri Waziri amesema hivyo. Kwa hiyo, *Addendum* hizi mnazo, zimewekwa.

**KATIBU MEZANI (ND. JOHN JOEL):** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, shughuli zote ambazo zimepangwa katika mkutano wa 15 sasa zimekamilika.

## KUAHIRISHA BUNGE

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwenye wingi wa Rehema kwa kutupatia uzima na afya hadi kufikia siku ya leo. Tumekuwepo hapa kwa takriban miezi miwili ambapo tumeweza kupokea na kujadili Taarifa za Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa mwaka 2013/2014 na Mwelekeo kwa mwaka 2014/2015 kwa Wizara mbalimbali na hatimaye kupitisha Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2014/2015. *(Makofi)*

Napenda kutumia nafasi hii ya awali kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kazi nzuri ya kutukuka ambayo wameifanya kwa nidhamu na ufanisi mkubwa, hususan wakati wa Mjadala wa Bajeti ya Serikali na Mafungu ya Wizara za Kisekta.

Mheshimiwa Spika, kipekee niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bajeti chini ya Uongozi mahiri wa Mheshimiwa Mtemi Andrew John Chenge, Mbunge wa Jimbo la Bariadi Magharibi kwa kazi yao nzuri ya kuchambua Bajeti ya Serikali na Sheria zinazoambatana na masuala ya

Bajeti. Changamoto zilikuwa nyingi, lakini kwa pamoja tumekubaliana na kuafikiana. Kazi kubwa iliyoko mbele yetu ni kwenda kushirikiana na wananchi katika utekelezaji wa Bajeti hii ili kuwaletea maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki tukiwa hapa Bungeni, yapo matukio ya kusikitisha yaliyotokea ambapo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walipoteza Wapendwa wao. Aidha, yapo matukio ya Kitaifa yaliyosababisha kupoteza maisha ya Ndugu, Jamaa na Marafiki. Napenda kutumia nafasi hii kuwapa pole Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote waliofikwa na misiba na majanga mbalimbali, ikiwa ni pamoja na wote waliopotelewa na Ndugu, Jamaa na Marafiki.

Mheshimiwa Spika, kipekee niwape pole ndugu, jamaa na marafiki waliopotelewa na ndugu zao na wote waliopata majeraha wakati kulipotokea Mlipuko wa Bomu pale Darajani, Zanzibar. Tukio hili la kusikitisha halipendezi kwa nchi yetu. Niwaombe wananchi wote kwa umoja wetu tushirikiane kuwa walinzi katika maeneo yetu na kuwezesha kuwatambua mapema wale wote wenye nia mbaya ya kuharibu amani na utulivu katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu Waheshimiwa Wabunge walipata fursa ya kufanya uchaguzi wa Wajumbe wa Wawakilishi kwenye Bodi za Taasisi, Mabaraza na Tume za Bunge. Napenda nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Terezya Luoga Huvisa, Mbunge wa Viti Maalum kuwa Mjumbe katika Bodi ya Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere. Mheshimiwa Goodluck Joseph Ole-Medeye, Mbunge wa Arumeru Magharibi kuwa Mwakilishi wetu katika Bunge la Jumuiya ya Mabunge ya Nchi za Kusini mwa Africa (SADC-PF); Mheshimiwa Alphaxard Kangi Lugola, Mbunge wa Mwibara kuwa Mjumbe katika Tume ya Utumishi wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile Mheshimiwa Henry Daffa Shekifu, Mbunge wa Lushoto; Mheshimiwa Sylvester Massele, Mbunge wa Dole; na Mheshimiwa Zainab Rashidi Kawawa, Mbunge wa Viti Maalum wote kuwa Wajumbe katika Baraza la Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Beatrice Matumbo Shelukindo, Mbunge wa Kilindi na Mheshimiwa Dkt. Maua Abeid Daftari, Mbunge wa Viti Maalum kuwa Wajumbe wa Baraza la Chuo Kikuu cha Sayansi Shirikishi – Muhimbili; na mwisho nimpongeze Mheshimiwa Rashid Mfutakamba, Mbunge wa Igalula kuwa Mjumbe wa Bodi ya Utawala ya Chuo cha Ufundi, Arusha. Tunaamini wote waliochaguliwa watatuwakilisha vyema katika Taasisi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kupokea, kujadili na kupitisha Bajeti ya Serikali, jumla ya Maswali 321 ya Msingi na 879 ya Nyongeza yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa na Serikali.

Aidha, Maswali 37 ya Msingi na 30 ya Nyongeza yaliulizwa na kujibiwa kwa utaratibu wa Papo kwa Papo kwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuuliza Maswali ambayo yalilenga katika kuwaletea wananchi maendeleo katika Majimbo yetu na kwa Taifa letu kwa ujumla. Vile vile, niwapongeze Mawaziri na Naibu Mawaziri wote ambao wamefanya kazi kubwa ya kuandaa majibu na maelezo ya ziada katika kila swali lililoulizwa.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu, Waheshimiwa Wabunge walipata fursa ya kujadili Miswada, Maazimio na Kauli mbalimbali za Mawaziri. Miswada iliyowasilishwa na Serikali na kukamilisha hatua zote ni Muswada wa Sheria wa Fedha wa Mwaka 2014 *(The Finance Bill 2014)*; na Muswada wa Sheria wa Kuidhinisha Matumizi ya Serikali wa Mwaka 2014 (*The Appropriation Bill, 2014*).

Mheshimiwa Spika, Miswada ifuatayo imesomwa kwa mara ya kwanza:-

(a) Muswada wa Sheria wa Kufanya Marekebisho katika Sheria ya Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi wa 2014 *(The Public Private Partnership (Amendment) Act, 2014)* ulisomwa kwa mara ya kwanza.

(b) Muswada wa Sheria ya Utawala wa Kodi 2014 (*The Tax Administration Act 2014*);

(c) Muswada wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (*Miscellaneous (Amendments) Bill 2014); na*

(d) Muswada wa Sheria Mpya ya Kodi ya Ongezeko la Thamani [*The Value Added Tax Act, 2014*] unaopendekeza kufuta Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani.

Mheshimiwa Spika, vile vile, katika Mkutano huu, Waheshimiwa Wabunge pia walikubali Maazimio ya Bunge kama ifuatavyo:-

(a) Azimio la kuridhia kubadilisha Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru kuwa Taasisi inayojitegemea kiutendaji *(Tengeru Institute of Community Development (Establishment Order, 2013*);

(b) Azimio la Kuridhia Itifaki ya *SADC* ya Fedha na Uwekezaji *(SADC Protocal on Finance and Investment)*;

(c) Azimio la Kuridhia Itifaki ya Kuanzisha Umoja wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (*Protocol on the Establishment of the East African Community Monetary Union*).

Mheshimiwa Spika, Katika Mkutano huu pia Mawaziri waliweza kutoa Kauli za Serikali zifuatazo:-

(1) Kauli ya Waziri wa Maji Kuhusu Matatizo ya Uzalishaji Maji katika Mtambo wa Maji wa Ruvu Juu;

(2) Kauli ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii Kuhusu Ugonjwa wa Homa ya *Dengue*; na

(3) Kauli ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii Kuhusu Hali ya Mashine za Mionzi za Taasisi ya Saratani ya Ocean Road *(ORCI)*.

Mheshimiwa Spika, wakati wa Mjadala wa Mpango na Bajeti ya Serikali ya mwaka 2014/2015; Waheshimiwa Wabunge wamepata fursa ya kujadili na kutoa maoni na ushauri kuhusu Sera na Mikakati iliyopangwa na Serikali ya kuimarisha maandalizi na usimamizi wa utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali. Tunashukuru kwa michango hiyo mizuri ambayo Serikali inaahidi kuifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuungana na Waheshimiwa Wabunge wengine kuwapongeza Mheshimiwa Stephen Masato Wasira, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Mahusiano na Uratibu na Mheshimiwa Saada Mkuya Salum, Waziri wa Fedha kwa kuwasilisha vizuri Hotuba za Mpango na Bajeti ya Serikali na pia kutoa maelezo mazuri ya ufafanuzi wakati wa kuhitimisha Hoja hii tarehe 24 Juni 2014. Vilevile, nawapongeza Mawaziri wa Kisekta na

Naibu Mawaziri kwa kuwasilisha Bajeti za Wizara zao kwa umahiri mkubwa. Pamoja na pongezi hizo, napenda kutoa msisitizo katika maeneo machache yafuatayo:-

(a) Kuimarisha utengamavu wa Viashiria vya Uchumi Jumla; Ukuaji wa uchumi jumla ulio endelevu unahitaji mazingira ya uchumi jumla yaliyotengamaa na yanayotabirika. Mwenendo wa ukuaji wa uchumi katika miaka ya hivi karibuni umekuwa ukiongezeka na kufikia wastani wa asilimia saba kwa mwaka licha ya changamoto za upandaji bei za chakula na mafuta ya petroli katika soko la dunia. Ili kuweza kuendeleza ukuaji huu mzuri wa uchumi hapana budi kuendelea kutengamaza vigezo muhimu vya uchumi jumla, ikiwa ni pamoja na kuendeleza na kuimarisha ukuaji halisi wa Pato la Taifa na kukua kwa kiwango cha juu zaidi ya asilimia saba; kudhibiti kasi ya upandaji bei kwa kuhakikisha kwamba kiwango cha mfumuko wa bei ni chini ya tarakimu moja, ikiwezekana kisichozidi asilimia tano; na kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kupunguza utegemezi.

Mheshimiwa Spika, kutengamaza viashiria hivi kutaihakikishia nchi yetu kuendelea kwa kasi katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini hasa ule wa kipato kwa wananchi wetu wengi wa Vijijini. Tayari dalili nzuri zinaanza kujitokeza, kwani kiwango cha Watanzania walio katika umaskini kimepungua kutoka asilimia 33.6 mwaka 2007 hadi asilimia 28.2 mwaka 2012. Aidha, wastani wa Pato la Mwananchi kwa mwaka limeongezeka kutoka Sh. 516,000 mwaka 2007 hadi Sh. 1,003,000 mwaka 2012.

(b) Kuimarisha utaratibu na usimamizi wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2014/2015. Mwaka 2014/2015, ni wa Nne wa utekelezaji wa Mpango wetu wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 – 2015/2016). Ili kuhakikisha kuwa utekelezaji wa Mpango unafikia malengo yaliyokusudiwa, Serikali imeiagiza Tume ya Mipango kuendelea na utaratibu wa kukagua na kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa miradi yote ya Maendeleo ya kipaumbele na ile ya kimkakati ili kuhakikisha kuwa inatekelezwa kwa kuzingatia viwango vya ubora vilivyokubalika na inalingana na thamani ya fedha zilizotolewa na Serikali *(Value for money)*.

Vile vile, kuhakikisha kuwa Miradi hiyo inakamilika kwa wakati na pale ambapo kuna changamoto za kiutekelezaji kutoa ushauri stahiki Serikalini wa njia za kufanikisha miradi husika. Kwa upande wa miradi inayotekelezwa katika ngazi za Sekretariati za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ambayo inasimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Serikali itaimarisha mfumo wa ufuatiliaji kwa kuzingatia uzoefu uliopatikana katika mfumo wa "Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa" (*Big Results Now – BRN*).

Mheshimiwa Spika, sambamba na hatua hizo, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali imeanza kufanya mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 – 2015/2016). Lengo la mapitio hayo ni kupima hatua ya utekelezaji wa mpango na kubaini changamoto pamoja na kuweka mikakati ya maandalizi ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017 – 2020/2021).

Taarifa ya mapitio ya Nusu ya Kwanza ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 – 2015/2016), itatolewa Desemba 2014. Madhumuni ya Taarifa hii ni kuhakikisha kuwa maeneo ambayo hayakutekelezwa ipasavyo na maeneo mapya yaliyoibuka *(emerging issues)* hususan kuiandaa nchi kwa uchumi wa gesi na umuhimu wa kuimarisha ushindani wa Tanzania katika uzalishaji na biashara ya Kimataifa.

(c) Kuimarisha usimamizi wa utekelezaji wa Bajeti ya Serikali, Kutokana na michango mizuri ya mawazo ambayo Serikali imepokea kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge wakati wa Mjadala wa Bajeti ya Serikali na Mafungu ya Wizara ya Kisekta, Serikali imejipanga vizuri zaidi

kuimarisha ukusanyaji wa Mapato katika Mwaka 2014/2015. Hata hivyo, ni vyema Waheshimiwa Wabunge kutambua kuwa kwenye eneo la mapato yanayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)*, Serikali ya Awamu ya Nne imefanikiwa kuongeza mapato hayo kutoka Wastani wa Shilingi Bilioni 117 kwa mwezi Mwaka 2005/2006 hadi Wastani wa Shilingi Bilioni 800 kwa Mwezi mwaka 2013/2014. Ongezeko hilo ni sawa na Asilimia 351**.** Lengo la Serikali ni kuongeza kasi zaidi katika eneo hili hata kuzidi kiwango hiki.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuipongeza *TRA* kwa jitihada hizo, Serikali itafanyia kazi maoni mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge ya kupanua wigo wa vyanzo vya kodi pamoja na taarifa zilizopatikana zinazoonesha kwamba bidhaa nyingi zinapita kwenye bandari bubu au vituo vya forodha bila kulipa kodi stahiki. Hatua za kupunguza misamaha ya kodi zitaendelea kuimarishwa. Aidha, napenda kutumia fursa hii kuielekeza Mamlaka ya Mapato Tanzania kuongeza ufanisi wa kiutendaji na kuimarisha zaidi miundo ya ukusanyaji na ulipaji kodi. Ni muhimu, Mamlaka ya Mapato kurahisisha zaidi taratibu za kukusanya kodi kwa kuweka na kutangaza kwa uwazi kodi zinazostahili kulipwa kulingana na aina ya bidhaa na kuondokana na utaratibu wa kufanya makadirio au kutumia mwanya wa majadiliano na walipa kodi jambo ambalo linaweza kutoa mwanya kwa rushwa na hivyo kuikosesha Serikali mapato yake stahiki. Vile vile, naviagiza Vyombo vya Ulinzi na Usalama kutoa ushirikiano wa kutosha katika kudhibiti na kuzuia ukwepaji wa kodi na ushuru katika bandari zetu na maeneo ya mipakani.

Mheshimiwa Spika, ni imani yangu kuwa, tukiweka wazi kodi zinazopaswa kulipwa na tukirahisisha taratibu za kukusanya mapato ya kodi hususan Bandarini na maeneo ya mipakani, tutaweza kuweka mazingira mazuri ya kusaidia kuongeza mapato ya Serikali na kupunguza urasimu na vishawishi vya kudai Rushwa. Nashauri, Mamlaka ya Mapato Tanzania ijipange upya vizuri ili kuhakikisha kwamba jukumu la kukusanya kodi linatekelezwa vizuri na kwa weledi mkubwa. Tukiwa na uhakika wa makusanyo ya mapato yetu ya ndani, naamini tutakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mapato yasiyotokana na kodi hususan maduhuli, uzoefu wa mwaka 2013/2014, umeonesha kwamba mwenendo wa ukusanyaji wa mapato hayo hauridhishi. Kwa mfano, kuanzia Mwezi Julai, 2013 hadi Aprili, 2014; Makusanyo yasiyotokana na Kodi yalifikia Shilingi Bilioni 425.5 ikiwa ni asilimia 57 ya lengo la kukusanya Shilingi Bilioni 741.1 kwa mwaka. Aidha, kwa upande wa mapato ya Halmashauri, makusanyo yalifikia Shilingi Bilioni 252.8 sawa na asilimia 66 ya makadirio ya mwaka. Mwenendo huo nao hauridhishi hivyo, ni lazima sasa tujipange upya kuhakikisha malengo yanafikiwa.

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato yatokanayo na kodi na yasiyo ya kodi (*Non-Tax Revenue*) na ya Halmashauri kuanzia Mwaka ujao wa Fedha, Wizara zenye jukumu la kukusanya Kodi na Maduhuli pamoja na makusanyo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wakala za Serikali, Idara za Serikali zinazojitegemea, kuanzia sasa zitatakiwa kuandaa Mpango Mkakati na Mpango Kazi (*Action Plan*) wa mwaka wa kukusanya Mapato na Maduhuli yao yote na kutoa taarifa bila kukosa kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu makusanyo ya kila robo mwaka; ifikapo tarehe 15 ya mwezi unaofuata kila baada ya robo mwaka ambaye atawasilisha taarifa hiyo ya utekelezaji kwenye Kamati Ndogo za Baraza la Kazi la Baraza la Mawaziri zinazohusika kwa ajili ya tafakuri na maelekezo.

Mheshimiwa Spika, tayari Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu ameagizwa kuandaa utaratibu mzuri wa kupata Taarifa za Makusanyo ya Mapato yatokanayo na Kodi na Maduhuli kutoka Wizara na Taasisi zote za Serikali zinazojitegemea. Aidha, naagiza kila Katibu Mkuu wa Wizara, Wakurugenzi wa Halmashauri na Watendaji Wakuu wote wa Taasisi, Wakala za Serikali

na Idara za Serikali zinazojitegemea kuhakikisha zinakusanya mapato kulingana na Mpango Mkakati wa Mpango Kazi na kuwasilisha taarifa hizo kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, misamaha ya kodi. Eneo la misamaha ya Kodi limekuwa likilalamikiwa na wananchi wengi na Waheshimiwa Wabunge kwa muda mrefu. Katika eneo hili, ni vyema wananchi na Waheshimiwa Wabunge kutambua kuwa kuna misamaha ya kodi ambayo haina tija na ile ambayo ina tija. Kwa misamaha ambayo nataka niieleze kidogo nataka niiweke katika makundi matatu:-

Kundi la Kwanza, ni misamaha ya kodi inayotolewa kwa Washirika wetu wa maendeleo wanaotoa misaada katika miradi mbalimbali ya maendeleo ya wananchi linajumuisha pia misamaha ya bidhaa za sukari, mchele, mafuta ya diseli na kadhalika.

Kundi la Pili, ni misamaha ya Kodi kwa Asasi zisizo za Kiserikali na Mashirika ya Dini yanayotoa huduma kwa wananchi pasipo kutegemea kupata faida.

Kundi la Tatu ni misamaha ya Kodi ambayo hutolewa ikiwa ni Mkataba wa kuvutia Uwekezaji nchini. Kwa kawaida Misamaha ya aina hii kwa maana ya kundi la tatu, hutolewa kupitia Kituo cha Uwekezaji *(TIC)* ili kuvutia Uwekezaji katika Miradi Mikubwa ambayo tunategemea kuwa manufaa yatakayopatikana kutokana na uwekezaji huo yatakuwa makubwa sana ikilinganishwa na msamaha wa kodi uliotolewa.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Takwimu za hivi karibuni za Mamlaka ya Mapato Tanzania za Mwaka 2012/2013, zinaonesha kuwa Misamaha ya Kodi ya bidhaa za mtaji kwa Wawekezaji waliopewa Hati za Usajili na Cheti cha Hadhi ya Uwekezaji Mahiri kupitia Kituo cha Uwekezaji *(TIC)* ni asilimia 19.7 ya misamaha yote.

Kwa mfano, utafiti uliofanywa na Kituo cha Uwekezaji *TIC* mwaka 2012 kwa Makampuni Makubwa 50 ya Uwekezaji yaliyosajiliwa na *TIC*, kiasi kilichowekezwa katika kipindi cha miaka mitano (2005 – 2010), ni Shilingi Trilioni 1.7 ambapo katika uwekezaji huo, Makampuni hayo yalilipa kodi Shilingi Trilioni 1.1. Aidha, Makampuni hayo yalitoa ajira 981,000 za moja kwa moja na 112,070 zisizo za moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika,Misamaha ya kodi iliyotolewa kwa Makampuni hayo ni Asilimia Saba (7) tu ya Kodi yote iliyolipwa na Makampuni hayo. Misamaha kwa makundi mengine ikiwemo Miradi ya Wahisani mbalimbali na Asasi Zisizo za Serikali *(NGOs),* na kadhalika ni asilimia 38.6; na Misamaha kwa Sekta Binafsi ni asilimia 23.8 ya Misamaha yote iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)*.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa bado tuna kazi ya kubwa ya kuhakikisha kwamba misamaha ya kodi inayotolewa kwa Wawekezaji na Walengwa wengine nchini inatumika vizuri katika miradi iliyokusudiwa na si vinginevyo. Kwa mfano, msamaha wa kodi uliotolewa kwenye mafuta ya dieseli hatutarajii mafuta hayo yaingie sokoni badala ya kutumika kwenye mradi wa uwekezaji uliokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, hivyo, kutokana na umuhimu wa kuvutia uwekezaji nchini, misamaha ya kodi iiliyoidhinishwa na Bunge Kisheria itaendelea kutolewa kwa Wahusika. Nitoe wito kwa wote watakaopata misamaha hii kuwa waadilifu na kuitumia kwa malengo yaliyokusudiwa. Hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa yoyote atakayetumia vibaya misamaha hii. Serikali kwa upande wake itaimarisha zaidi usimamizi wa matumizi ya misamaha hii na itahakikisha inatumika kwa lengo lililokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kuondoa urasimu katika vituo vya forodha. Mwezi Februari, 2014 nilipata nafasi ya kukutana na Wafanyabiashara waliotaka kugoma kutumia Mashine za kisasa za kutoa Risiti *(Electronic Fiscal Devise - EFD)* walinieleza kwamba moja ya eneo linalowasumbua ni urasimu mkubwa katika maeneo mengi ya Vituo vya Forodha Mipakani na Bandarini hasa Dar es Salaam. Katika Vituo hivyo vya Forodha walisema zipo Taasisi nyingi za Serikali zinazofanya ukaguzi wa mizigo inayoingizwa nchini na ile inayotoka kwenda nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa Taasisi hizo ni pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)*; Idara ya Uhamiaji; Jeshi la Polisi; Wakala wa Viwango *(TBS)*; Mamlaka ya Udhibiti wa Chakula na Dawa *(TFDA)*; Mkemia Mkuu wa Serikali; Tume ya Nguvu za Atomiki; Idara ya Misitu na Nyuki; Taasisi ya Utafiti wa Dawa za Mimea na Wadudu *(TPRI)*; Kitengo cha Afya ya Mimea cha Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika; na Kitengo cha Afya ya Mifugo cha Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliweka Taasisi nilizozitaja hapa kwa nia njema ya kusimamia vizuri na kudhibiti uingizaji na utoaji wa mizigo bandarini na bidhaa zinazopitishwa katika mipaka ya nchi yetu. Hata hivyo, baadhi ya Watendaji wasio waaminifu wanatumia mwanya huo kuwalazimisha wafanyabiashara kutoa fedha zao bila kupata risiti eti kwa ajili ya kusaidia mizigo kupitishwa kwa urahisi. Aidha, nimeelezwa kuwa baadhi ya Watendaji wanatumia nafasi zao kuongeza urasimu usio na lazima ili kudai rushwa, jambo ambalo linaongeza gharama kwa wafanyabiashara na kuleta athari za kuchelewesha utoaji wa mizigo bandarini na hivyo kuathiri sifa za bandari zetu.

Mheshimiwa Spika, naagiza Wizara husika kufuatilia utendaji kazi wa vyombo hivyo kwa karibu na kushughulikia kwa haraka malalamiko mbalimbali na kupata ufumbuzi wa tatizo la urasimu katika Vituo vya Forodha. Yapo Makampuni ya Mawakala yapatayo 527 yanayofanya kazi za Mawakala wa kutoa bidhaa Bandarini na hasa bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, tunayo taarifa kuwa, utitiri wa Makapuni hayo nao umekuwa chanzo kikubwa cha rushwa na ukwepaji kodi. Serikali haikubaliani na aina hii ya utendaji wa Makampuni hayo, utendaji huo uachwe sasa. Kwa hiyo, navitaka vyombo husika kufuatilia kwa karibu sana mienendo ya Makampuni yote ya Mawakala wa kutoa bidhaa Bandarini na kuchukua hatua stahiki mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto zilizopo katika bandari zetu, napenda kutumia fursa hii kumpongeza Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe kwa kazi kubwa anayofanya ya kusimamia kwa karibu uboreshaji wa utendaji katika Mamlaka ya Bandari; hasa kupunguza muda wa kutoa mizigo bandarini kutokana na kuweka utaratibu wa kufanya kazi kwa saa 24. Namtaka aongeze juhudi zaidi ili kuimarisha utendaji kazi katika eneo hili ili kuongeza sifa kwa Bandari zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Miradi ya Matokeo Makubwa Sasa *(Big Results Now – BRN)*. Utekelezaji wa mfumo wa Matokeo Makubwa Sasa umeendelea vizuri na licha ya matatizo ya upatikanaji wa fedha, matokeo yake yameanza kuonekana kama ilivyoainishwa na Waheshimiwa Mawaziri wa Sekta husika walipowasilisha Hotuba zao katika Mkutano huu. Uzoefu tulioupata katika kipindi hiki ni kwamba, upatikanaji wa matokeo makubwa kwa muda mfupi unawezekana, ilimradi tuwe tumechagua vipaumbele vyetu kwa usahihi, tunafuatilia utekelezaji kwa karibu, na kutanzua changamoto mara zinapojitokeza.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii tena kuwashukuru Wadau wote wa Maendeleo waliowezesha kupata matokeo haya. Natoa wito kwa Viongozi na Watendaji katika ngazi zote tuendeleze kasi na umakini wa kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya kipaumbele ya Mfumo wa "Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa" ili tuweze kufanikiwa zaidi katika kipindi kijacho.

Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba katika Mwaka 2014/2015, Serikali itakamilisha mchakato wa ajira za nafasi wazi za Watumishi wa Taasisi ya Kuratibu na Kusimamia Mfumo wa Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa iliyopo Ofisi ya Rais, yaani *President's Delivery Bureu (PDB)*. Vile vile, Serikali itaimarisha Vitengo na Taasisi zote zinazosimamia mfumo huu, ikiwa ni pamoja na kukamilisha uundaji wa Vitengo na Kamati za kuratibu utekelezaji katika Wizara na Taasisi zinazotekeleza Programu ya Uboreshaji wa Mazingira ya Biashara Nchini. Serikali pia itaandaa na kutangaza matokeo ya utekelezaji wa mfumo huu katika mwaka wake wa kwanza wa 2013/2014, baada ya kuhakikiwa na jopo huru la Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, hatua hii inalenga kukamilisha mfumo wa uwajibikaji ambao ni chachu muhimu ya mafanikio ya mfumo wa Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa. Vilevile, Wizara zingine, Mikoa na Halmashauri zote zinaendelea kuhimizwa kutumia mfumo huu katika kuchambua, kupanga na kutekeleza mipango na miradi yake yote ya maendeleo kwa kuzingatia mfumo huu wa Matokeo Makubwa Sasa.

Mheshimiwa Spika, kilimo…

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kutumia Kanuni ya 28(5), naongeza muda mpaka umalize hotuba yako.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, hali ya upatikanaji wa chakula nchini imeendelea kuwa ya kuridhisha katika maeneo mengi kufuatia albaki ya mavuno ya msimu uliopita na matarajio ya mavuno mazuri katika msimu wa kilimo wa 2013/2014 ambayo uvunaji wake umeanza katika baadhi ya maeneo. Aidha, kufuatia mwenendo mzuri wa hali ya unyeshaji wa mvua katika msimu wa 2013/2014 katika maeneo mengi ya nchini, kuna matarajio ya uzalishaji mkubwa wa mazao ya chakula na hivyo upatikanaji mzuri zaidi wa chakula kwa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, hali ya akiba ya chakula katika Maghala ya Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula ni nzuri. Mwanzoni mwa mwaka 2013/2014, Akiba ya Chakula ilikuwa tani 25,452.6 na baada ya kununua tani 219,377.3, akiba ilifikia tani 244,829.9. Hadi kufikia tarehe 4 Juni, 2014 Serikali ilitoa jumla ya tani 54,845.0 kama chakula cha Msaada na Maafa ikiwemo njaa, mafuriko na operesheni mbalimbali na kubaki na akiba ya tani 189,984.9.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali ina mpango wa kuuza tani 75,000 ili kuacha Maghala wazi kwa ajili ya mazao mapya yatakayonunuliwa katika msimu mpya wa 2014/2015 na hivyo, kuyaacha Maghala ya Serikali yakiwa na akiba ya tani 114,984.9 za Mahindi ifikapo Julai, 2014.

Katika mwaka 2014/2015 Serikali itanunua tani 160,000 za nafaka na kuzijumlisha zile za akiba kutoka msimu wa 2013/2014, hivyo kuwa na hifadhi ya jumla ya tani 274,984.9 za nafaka.

Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu na wananchi kuwa Serikali kwa mara ya kwanza imefikia uamuzi wa kununua mpunga na kuhifadhi katika Maghala ya Taifa kama Chakula cha Akiba. Uamuzi huu umefikiwa kwa kuzingatia kuwa baada ya Serikali kuruhusu wafanyabiashara kuingiza mchele kutoka nje ya nchi kufidia pengo la upungufu wa mchele hapa nchini, baadhi ya wafanyabiashara hao waliendelea kuingiza mchele hata baada ya muda wa vibali vyao kwisha, hivyo kuwafanya Wakulima kukosa soko la mpunga baada mavuno kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa katika msimu huu wa mavuno, Serikali imedhamiria kuanza na hifadhi ya tani 10,000 za mpunga kwa lengo la kujiridhisha kama hifadhi ya mpunga haitakuwa na matatizo. Baada ya kujiridhisha, katika misimu inayofuata, Serikali itaongeza kiasi cha mpunga utakaohifadhiwa na Serikali kwa nia ya kuziba pengo la upungufu wa mchele iwapo hali hiyo itatokea badala ya kutegemea wafanyabiashara tu kuagiza mchele kutoka nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwahimiza wakulima kuongeza uzalishaji wa zao hili kwa vile sasa Serikali imeamua kuhifadhi mpunga kama ilivyo kwa mahindi na mtama. Aidha, niwaahidi wananchi kuwa Serikali itaendelea kuboresha miundombinu ya kuhifadhi mpunga katika Maghala ya Taifa ili kuwawezesha wakulima wengi kupata soko kama ilivyo kwa mazao ya mahindi na mtama. Naagiza kuanzia sasa Taasisi zote zinazotoa vibali vya kuingiza sukari, mchele na ngano kutoka nje ya nchi kuhakikisha kuwa wafanyabiashara wenye vibali vinatumika tu kwa muda uliopangwa na pale itakapokuwa imeamriwa.

Mheshimiwa Spika, naagiza pia kwa Wakala wa Hifadhi ya Taifa ya Chakula kuanza kununua nafaka kwa wakati ili wakulima waweze kunufaika na bei nzuri zitakazotolewa. Ni matarajio yangu kuwa Wakala pamoja na kununua nafaka kwa bei ya soko na kupitia vituo vya ununuzi, vikundi vya wakulima na mawakala, watahakikisha kuwa wakulima hasa wa mahindi wanapata si chini ya Sh.  500/= kwa kilo ambayo ni bei ya msimu uliopita ili kuwawezesha kurudisha gharama za uzalishaji kwa chakula hicho.

Mheshimiwa Spika, aidha, nawasihi wakulima wasikubali kuuza mazao yao chini ya bei hiyo. Lengo ni kuwawezesha kurejesha gharama za uzalishaji. Bei elekezi kwa nafaka nyingine pia zitangazwe kwa kuzingatia gharama za uzalishaji mapema kabla ya msimu wa ununuzi kuanza. Nichukue fursa hii kuwasihi wananchi hasa katika Kanda zile wanazouza nafaka iliyo na ubora hafifu hasa uchafu kujirekebisha na kuacha tabia hiyo mara moja, kwani kwa kufanya hivyo wanavuruga jitihada za Serikali za kusaidia Wakulima Wadogo kuinua maisha yao.

Mheshimiwa Spika, Mazao ya Asili ya kuingiza Fedha za Kigeni. Nchi yetu inayo mazao yanayotuingizia fedha za kigeni ikiwa ni pamoja na pamba, kahawa, chai, korosho, tumbaku na kadhalika. Kwa madhumuni ya Hotuba yangu ya leo nimeona nizungumzie uendelezaji wa mazao ya korosho na pamba.  Kutokana na bei ya mazao haya kuendeea kutegemea bei

katika Soko la Dunia, wakulima wetu wameendelea kupata bei za chini na zisizokuwa na uhakika kila msimu wa mauzo unapowadia.

Mheshimiwa Spika, hivyo, ni vyema sasa tukazingatia umuhimu wa kuweka mikakati ya kuhakikisha kuwa soko la ndani linakuwa la uhakika kwa mazao haya. Aidha, Serikali imekuwa ikiweka mikakati ya kusindika mazao ya pamba na korosho hapa nchini kwa lengo la kuyaongezea thamani na kuongeza tija katika uzalishaji kwenye eneo hili. Kwa kutimiza azma hiyo, Serikali sasa imejikita katika utafiti wa mbegu na miche bora pamoja na kufufua viwanda ambavyo vitatumia malighafi zitokanazo na mazao haya hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, mpango wa kufufua Viwanda vya Korosho. Uzalishaji wa korosho umeendelea kuwa tegemeo kubwa la wakulima wa Mikoa ya Kusini ya Lindi na Mtwara na pia Mkoa wa Pwani. Kutokana na juhudi mbalimbali za Serikali za kufufua zao hili, katika msimu wa 2013/2014, uzalishaji wa korosho umeongezeka hadi kufikia tani 127,939.4 ikilinganishwa na tani 121,703.8 kwa msimu wa 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ongezeko katika uzalishaji, mchango wa zao hili kwa Pato la Mkulima na Taifa umekuwa mdogo kutokana na Taifa kuendelea kuuza korosho ghafi nje ya nchi kwa zaidi ya asilimia 90 hivyo, kuikosesha nchi mapato na faida nyingine nyingi kwa wakulima. Hali hii imetokana na Wawekezaji wa Viwanda 12 vya Kubangua Korosho vilivyojengwa na Serikali miaka ya 1980 na kubinafsishwa mwaka 2004 kushindwa kuvifufua viwanda hivyo kutokana na changamoto mbalimbali ikiwemo kukosa mitaji na kuendelea kutumia teknolojia iliyopitwa na wakati.

Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako na wananchi kwamba kutokana na changamoto hizo, mwezi Februari, 2014 niliitisha Kikao kilichohusisha baadhi ya Watendaji Wakuu wa Serikali, baadhi ya Wamiliki wa Viwanda vya kubangua Korosho na baadhi ya Taasisi ya Fedha kujadili mikakati ya kufufua viwanda vya kubangua korosho hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, hivyo, Serikali kwa kushirikiana na wadau hao iliamua ifanyike tathmini ya gharama na mikakati ya kufufua Viwanda vya Kubangua Korosho hatua kwa hatua na kwa kuanzia Serikali kwa kushirikiana na Wamiliki itaanza kufufua Viwanda vinne (4) vyenye uwezo wa uzalishaji (*Installed Capacity*) wa kati ya tani 5,000 hadi 10,000 kwa mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuanzia Serikali iliamua tathmini ifanyike kwa viwanda vya Newala-I; Masasi; *Lindi Farmers* kilichopo Nachingwea; na Kiwanda cha Kampuni ya *BUCCO* kilichopo Lindi kwa ushirikiano kati ya Serikali na Kampuni ya *Oltremare* ya Italy ambayo ina uzoefu mkubwa duniani katika utengenezaji wa mashine za usindikaji wa korosho. Kampuni hii ndiyo iliyojenga baadhi ya Vwanda vya kubangua korosho hapa nchini kikiwepo Kiwanda cha *TANITA*.

Mheshimiwa Spika, tathmini hii itaangalia hali ilivyo katika masuala ya kiufundi, usindikaji na miundombinu; uwezo na madeni ya Kifedha; Masuala ya Kisheria kuhusu Mikataba mbalimbali iliyowekwa na wawekezaji hawa, Mfumo wa upatikanaji wa malighafi; na uwezo wa rasilimali watu wa viwanda hivyo.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya awali ya gharama za kufufua viwanda hivyo vinne iliyofanywa na Kampuni ya Oltremare kwa kushirikiana na Kampuni ya Agrofocus ya hapa Tanzania, ilibaini kuwa njia mbili zinazoweza kutumika:-

Kwanza, iwapo Serikali itaamua kuvifufua viwanda vya Newala I, Masasi na Lindi kwa kuvijengea uwezo wa kila kimoja kubangua tani 15,000 kwa mwaka, pamoja na cha

Nachingwea kubangua tani 7,500 kwa mwaka, kwa pamoja zitahitajika jumla ya paundi 31,280,690.

Pili, iwapo Serikali itaamua kuvifufua viwanda vya Newala I, Masasi na Lindi kwa kuvijengea uwezo wa kila kimoja kubangua tani 22,000 kwa mwaka na Kiwanda cha Nachingwea kubangua tani 7,500 kwa mwaka, kwa pamoja zitahitajika jumla ya paundi 44,185,022. Hata hivyo, kabla ya kuweka mikakati ya kupata fedha hizo, Serikali imeamua kupeleka kikosi kazi chake kutathmini tena gharama hizo na kuzilinganisha na hizo za awali kwa nia ya kushirikiana na vyombo vya fedha na Kampuni ya Oltremare ya Italy kufufua viwanda hivi. Aidha, Kampuni ya Oltremare ya Italy imekubali kutoa mafunzo kwa wazawa kuhusu utawala na uendeshaji wa viwanda hivyo pindi vitakapofufuliwa na kuisaidia Tanzania kupata soko la korosho zitakazobanguliwa. Ninaamini kabisa ufufuaji wa viwanda hivi utasaidia kuboresha teknolojia, kuongeza ufanisi, ajira na mapato ya Serikali na bei ya korosho ghafi kwa mkulima badala ya kutegemea soko la dunia pekee.

Mheshimiwa Spika, zao la pamba lina mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa nchi yetu na kuondoa umaskini kwa zaidi ya wakulima 400,000 na wategemezi wao katika mikoa takribani 15 hapa nchini. Hata hivyo, bado kilimo chake kinakabiliwa na changamoto nyingi. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na tija ndogo, matumizi kidogo ya teknolojia za kisasa na zana duni. Aidha, kuna huduma duni za ugani na utafiti, kukosa mitaji na soko la uhakika, migogoro baina ya wakulima na wafanyabiashara na uhaba wa viwanda vya kuongezea pamba thamani.

Mheshimiwa Spika, katika msimu wa mwaka 2011/2012 Serikali kwa kushirikiana na Shirika la *Gatsby Charitable Foundation* ya Uingereza chini ya ufadhili wa *Lord David Sainsbury* ilianza majaribio ya mfumo wa kilimo cha pamba cha mkataba kupitia programu ya kuendeleza zao la pamba katika mkoa wa Mara na Wilaya za Bariadi na Kibondo kwa madhumuni ya kutafuta ufumbuzi wa changamoto nilizoeleza punde. Matokeo ya majaribio yalionesha kuwa uzalishaji uliongezeka kutoka kilo 398 kwa ekari hadi kilo 558 kwa ekari na ubora wa pamba uliongezeka hadi kufikia asilimia 78 kutoka asilimia 48 za awali.

Mheshimiwa Spika, baada ya Serikali kupitia Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuanza mikakati ya kusimamia kilimo cha mkataba cha pamba, takwimu za mwezi Mei, 2014 zinaonesha kuwa Wilaya saba katika Kanda ya Magharibi zilishiriki katika kilimo cha mkataba. Aidha, takribani wakulima 90,000 wamenufaika na mikopo ya pembejeo ya kilimo cha mkataba msimu huu kupitia wachambuzi takribani 15, ikilinganishwa na wakulima 30,000 katika msimu uliopita.

Vilevile takwimu hizo zinaonyesha wakulima 140,000 ndani ya kilimo cha mkataba wamelima zaidi ya ekari 400,000 na kwamba katika msimu huu kati ya makampuni 42 ya pamba, makampuni 26 yameshiriki kwenye kilimo cha mkataba ikilinganishwa na makampuni 12 yaliyoshiriki msimu uliopita. Kwa ujumla wakulima wengi wameelezea kunufaika kutokana na kilimo cha pamba cha mkataba hasa kutokana na kuongezeka kwa kipato.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo yaliyojitokeza changamoto kadhaa ikiwepo ya baadhi ya wakulima kuuza na makampuni kununua pamba nje ya mkataba jambo lililokwamisha mfumo wa kurudisha mikopo ya pembejeo katika maeneo yaliyolimwa kwa mfumo wa kilimo cha mkataba. Hivyo, Mheshimiwa Rais alitoa maelekezo kwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya kusimamia utekelezaji wa kilimo cha mkataba kwenye zao la pamba katika maeneo

yote yanayolimwa pamba na yale ambayo yamepata huduma kutoka kwa waliowekeza, lengo ni kushirikisha wadau wengine kuainisha na kupata ufumbuzi wa kasoro zilizojitokeza katika misimu iliyopita, kupanga mikakati ya utekelezaji, kuweka utaratibu mzuri wa kulinda uwekezaji wa wachambuaji na pia kulinda haki za wakulima kwa kuzingatia mikataba inayowekwa kati ya wakulima na wachambuaji.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwakumbusha Wakuu wa Mikoa na Wilaya kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais kwa viongozi kusimamia kikamilifu kazi hiyo ili wakulima wanufaike na mfumo huu wa kilimo cha mkataba. Njia nyepesi ya kutoa elimu juu ya kilimo cha mkataba ni kutumia mashamba darasa na mashamba ya mfano. Nawaagiza Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri wasimamie vema na kwa karibu utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na tatizo lililojitokeza la baadhi ya wakulima wa pamba kuuziwa tani 1,088 za mbegu ya pamba kipara ambayo haikuota kutoka Kampuni ya Quton, kwa niaba ya Serikali napenda kuwapa pole kwanza wakulima hao, kama Serikali ilivyoahidi hapo awali, tumesitisha malipo ya shilingi bilioni 1.7 za ruzuku kwa kampuni hiyo. Aidha, Serikali inaitaka Kampuni ya Quton kutorudia makosa haya katika siku zijazo na Maafisa Ugani wasimamie kwa karibu upandaji wa mbegu hizi wakati wa msimu kwa kutoa elimu stahiki.

Mheshimiwa Spika, katika kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa tatizo hili la mbegu hafifu, Serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika inaendelea na juhudi za kukaribisha uwekezaji katika viwanda vya kuzalisha mbegu bora kipara kutoka ndani na nje ya nchi ili kuweka mazingira ya ushindani ambao utaleta ubora zaidi.

Aidha, taasisi zinazohudumia zao la pamba ziangalie kama kuna uwezekano wa kupata mbegu za pamba hata kutoka nje ya nchi kwa kuzingatia masuala ya ubora na unafuu wa bei. Nichukue fursa hii kuwakumbusha Bodi ya Pamba na wagani wa zao la pamba kuhakikisha kuwa ubora wa mbegu *(germination percentage)* unafanyiwa tathmini kabla mbegu hazijagawiwa kwa wakulima. Aidha, wakulima waelimishwe manufaa ya kutumia mbegu kipara kwamba wakati wa kuziandaa zinawekewa viuatilifu ambavyo vinaua vimelea na wadudu ambao wanatokana na mavuno ya msimu uliopita, hivyo kupunguza uwezekano wa pamba inayotokana na mbegu hizi kupata magonjwa na wadudu mapema ikilinganishwa na mbegu za manyoya.

Mbegu kipara zinaweza pia kutumika na mashine za kupandia *(planter)* hivyo kuwezesha mimea ya pamba kuota katika mstari na kwa nafasi stahili na kumwezesha mkulima kupata mimea mingi kwa ekari *(plant population)* kama inavyoshauriwa kitaalamu miche 22,222 na hivyo kuongeza tija kwa ekari tofauti na mbegu za manyoya.

Naamini kupitia ushirika na kilimo cha mkataba wakulima wataweza kuungana kupata *planter* ili kupunguza sulubu ya jembe la mkono wakati wa kupanda. Ninaiagiza Bodi ya Pamba iendelee kusimamia zoezi la wakulima waliochaguliwa kuzalisha mbegu bora kwa Kampuni ya Quton ili kuwezesha ongezeko la upatikanaji wa mbegu bora kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto zinazoikumba tasnia ya pamba na hasa kilimo cha mkataba cha pamba, nichukue fursa hii kuwasihi wakulima wa pamba ambao hawajajiunga na mfumo huu kufanya hivyo kutokana na mafanikio yaliyopatikana kwa wale waliojiunga tayari.

Napenda kuwakumbusha wagani wa pamba kusimamia ipasavyo suala la usafi wa pamba inayouzwa na wakulima ili wakulima wapate bei nzuri. Aidha, kutokana na kilimo cha

mkataba katika zao la tumbaku na mfumo wa stakabadhi ya mazao ghalani kwa zao la korosho kuwanufaisha sana wakulima wa mazao hayo, niwatake viongozi wote wanaohusika na uimarishaji wa zao la pamba kuimarisha kilimo cha pamba na suala la kilimo cha pamba cha mkataba ili kuweka utaratibu utakaomfanya mkulima kuuza pamba kwa yule aliyemwezesha kupata pembejeo na kwa kutumia mfumo wa ushirika.

Mheshimiwa Spika, kupitia mkutano mkuu wa wadau wa sekta ya pamba wa tarehe 4 Julai 2013 Jijini Mwanza, wajumbe waliiomba Serikali kusimamia uanzishwaji wa viwanda vya kuongeza thamani ya zao la pamba na utengenezaji wa bidhaa za pamba hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na azimio hilo kwa sababu hatuwezi kama nilivyoeleza kwa zao la korosho, kuendelea kusafirisha sehemu kubwa ya pamba inayozalishwa hapa nchini kama malighafi kwa vile hakutunufaishi kama nchi na wala wakulima. Hivyo, narudia tena wito wangu kuitaka Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kuhimiza uwekezaji katika viwanda vingi vya kusindika na kutengeneza bidhaa za pamba hapa nchini badala ya kuuza pamba ghafi.

Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu na wananchi kuwa katika kujiandaa na rasilimali watu kwa ajili ya viwanda vya nguo hapa nchini, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimewezeshwa kuanzisha kozi za shahada mbili za Uhandisi wa Viwanda vya Nguo na Ubunifu na Vyuo vya VETA sasa vinatoa mafunzo hayo kwa kada za chini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa msimu wa ununuzi wa pamba mwaka 2014/2015 umeshazinduliwa tangu tarehe 18 Juni, 2014, ninawasihi Wakuu wa Mikoa yote inayolima pamba kusimamia kwa karibu mambo yafuatavyo:-

Kwanza, kuhakikisha kuwa bei ya chini ya kununua pamba inakuwa shilingi 750 kwa kilo.

Pili, kuhakikisha kuwa maeneo yote ambayo Bodi ya Pamba itathibitisha kwamba hakuna mnunuzi aliyetoa huduma au mkopo kwa mkulima, yawe huru kwa mnunuzi yeyote kupewa leseni ya kununua pamba ili kuwapa fursa wakulima ambao hawapo katika mfumo wa kilimo cha mkataba kuuza bila matatizo.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu kwamba hatua hizi zitasaidia kwa kiasi kikubwa uboreshaji wa zao la pamba.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa viwanda na kulinda viwanda nchini. Maendelea ya nchi yoyote ile yanategemea sana ujenzi wa viwanda. Kwa maana hiyo, suala la ujenzi wa viwanda haliepukiki kutokana na sababu kwamba viwanda husaidia kuongeza thamani mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na mazao ghafi yanayozalishwa katika sekta zingine.

Aidha, viwanda huongeza muda wa bidhaa hizo wa kutumika kabla ya kuharibika. Vilevile mazao yaliyoongezwa thamani humpatia mkulima bei nzuri na kupunguza kwa kiasi kikubwa upotevu wa mazao. Uwepo wa viwanda pia unatusaidia kupata fedha za kigeni, kutoa ajira na hivyo kupunguza tatizo la ajira kwa watu wetu hasa vijana. Kwa maana hiyo tuna haja ya kuwepo sera na sheria mahsusi zitakazohimiza na kuchagiza uwekezaji katika sekta ya viwanda na pia kuondoa vikwazo vya kibiashara.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa viwanda nchini, ndio maana Serikali imeanzisha Mpango wa Uanzishaji wa Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo Nje yaani

*Export Processing Zones (EPZ)* na Maeneo Maalum ya Kiuchumi yaani *Special Economic Zones (SEZ)* kama mkakati mahususi wa kuvutia wawekezaji.

Katika kipindi cha mwaka 2012/2013 jumla ya miradi ya viwanda ipatayo 52 yenye thamani ya dola za Kimarekani milioni 474.37 ilisajiliwa na Mamlaka ya *EPZ* ambapo ajira 12,347 za moja kwa moja zinatarajiwa kupatikana. Aidha, katika kipindi cha Januari hadi Mei 2014 pekee jumla ya miradi 21 yenye thamani ya dola la Kimarekani milioni 121.4 inayotarajia kutoa ajira za moja kwa moja zipatazo 4,814 imesajiliwa. Katika miradi hiyo, ipo miradi inayosajiliwa kwa utaratibu wa kushirikisha Sekta ya Umma na Binafsi yaani *Private Public Partnership (PPP),* lakini ujenzi wa miradi hiyo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali imeweka juhudi kubwa katika ujenzi wa viwanda katika sehemu mbalimbali na pia kupanua wigo wa bidhaa zinazozalishwa. Kwa mfano, hivi sasa kuna viwanda vya chuma takribani 17 vinavyojumuisha viwanda vya mabati, misumari, nyaya za uzio, nyaya za umeme, bidhaa za chuma ikiwemo nondo na mabomba ya chuma kwa ajili ya matumizi mbalimbali. Lakini pia tunavyo viwanda vya kuzalisha saruji vipatavyo vitano vya Dar es Salaam, Tanga, Mbeya, Pwani na Lindi.

Vilevile viwanda vipya vya saruji vinajengwa Arusha, Dar es Salaam, Tanga, Lindi, Pwani na Mtwara. Upanuzi huu wa viwanda vya saruji vitaifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi wazalishaji wakuu Barani Afrika na hivyo kujitosheleza kitaifa na kuweza kuuza nje.

Tunavyo pia viwanda vikubwa vya kusindika ngozi saba katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Morogoro, Pwani na Shinyanga. Tunavyo viwanda vya nguo tisa katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Mara, Morogoro, Mwanza na Tanga na tunavyo pia viwanda vya sukari katika mikoa ya Kilimanjaro, Kagera na Morogoro ambavyo vyote kwa ujumla wao vina mchango mkubwa katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada kubwa iliyowekezwa katika ujenzi wa viwanda hivyo nchini, tunayo changamoto kubwa ya namna ya kuvilinda niwanda hivi dhidi ya ushindani usio halali *(unfair competition)* ili viweze kukua na kuimarika kiushindani, kikanda na kimataifa. Mathalani, zipo bidhaa au vifaa vinavyoingizwa nchini na kuuzwa kwa bei ya chini ikilinganishwa na bei ya bidhaa aina hiyo hiyo zinazozalishwa nchini.

Mheshimiwa Spika, bidhaa hizo huuzwa kwa bei ya chini kutokana na wazalishaji wa nchi zinakotoka bidhaa husika kupewa ruzuku au bidhaa hizo zinakuwa na ubora duni usiokidhi viwango vya ubora au kutozwa ushuru mdogo au kupewa msamaha wa ushuru.

Hali hii husababisha ushindani usio wa haki katika soko la ndani na ni changamoto kubwa kwa Taifa letu na Afrika Mashariki kwa ujumla. Naomba uniruhusu nitoe mifano michache ambayo itatuwezesha kuona ni namna gani tunaweza kukabili changamoto hii kwa lengo la kulinda viwanda vyetu nchini.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na saruji. Kama nilivyosema tunavyo viwanda vitano vya saruji vyenye uwezo wa kuzalisha saruji hadi tani milioni 3.8 kwa mwaka. Mahitaji ya saruji kwa sasa ni tani milioni 3.9 kwa mwaka na zipo juhudi za kuongeza uzalishaji kupitia uwekezaji katika miradi tisa mipya ya ujenzi wa viwanda vya saruji ambavyo kwa ujumla wake inatarajiwa vitazalisha tani milioni 8.3 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uzalishaji huo mkubwa, changamoto kubwa ni namna ya kuhimili gharama kubwa za uzalishaji wa saruji ikiwemo umeme, gharama za usafirishaji na

ushindani mkubwa dhidi ya saruji kutoka nje ya nchi ambayo ina ruzuku, hivyo kuvuruga soko la ndani kwa viwanda vya saruji.

Aidha, zipo taarifa za ukwepaji kodi na udanganyifu ambao umeendelea kuwa tatizo kubwa sana katika sekta ya saruji. Kwa kutambua changamoto hiyo, nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zilikubaliana kuweka Ushuru wa Forodha wa asilimia 55 mwaka 2005 na kuushusha kufikia asilimia 35 mwaka 2010. Matarajio yalikuwa ni kuvilinda viwanda hivi ili vijijenge kwa miaka mitano na baada ya hapo kuendelea kuvilinda kwa kuviweka chini ya kundi la bidhaa nyeti yaani kuwa na wigo wa pamoja wa Ushuru wa Forodha wa zaidi ya asilimia 25.

Mheshimiwa Spika, hali iliyojitokeza katika viwanda vya saruji haitofautiani sana na viwanda vya chuma ambavyo navyo vina changamoto kubwa hasa katika uzalishaji na ubora wa bidhaa za chuma. Mathalani, zipo taarifa ambazo hazijathibitishwa kwamba karibu viwanda vyote vya nondo nchini vinazalisha chini ya viwango, jambo ambalo halikubaliki kabisa.

Nilibahatika kufanya ziara Mkoa wa Mwanza ambapo nilikuta katika mradi mmoja wa ujenzi wa tanki la maji, mkandarasi alikuwa ananunua nondo kutoka Uganda kwa madai kuwa nondo zilizokuwa zinazalishwa na viwanda vyetu kwa maelezo yake zilikuwa chini ya viwango. Kiwango stahiki kinapaswa kuwa BS 406, BS 500 na kadhalika. Lakini viwanda vyetu vinazalisha chini ya kiwango hicho. Ni wakati muafaka sasa viwanda vyote kuzingatia viwango vya kimataifa ili kuepusha majanga yanayotokana na udhaifu huo na pia kuwezesha nondo hizo kutumiwa na wahitaji wote wa hapa ndani na nje ya nchi.

Ninahimiza Shirika la Viwango nchini liendelee kusimamia ubora wa bidhaa za nondo kwa maslahi ya Taifa letu. Kwa sasa kuna viwanda vya nondo takribani 15 ambavyo vina uwezo wa kuzalisha nondo tani 420,000 kwa mwaka. Mahitaji ya nondo ni tani 200,000 kwa mwaka, ikiwa ni ziada ya asilimia 40 zaidi ya mahitaji. Aidha, viwanda hivi vya nondo peke yake vinatoa ajira ya moja kwa moja ya watu 4,000 na wengine takribani 40,000 ambao siyo wa moja kwa moja.

Lakini pia tuna viwanda vikubwa vya chuma viwili vyenye uwezo wa kuzalisha mabati tani 150,000 kwa mwaka, wakati mahitaji ni tani 100,000 kwa mwaka ikiwa ni ziada ya tani 50,000, sawa na asilimia 50 ya mahitaji. Viwanda hivi navyo vimezalisha ajira ya takribani watu 16,000.

Mheshimiwa Spika, mifano hiyo miwili ya uzalishaji wa nondo na mabati inadhihirisha kwamba tatizo la uzalishaji kukidhi mahitaji halipo, bali tatizo ni uagizaji wa nondo zinazoingizwa nchini kwa kulipiwa ushuru mdogo au bila kulipiwa, na naambiwa wa asilimia 10 tu kama kodi kwa visingizio mbalimbali na hivyo kutoa ushindani usio halali kwa nondo zinazozalishwa nchini. Aidha, mabati yanayoingizwa nchini yamewekwa katika orodha ya *deemed capital goods* ambayo haiwabani watekelezaji wa miradi mbalimbali nchini kutumia mabati yanayotengenezwa na viwanda vya ndani.

Mheshimiwa Spika, tunavyo viwanda vya kusindika ngozi takriban tisa. Viwanda hivi vina uwezo wa kusindika vipande vya ngozi milioni 13.2 kwa mwaka katika hatua ya mwanzo yaani *wet blue*. Kati ya hivyo vipande vya ngozi za ng'ombe ni milioni 2.5 na vya mbuzi na kondoo ni milioni 10.7. Aidha, usindikaji wa ngozi ghafi umefikia vipande 945,596 vya ng'ombe na vipande 2,713,636 vya mbuzi na kondoo kwa mwaka 2013. Kama ilivyo kwa viwanda vya chuma na saruji, changamoto kubwa ya usindikaji wa ngozi ni pamoja na ushindani usio wa haki unaosababishwa na uingizaji wa viatu vya plastiki na mitumba ambao umeathiri kwa kiasi kikubwa uzalishaji wa viatu vya ngozi na bidhaa nyingine za ngozi nchini.

Mheshimiwa Spika, vilevile tunalo tatizo kubwa katika viwanda vya uzalishaji wa sukari nchini. Tunavyo viwanda takriban vinne vya sukari. Uwezo wa uzalishaji sukari nchini ni tani 300,000 kwa mwaka. Mahitaji ya sukari ni tani 590,000 kwa mwaka, tani 420,000 ni sukari ya matumizi ya kawaida na tani 170,000 sukari ya matumizi ya viwandani, kwa maana hiyo, kuna upungufu wa tani 290,000 sawa na asilimia 49. Kati ya hizo tani 170,000; 29% ya sukari ya matumizi ya viwandani na tani 120,0000 (20%) sukari ya matumizi ya kawaida. Kutokana na upungufu huo, Serikali iliweka utaratibu wa kuagiza na kusambaza sukari kutoka nje ya nchi ili kufidia pengo hilo kwa kuruhusu waagizaji kulipa ushuru wa asilimia 25 na pia ushuru wa asilimia 10 kwa viwanda vinavyotumia sukari kwa ajili ya matumizi ya viwandani. Vipo pia vibali vya bila ushuru kabisa vinavyotolewa wakati wa upungufu wa sukari.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu pamoja na kusimamiwa na Bodi ya Sukari Tanzania (SBT) umesababisha malalamiko mengi kuwa hatua hizi za kushusha viwango vya ushuru wa forodha zimesababisha waingizaji sukari kukwepa kabisa kodi, ikiwemo Ushuru wa Forodha na VAT. Aidha, zipo hisia kuwa sukari hiyo ambayo ni nyingi zaidi ya kiasi kilichoruhusiwa kuingizwa nchini inatokana na wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu kutumia kinyume cha sheria vibali vya Mamlaka ya Mapato Tanzania vinavyowaruhusu kupitishia nchini sukari inayosafirishwa kwenda nje ya nchi yaani *transit sugar* kwa kuibakiza bidhaa hiyo hapa nchini na sukari ya viwandani kuuzwa kama sukari ya mezani.

Mheshimiwa Spika, sukari hii inayoingizwa nchini huathiri uzalishaji na mtiririko wa usambazaji sukari ya ndani ya nchi hivyo kutishia ukuaji wa viwanda vya ndani vya sukari na uzalishaji wa sukari kwa ujumla.

Vilevile itakumbukwa kuwa Serikali kwa nia njema, tulianzisha utaratibu wa *outgrowers* ili wakulima wanaoishi kandokando ya viwanda vya sukari kulima miwa na kuuzia wenye viwanda kule Kilombero, Mtibwa na Kagera ili kuboresha maisha yao kiuchumi. Hivyo kutokana na hali ilivyo, wakulima hawa wakiwemo wakulima wa Kilombero wameshindwa kabisa kulipwa kwa wakati baada ya kuuza miwa yao kiwandani kwa vile wazalishaji wamekuwa wakiuza sukari chini ya wastani wa mauzo ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, nimeamua kuyaongea haya yote kuhusu hali halisi ya viwanda vyetu na bidhaa zinazozalishwa humu nchini ili kuona umuhimu wa kujenga viwanda na changamoto tulizonazo katika kulinda viwanda vyetu vya ndani kwa kutumia mifano ya bidhaa za chuma ikiwemo mabati, nondo, saruji na sukari. Yapo mambo mengi ambayo yanajitokeza katika kila moja, lakini jambo la msingi ni namna ya kuangalia kama tunapokuwa na mahitaji yanayozidi uwezo wa uzalishaji viwandani tuchukue hatua gani. Ni lazima kama nchi pamoja na upungufu wa bidhaa uliopo, sasa tuamue kulinda viwanda vyetu vya ndani dhidi ya ushindani usio halali kwa nguvu zetu zote. Lazima sasa tukae tuone namna ya kudhibiti uingizaji wa bidhaa ambazo zinakwamisha maendeleo ya viwanda vya ndani.

Aidha, tuangalie njia bora ya kupunguza gharama za uzalishaji, ikiwemo bei kubwa za umeme. Matarajio ni kwamba baada ya kupatikana kwa gesi tunaamini gharama za umeme zitapungua na kupunguza gharama za uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, tumeona changamoto zinazokabili bidhaa za mabati, nondo, sukari, ngozi na saruji, ninaagiza taasisi zetu zikiwemo Wizara ya Fedha, Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na taasisi za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Bodi ya Sukari, Jeshi la Polisi na Uhamiaji kukaa kwa pamoja kuangalia njia bora ya kudhibiti uingizaji kiholela wa bidhaa zinazokwamisha maendeleo ya viwanda vyetu.

Kwa maana hiyo ni vizuri sasa kuchukua hatua stahiki kulinda viwanda vyetu naomba kuhimiza mambo muhimu yafuatayo:-

Kwanza, Wizara ya Viwanda na Biashara ni lazima sasa kuhakikisha kwamba viwanda vyetu vinazalisha bidhaa zenye ubora kwa viwango vya kimataifa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) lisaidie, lakini lazima ubora uwe unalingana na viwango ambavyo vinawezesha bidhaa hiyo kuweza kuuza ndani na nje bila maswali.

Pili, Wizara ya Fedha ihakikishe kuwa bidhaa zilizomo katika kundi la bidhaa nyeti katika Afrika Mashariki haziondolewi katika kundi hilo katika kipindi kirefu kijacho hadi hapo suala la ruzuku likipatiwa ufumbuzi wenye manufaa kwa nchi changa katika Shirika la Biashara Duniani (WTO).

Tatu, Wizara ya Fedha iangalie uwezekano wa watumiaji wa *industrial sugar* wawe wanalipia ushuru kamili na kisha baadaye wapewe *duty drawback* baada ya kuthibitishwa kuwa sukari husika kweli ilitumika katika uzalishaji.

Wizara ya Fedha pia iweke utaratibu ulio bora wa uagizaji wa sukari kufidia upungufu huu kwa kutumia utaratibu kama vile *bulk importation* na kisha kusambazwa kwa usimamizi madhubuti na kwa bei maalum.

Nne, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na Bodi ya Sukari wakae na kutathmini mahitaji halisi ya sukari, ikilinganishwa na uwezo wa viwanda vya sukari vilivyopo nchini, pamoja na kukamilisha taratibu za kisheria na kimfumo za uagizaji wa sukari kuziba upungufu pale inapobidi. Aidha, ni muhimu kuhimiza upanuzi katika uzalishaji wa sukari kwa kuhamasisha uwekezaji mpya katika sekta hii.

Tano, utaratibu wa kuagiza bidhaa zitakazoingizwa nchini kuziba pengo lililopo lazima uangaliwe upya ili uagizaji huo usiviathiri viwanda vya ndani.

Sita, tathmini ya upungufu wa bidhaa unaojitokeza uangaliwe kwa umakini na kupanga njia bora ya kufidia upungufu huo, ikiwa ni pamoja na kuweka utaratibu wa vibali vya kuruhusu kuingiza bidhaa nchini. Vibali vihusishe muda ule wenye upungufu pekee. Aidha, utaratibu wa sasa wa kutumia wafanyabiashara kuleta bidhaa kwa lengo la kufidia upungufu wa bidhaa husika uangaliwe upya ili kuepuka uingizaji bidhaa kwa wingi kuliko upungufu ambako kunasababisha kudumaza viwanda vya ndani.

Na mwisho bei za bidhaa zizingatie maeneo yanayozunguka eneo la uzalishaji, kwa mfano, haitarajiwi bei ya sukari kilo moja inayozalishwa na Kiwanda cha Sukari cha Kagera au pale Moshi - TPC au hapa Mtibwa na Kilombero iwe kubwa tena sawa na bei ambayo ni ya sukari kule Ruvuma, Mtwara na Katavi.

Mheshimiwa Spika, ipo mifano kwa baadhi ya nchi duniani ikiwemo india ambazo zimejaribu kuweka nembo inayoonesha kwamba bidhaa hizi zinazalishwa nchini na bei yake ni kiasi fulani, lengo likiwa ni kuhakikisha kulinda watumiaji wa bidhaa hizo na kulinda pia vuwanda. Gharama hizo zinazingatia gharama zote pamoja na faida ambayo anaipata mfanyabiashara huyo kwa kutumia umbali mrefu.

Mheshimiwa Spika, majirani zetu Kenya wameanza kuchukua hatua katika Bajeti ya 2014 kulinda viwanda vyao, kwa mfano, Serikali ya Kenya imeongeza ushuru wa bidhaa za chuma kutoka asilimia 0 hadi 10 na kufikia asilimia 25 na kuahidi kuweka mezani Muswada Mpya wa Sheria ya Ushuru wa Forodha ili kulinda viwanda vyake. Nasi tukidhamiria hata kama

hatukufanikisha sasa tunaweza kufikia lengo hilo kwa mwaka ujao wa Bajeti. Nina hakika tukidhamiria tutaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum nchini. Sera ya elimu na mafunzo ya mwaka 1995 inasisitiza kuhusu haki ya kila raia wa Tanzania kupata elimu wakiwemo watu wenye mahitaji maalum, sera ya maendeleo ya mtoto ya mwaka 1996 inayozungumzia umuhimu wa kila mtoto mwenye umri wa kwenda shule kwenda na kupata elimu bora na sera ya Taifa ya watu wenye ulemavu ya mwaka 2004 inasisitiza umuhimu wa elimu ya watoto wenye ulemavu kutolewa katika mazingira jumuishi na rafiki.

Katika kutekeleza sera hizo, Serikali imekuwa ikijitahidi kutoa elimu bora kwa watoto wote wenye umri wa kwenda shule, wakiwemo wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa zipo shule za msingi 22 ambazo ni maalum kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum na shule za msingi 354 zenye vitengo maalum kwa ajili ya wanafunzi hao. Jumla ya wanafunzi wenye mahitaji maalum katika shule za msingi na vitengo hivyo ni 11,689. Aidha, ipo shule moja ya sekondari ambayo ni maalum kwa wanafunzi wa sekondari wenye mahitaji maalum pamoja na shule za sekondari 61 ambazo zina vitengo maalum kwa ajili ya wanafunzi wa aina hiyo. Kwa sasa, wapo wanafunzi 1,406 wenye mahitaji maalum waliopo katika shule za sekondari nchini.

Mheshimiwa Spika, tarehe 3 Mei, 2014 nilifungua maonesho ya elimu yaliyokuwa yameandaliwa na wadau mbalimbali wa elimu kwenye Uwanja wa Jamhuri hapa Dodoma. Nilipata fursa ya kutembelea mabanda mbalimbali yaliyokuwa yakionesha shughuli mbalimbali za elimu. Moja ya banda nililotembelea ni lile lililokuwa likionesha hatua mbalimbali za utoaji wa elimu maalum. Katika banda hilo nilielezwa njia zinazotumiwa kuwafundisha wanafunzi wenye mahitaji maalum hususan wasioona na nilioneshwa vifaa vinavyotumika na kuelezwa changamoto zake.

Mheshimiwa Spika, tarehe 4 Juni, 2014 nilitembelea na kukagua shule ya msingi Bwigiri ya Wasioona, Wilayani Chamwino. Katika ziara hiyo nilikagua maktaba, chumba cha kompyuta, chumba cha kutayarishia mitihani na vyoo. Niliongea pia na wanafunzi waliokuwa wamebaki hapo shuleni baada ya wanafunzi walio wengi kuwepo kwenye likizo. Shule hiyo ni miongoni kwa shule 120 za msingi zilizoko kwenye Wilaya ya Chamwino ikiwa na jumla ya watumishi 39 kati yao 25 wakiwa ni walimu. Shule ina wanafunzi 87, kati yao 61 ni wasioona na 26 wanaona.

Mheshimiwa Spika, jambo lililonifurahisha katika shule hiyo ni kuwa wanafunzi wanaohitimu darasa la saba wamekuwa wakifaulu wote yaani asilimia 100 kwa muda wa miaka 13 mfululizo. Wanafunzi hao wanaofaulu wamekuwa wakijiunga na shule maalum za sekondari kama vile Shule ya Sekondari *Diocese of Central Tanganyika* (*DCT*) - Mvumi.

Mheshimiwa Spika, tarehe 7 Juni, 2014 nilitembelea pia Shule ya Sekondari ya Mvumi DCT ambako baadhi ya wanafunzi wasioona wanasoma. Nilikutana na walimu pamoja na wanafunzi wa kidato cha pili na nne ambao walikuwa wanajiandaa na mitihani ya kitaifa ya mwaka 2014. Nilifurahishwa na kazi kubwa inayofanywa na Serikali, Kanisa la Anglikana nchini na walimu wa shule hiyo kwa kuwawezesha wanafunzi wasiiona kupata haki yao ya elimu. Nilijaribu kuuliza maswali mbalimbali, nilishangaa kuona kwamba wana uwezo mkubwa sana wa kuweza kuyajibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ziara zangu hizo zilinithibitishia kuwa walimu nchini wakiwemo walimu wa wanafunzi wenye mahitaji maalum wanafanya kazi kubwa na ya kizalendo ambayo inahitaji kuungwa mkono wakati wote.

Naomba kuwapongeza walimu wote nchini kwa kazi yao muhimu ya kutoa elimu kwa Taifa letu. Lakini nitumie fursa hii ya kipekee kabisa kuwapongeza walimu na wanafunzi wote wa shule ya msingi Bwigiri - Wasioona kwa kuwezesha mafanikio makubwa na ya kuigwa yaliyopatikana shuleni hapo. Aidha, nawapongeza wasimamizi wa elimu wa mkoa wa Dodoma, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kwa usimamizi wao mzuri uliowezesha ufaulu na mafanikio hayo kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, ziara zangu hizo ziliniwezesha kufahamu changamoto zinazowakabili wanafunzi wasioona wakiwa shuleni. Ni kweli changamoto ni nyingi, lakini kubwa nililoliona na ambalo limewagusa wanafunzi hao pekee ni lile la wanafunzi wasioona kutofundishwa somo la hisabati katika ngazi ya sekondari na hivyo, kutofanya mtihani wa somo hilo wa kumaliza kidato cha nne na kusababisha kushushwa madaraja yao ya ufaulu sawa na wanafunzi wa kawaida katika shule zingine wasiofaulu somo hilo. Lakini shule hizi zinakosa vitendea kazi muhimu kama vile *braille printer, embossing photocopy machine,* kompyuta na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ninafahamu kuwa changamoto nyingine si za wanafunzi wasioona tu bali zinawahusu pia wanafunzi wenye mahitaji maalum pamoja na walimu wao kwa ujumla. Napenda kutoa wito kwa watendaji wanaohusika na elimu maalum nchini kushughulikia changamoto zonazowakabili walimu na wanafunzi wenye mahitaji maalum pamoja na majengo ya shule zao. Ni imani yangu kuwa kila mmoja anayehusika atachukua hatua mapema ili kuwawezesha wanafunzi wasioona na wote wenye mahitaji maalum kupata elimu stahiki kwa mazingira stahiki.

Mheshimiwa Spika, uwiano wa idadi ya watu wa vijijini na mijini wanaohudumiwa na daktari. Idadi ya Watanzania inakadiriwa kuwa milioni 48.2 kati yao wanaoishi vijijini ni milioni 36.6 na wanaoishi mijini ni milioni 11.6. Watanzania hao wanahudumiwa na madaktari ni 2,311 waliopo nchini kwa sasa. Madaktari wanaoishi maeneo ya vijijini ni 523 na wanaoishi maeneo ya mijini ni 1,788.

Mgawanyo huu wa madaktari unafanya kuwa daktari mmoja kitaifa anahudumia wastani wa Watanzania 19,982. Kwa upande wa vijijini, daktari mmoja anahudumia wananchi 66,211 wanaoishi vijijini na kwa maeneo ya mijini, daktari mmoja anahudumia wananchi 6,460. Hali hii inaonesha kuwa daktari mmoja anayehudumia maeneo ya vijijini anahudumia zaidi ya mara kumi ya idadi ya watu wanaohudumiwa na daktari anayefanya kazi mjini.

Kiwango hiki cha daktari mmoja kwa Watanzania 19,982 ni kikubwa mno ikilinganishwa na wastani wa kawaida wa daktari mmoja kwa watu 10,000 kinahitaji kupunguzwa kwa kuongeza idadi ya madaktari nchini. Serikali itaendelea kugharamia elimu ya madaktari nchini na kuwawezesha kuwa na mazingira bora ya kazi kwa kuzingatia hali ya uchumi wa nchini, nia ni kuongeza idadi ya madaktari wa ngazi zote katika Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuhusu saratani ya shingo ya kizazi, Serikali imeanzisha mpango wa kitaifa wa kukinga na kuzuia saratani ya shingo ya kizazi. Aidha, Serikali itaendelea kutoa elimu kuhusu kujikinga na saratani ya awali, kupanua vituo vya kupima dalili za awali za saratani na kupatiwa tiba ya upandishaji baridi kwenye mikoa mitatu iliyobakia ya Mtwara, Rukwa na Simiyu. Huduma ya rufaa itaboreshwa kwa wagonjwa wanaofikiriwa kuwa na saratani kwa ajili ya tiba katika Taasisi ya Saratani ya Dar es Salaam. Aidha, chanjo ya kuwakinga wasichana wenye umri wa miaka 9 mpaka 13 dhidi ya saratani imeanza kutolewa katika Mkoa wa

Kilimanjaro ili kujifunza mfumo wa kutumia shule kwa ajili ya kutoa chanjo ili kuingika nchi na balaa hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla hali ya usalama katika Mipaka yote ya nchi yetu inaendelea kuwa shwari licha ya kuwepo changamoto kadhaa, mathalani katika Mpaka wa Kaskazini ambapo Tanzania inapakana na Kenya na Uganda kumekuwepo na changamoto ya wahamiaji haramu hususan katika Wilaya za Misenyi na Karagwe na changamoto ya uharibifu wa alama za Mipaka. Aidha, katika Mpaka wa Kusini pamekuwepo na changamoto ya utata wa Mpaka kati ya Tanzania na Malawi kati ya Ziwa Nyasa na changamoto ya ujenzi holela unaofanywa na wananchi waishio Mpakani eneo la Tunduma.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia vyombo vyake vya ulinzi na usalama na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kudhibiti hali hiyo ikiwa ni pamoja na kufanya mazungumzo ya pamoja baina ya wataalam wetu na wataalam wa nchi hizo jirani.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba kwa ujumla hali ya usalama ya mipaka yetu ni shwari bado nchi yetu kama sehemu ya Afrika Mashariki inakabiliwa na tishio la mashambulizi ya kigaida ambalo linawakumba majirani zetu. Serikali kupitia Jeshi la Wananchi Tanzania na vyombo vingine inaendelea kushirikiana na vyombo vyote hivyo kuhakikisha kwamba nchi yetu inaendelea kuwa salama.

Naomba nitoe wito tena kwa Watanzania wote kutoa ushirikiano wa kutosha kwa vyombo vya usalama katika kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa salama.

Mheshimiwa Spika, suala la ajali za barabarani bado ni changamoto kubwa hapa nchini likichangia vifo na majeruhi wengi na uharibifu wa mali.

Pamoja na hatua mbalimbali za kisheria, bado kumekuwa na ongezeko la ajali za barabarani mwaka hadi mwaka. Katika kipindi cha Januari, 2011 hadi Mei 2014, jumla ya ajali 78,654 ambazo zilisababisha vifo 13,375 na majeruhi 67,936 zilitokea. Hii ni idadi kubwa ya ajali, vifo na majeruhi.

Mheshimiwa Spika, zipo sababu mbalimbali zinazochangia kuongezeka kwa ajali za barabarani zikiwemo makosa ya kibinadamu, uzembe wa madereva, ulevi, mwendo kasi na uegeshaji mbaya wa magari barabarani ambayo kwa ujumla yanachangia asilimia 77 ya ajali zote zinazotokea, ubovu wa vyombo vya moto unaochangia asilimia 16 na mazingira ya barabara yaani ubovu wa miundombinu na hali ya hewa vinavyochangia asilimia saba.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na ajali za barabarani, tutaendelea kutoa msukumo zaidi katika kusimamia usafiri wa barabarani kwa mabasi, magari na magari madogo.

Aidha, mfumo wa kufuatilia mwendo wa mabasi na malori utakaodhibiti makosa mbalimbali ya usalama barabarani nao utaendelezwa. Hatua nyingine ni kuanzisha mfumo wa uwekaji nukta *(point system)* katika leseni za madereva ili kuwaondoa barabarani madereva wanaokithiri kwa makosa, kupima kiasi cha ulevi kwa madereva na kupanua wigo wa elimu ya usalama barabarani kwa njia ya televisheni, redio, simu na magazeti.

Kwa upande wa usimamizi wa sheria zilizopo, hatua stahiki zinachukuliwa kwa kuongeza usimamizi na mafunzo kwa watendaji wote wanaosimamia sheria ili kuwaongezea ufanisi na kudhibiti nidhamu yao.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ubovu wa vyombo vya moto, Serikali inaandaa kanuni za ukaguzi wa lazima. Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kimekamilisha ujenzi wa mtambo wa kisasa wa ukaguzi wa magari ikiwa ni pamoja na mitambo ya kukabiliana na uchafuzi wa hewa. Ninatoa wito pia kwa sekta binafsi kujitokeza kuwekeza katika eneo hili ili mitambo hii iwepo ya kutosha.

Aidha ni muhimu sasa kuanzisha gereji maalum kwa ajili ya matengenezo yatakayokuwa yanapimwa kwa mfumo huu. Sambamba na hatua hizo, Jeshi la Polisi pia linaandaa kanuni zitakazowalazimu madereva kubandika mkanda ang'avu kuzunguka magari makubwa ya mizigo na mabasi ili kusaidia kuongeza muonekano wa magari hayo wakati wa giza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mauaji ya walemavu wa ngozi na vikongwe, nchi yetu bado inaendelea kukumbwa na tatizo la mauaji ya watu wenye ulemevu wa ngozi na vikongwe kwa imani za ushirikina. Katika kipindi cha mwaka 2012 hadi 2014, takwimu zinaonesha kwamba jumla ya watu watatu wenye ulemavu wa ngozi waliuawa katika mikoa ya Arusha, Tabora na Simiyu na wengine wawili walijeruhiwa katika mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Spika, kufuatia matukio hayo, watuhumiwa nane wamekamatwa na kufikishwa mahakamani kwa mauaji na wengine wanne wanashtakiwa kwa kujeruhi. Aidha, katika kipindi hicho jumla ya vikongwe 1,393 waliuawa kikatili katika Mikoa ya Geita, Shinyanga, Mara, Simiyu, Mwanza, Tabora, Singida, Mbeya, Iringa, Njombe na Rukwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua ukubwa wa tatizo hili, Serikali inachukua hatua ya kuzihusisha Kamati za ulinzi na usalama za ngazi mbalimbali kuanzia vitongoji na mitaa katika mapambano dhidi ya mauaji ya vikongwe kwa kufanya mauaji ya watu wenye ulemavu na vikongwe kuwa ajenda ya kudumu katika mikutano yao. Aidha, tutaendelea kutoa elimu kwa wananchi kupitia vyombo vya habari, viongozi wa dini na watu mashuhuri katika maeneo husika ya kupunguza imani potofu zilizojengeka kwa miaka mingi. Jeshi la Polisi litaendesha programu mbalimbali kuelimisha jamii kukabiliana na uhalifu huo.

Mheshimiwa Spika, mauaji ya wanawake mkoani Mara, pamoja na mauaji ya vikongwe na watu wenye ulemavu wa ngozi katika mkoa wa Mara kumetokea mauaji ya kinyama ya wanawake kutokana na sababu za kishirikina katika kipindi cha Januari hadi Mei, 2014 hususan katika Wilaya za Butiama na Musoma. Waathirika wa matukio haya walikuwa wakiuawa kwa kunyongwa kwa kutumia khanga nyakati za mchana wakiwa katika shughuli zao na hivyo kusababisha hofu kubwa katika jamii. Jumla ya matukio tisa ya kuuawa wanawake yaliripotiwa katika kata nne za Mugangwa, Etaro, Nyegina na Nyakatende.

Mheshimiwa Spika, kufuati matukio hayo Serikali kupitia Jeshi la Polisi na kwa kushirikiana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa imechukua hatua za haraka na jumla ya watuhumiwa 15 wamekamatwa na kufikishwa mahakamani kwa kesi za mauaji.

Aidha, kikosi cha makosa dhidi ya binadamu na vitendea kazi kutoka Makao Mkuu ya Upelelezi kikiongozwa na Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Tanzania, Kamishna Isaya Mungulu walifika Mkoani Mara kwa ajili ya ufuatiliaji wa karibu wa kitaalam wa matukio hayo, timu hiyo yenye watu mahiri katika eneo la upelelezi bado wanaendelea kufuatilia matukio hayo sambamba na kutoa elimu juu ya ulinzi shirikishi wa namna ya kukabiliana na matukio kama hayo, ikiwa ni pamoja na kutoa eluimu zaidi kuhusu uhalifu huu na kufanya operesheni ijulikanayo kama "Zuia Mauaji ya Akina Mama Wilaya ya Butiama."

Mheshimiwa Spika, ninataka nitoe wito kwa Watanzania na hasa wananchi wa eneo hili waendelee kuona kuwa jukumu la ulinzi ni la kila mwananchi hivyo hatuna budi wote kushirikiana kuwafichua wale wote wanaofanya uhalifu katika jamii ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa Katiba mpya na mustakabali wa Taifa. Kama wote tunavyofahamu Bunge Maalum la Katiba lilianza majukumu yake mapema mwezi Februari 2014, ambapo katika kipindi hicho Wajumbe walikamilisha kuandika na kupitisha Kanuni za Bunge Maalum la Katiba, kufanya uchaguzi wa viongozi wa Bunge Maalum, Wajumbe kujadili Sura ya Kwanza na ya Sita ya ya Rasimu ya Katiba hiyo na Kamati za Bunge Maalum kuwasilisha maoni yao Bungeni.

Hata hivyo kwa masikitiko makubwa wakati tukiwa katika hatua za uwasilishaji baadhi ya Wajumbe wanaounda Umoja wa Katiba ya Wananchi yaani UKAWA waliamua kutoka nje ya Bunge kwa sababu ambazo hazikueleweka wakati huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wote tunafahamu kuwa Bunge Maalum la Katiba lina Wajumbe wa aina tatu wakiwemo Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Waheshimiwa Wawakilishi wa Baraza la Wawakilishi na Wajumbe 201 wanaotoka katika makundi mbalimbali.

Kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge hili ni sehemu ya Wajumbe wa Bunge Maalum ninaomba nitumie fursa hii kwa mara nyingine tena kuendelea kuomba sana kwamba sisi ambao tumepewa dhamana hii na wananchi tukubali kuibeba dhamana hii kwa utukufu wote kwa kadri Mwenyezi Mungu atakavyokuwa ametuwezesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 46 ya Bunge hilo inaeleza wazi mambo gani yanaruhusiwa na mambo yapi hayaruhusiwi, hivyo kama zipo kasoro ambazo zimetokana ama na ukiukwaji katika utekelezaji wa kanuni hiyo basi njia rahisi ni kukaa chini, kuzungumza, kukubaliana ili yale makosa yaweze kurekebishwa na siyo kutoka na kuacha programu nzima ikaachwa inaogelea hewani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchakato huu wa kuandika Katiba ambao kimsingi ni wa kisheria umeanza muda mrefu kidogo, ni matumaini yangu kwamba tutarudi mwezi wa nane ili tuweze kuendelea na kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuwakumbusha Wajumbe wenzangu wa Bunge Maalum la Katiba popote pale walipo ndani na nje ya Bunge hili kuwa kuwepo kwetu katika Bunge Maalum la Katiba ni jambo la kisheria na siyo jambo la kawaida, wala la hiari. Wajumbe wa Bunge Maalum la Katiba sote kwa ujumla wetu tunawajibu wa kukamilisha sehemu yetu kama Wajumbe wa Bunge Maalum kwenye mchakato mzima wa kuandaa Katiba Mpya.

Ninapenda kukumbusha pia kuwa Bunge Maalum la Katiba siyo hatua ya mwisho ya mchakato huu baada ya Bunge Maalum la Katiba kumaliza wajibu wake Rasimu itakayokuwa imependekezwa kwa vyovyote vile na Bunge Maalum itatakiwa kuwasilishwa kwa wananchi wote wa Tanzania waisome, waielewe na kisha waweze kuipigia kura ya maoni kuikubali au kuikataa kwa mujibu wa Sheria iliyopo ya Kura ya Maoni ya 2013.

Mheshimiwa Spika, hivyo ni vyema tukaelewa vizuri suala hili na na kwamba bado kuna wananchi wenzetu wengi kwa idadi ambao nao kwa wanasubiri haki yao ya kisheria katika kukamilisha mchakato huu kabla ya kupata Katiba Mpya hivyo tujitahidi tusiwanyime fursa hiyo.

Ninaomba nirejee kuwashauri Wajumbe wenzangu kwamba wote tuone buisara na hekima ya kurudi katika Bunge hili Tukufu ili tuwawezesha Watanzania wapate furasa ya kusikia tukijadili Katiba hiyo na hatimaye tuweze kuwapelekea mapendekezo kwa kadri tutakavyokuwa tumekubaliana. Kasoro zozote ambazo zinaweza kuwa zimepatikana katika mchakato mzima tukae chini tuzizungumze na tukubaliane namna ambavyo tutaweza kuepukana na makosa yaliyokwishafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hitimisho, changamoto kubwa iliyopo mbele yetu baada ya kuwepo hapa Bungeni kwa takribani miezi miwili ni kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali tuliyoipitisha, sisi kama Wabunge tuondoke hapa kwa lengo moja la kushirikiana na wananchi kusukuma maendeleo na Bajeti tuliyopitisha ikiwa ndiyo kichocheo kikuu.

Mheshimiwa Spika, twendeni tukasisitize umuhimu wa kuishi kwa amani, upendo na mshikamano tukiwasimamia vizuri na kuwaongoza wananchi katikma matumizi ya rasilimali hata kama ni kidogo kiasi gani nchi yetu itasonga mbele kimaendeleo na maisha bora kwa watu wetu yatapatikana.

Baada ya kusema hayo ninapenda sasa nimalizie kwa kuwashukuru wote waliosaidia kufanikisha Mkutano huu, nikushukuru kwa namna ya pekee wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika na Naibu Spika kwa kutuongoza vizuri kulingana na Kanuni za Bunge letu, aidha, nimshukuru Mwenyekiti Mheshimiwa Mussa Zungu Azzan, Mbunge wa Ilala kwa kuongeza vizuri baadhi ya vikao vya Bunge wakati wa Mkutano huu. *(Makofi)*

Ninawashukuru tena Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yenu ya dhati na yenye mantiki kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu, niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri, watumishi na wataalam wote wa Serikali waliosadia kujibu maswali, hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge na mambo mengine yanayohusiana na Bajeti hii. Vilevile ninawashukuru waandishi wa vyombo vya habari kwa kuwapatia wananchi habari kuhusu majadiliano yaliyokuwa yanaendelea hapa Bungeni wote kwa ujumla wenu ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pekee ninapenda kuwashukuru madereva wote ambao wamekuwa makini katika kazi ya kuendesha viongozi wetu, wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, wataalam kutoka sehemu mbalimbali nchini na kuwawezesha kufika hapa Dodoma kuhudhuria Mkutano huu wa Kumi na Tano. *(Makofi)*

Vilevile ninawashukuru wananchi wa Mkoa wa Dodoma wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa Mheshimiwa Dkt. Rehema Nchimbi kwa ukarimu wao kwa muda wote tuliokaa hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, nivishukuru pia vyombo vya ulinzi na usalama ambavyo vimehakikisha muda wote tumekaa kwa amani na utulivu mkubwa.

Mwisho, ninamshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah na watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa huduma nzuri zilizowezesha kukamilisha shughuli zilizopangwa katika Mkutano huu bila ya matatizo. *(Makofi)*

Ninatumia fursa hii kuwaombea safari njema mnaporudi katika maeneo yenu ya kazi, lakini pia niwaombee heri na baraka waislamu wote ambao wameanza au wanatarajia kuanza kuendelea na mfungo wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani kilaatayeamua kufanya ibada hiyo aifanye kikamilifu na kama kitabu cha Qurani Tukufu kinavyoelekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ninapena kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa liahirishwe hadi tarehe 4 Novemba, 2014, siku ya Jumanne, saa tatu asubuhi litakapokutana katika Mkutano wa Kumi na Sita kwenye ukumbi huu wa Dodoma. *(Makofi)*

Ninakushukuru sana Mheshimiwa Spika, ahsante sana na ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKINO WA AFRIKA YA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Haya hoja hiyo imeungwa mkono. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwanza kabisa nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa maneno aliyotueleza kwenye hotuba yake, amefanya *summary* ya mambo mengi ambayo yanaendelea hivi sasa.

Lakini mimi binafsi naomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kazi ambayo tumeifanya katika mazingira ambayo kwa kiwango fulani yalikuwa ni magumu kwa sababu ya ukosefu wa muda tuliozoea kufanya kazi zetu. Lakini hata hivyo tumefanya vizuri kwa sababu watu walijiweka vizuri, wakajipanga vizuri na kutoa hoja zao ambazo zilikuwa na mashiko.

Mimi binafsi ninaweza kusema kipindi hiki Waheshimiwa Wabunge wamejitahidi sana kuwa na nidhamu nzuri ndani ya Bunge kitu ambacho ninadhani tumekuwa pamoja kujifunza utaratibu mzima wa kuendesha Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, lakini jambo lingine ninataka kuwaeleza ni kwamba Kamati ya Uongozi imefikia uamuzi wa kufanya huu Mkutano tarehe 4 Novemba kwa kuzingatia kwamba mwaka huu umekuwa na maingiliano haya ya mambo makubwa kama Katiba. Kwa hiyo ratiba ya kawaida hatujaipanga kama tulivyozoea ndiyo maana Mkutano wa Kumi na Sita ulitakiwa uwe mwezi wa nane, lakini ikaonekana kuwa mwezi wa nane ndiyo tuna shughuli ile nyingine ya Bunge Maalum la Katiba ambapo Kamati ya Uongozi ilipotaka kuwa ifanywe sasa hivi ikaonekana kwamba kwa kweli watu wamekuwepo Bungeni karibu tangu mwezi Januari, kwa hiyo, ni vizuri wakapata nafasi ya kuwasalimia wananchi katika maeneo yao mwezi huu wa saba. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mwezi Novemba kama hali itakuwa kama ilivyo tutaunganisha Mkutano wa Kumi na Sita na Kumi na Saba. Kwa hiyo utakuwa ni muda mrefu zaidi kuliko vikao vya kawaida vya mwezi Novemba kwa sababu tutaunganisha Mikutano hiyo ya Kumi na Sita na Kumi na Saba. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge ninawaomba sana mtumie muda wenu vizuri kwa sababu mwaka huu una shughuli nyingi, mkienda kwenye maeneo yenu mtumie muda wenu vizuri kila siku ni siku muhimu sana katika kipindi hiki.

Baada ya kueleza hayo ninaomba pia niseme Waheshimiwa Wabunge niwashukuru ninyi wenyewe, niishukuru na Serikali kwa kuweza kufanya kazi yao vizuri ahadi nyingi mlizotoa Serikalini tunategemea mtazitekeleza kwa sababu msipofanya hivyo itarudi tena kwenu uzuri wake rekodi ya Waheshimiwa Wabunge sasa hivi imekaa vizuri. Kwa hiyo ni vizuri kila Waziri aliyoahidi hapa katika kipindi chetu hiki yakafanyiwa kazi ili tusonge mbele na tusiwe tunarudi nyuma. *(Makofi)*

Nichukue nafasi hii pia kuwashukuru wataalam wenu wote walioshirikiana na ninyi kufanya kazi tuliyofanya na mimi niwashukuru wenzangu katika Ofisi yangu kuanzia Katibu Mkuu na wasaidizi wake wote kwa kazi kubwa waliyofanya katika kipindi hiki katika mazingira ambayo pia hayakuwa rahisi yalikuwa ni magumu.

Lakini baada ya kusema hivyo Waheshimiwa niwatakie safari njema na wale wenzetu ambao wataanza mwezi Mtukufu wa Ramadhani wauchukue huo mwezi kama ni kuombea nchi yetu katika mazingira yoyote yale. Nchi yoyote inayoongozwa na Mwenyezi Mungu kwa maombi hayo ninaamini tutapata baraka za Mwenyezi Mungu katika maamuzi yetu mazito yanafuata mbele yetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hivi ninaomba kuwahoji kuhusu hoja ya Waziri Mkuu ya kuahirisha Bunge mpaka tarehe 4 Novemba, 2014.

Waheshimiwa Wabunge kwanza nitatoa hoja halafu tutaimba wimbo na kuagana.

Kwa hiyo, nitawahoji kuhusu tarehe ya kuahirisha Bunge. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Sasa ambao hawataki Bunge liahirishwe, haya mtakuwa mnakaa humu humu mpaka tutakapoonana tena.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo walioafiki kwamba Bunge liahirishwe mpaka tarehe 4 Novemba, 2014 wameshinda. Kwa hiyo sasa ninaomba tusimame kwa ajili ya Wimbo wa Taifa.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge Waliimba Wimbo wa Taifa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninaahirisha Bunge mpaka siku ya Jumanne, tarehe 4 Novemba, 2014.

*(Saa 7.55 mchana Bunge liliahirishwa Mpaka siku ya Jumanne,*
*Tarehe 4 Novemba, 2014, Saa Tatu Asubuhi)*